

Msimulizi, 1891¹

Edited and corrected by
Arvi Hurskainen
Department of World Cultures, Box 59
FIN-00014 University of Helsinki, Finland
arvi.hurskainen@helsinki.fi

Abstract

This is a corrected version of Msimulizi, the first periodical written and printed in Swahili language. The periodical was established to be an information channel between scattered mission station of the Universities' Mission to Central Africa, and also between the supporters of the mission work in Great Britain. The periodical was originally scanned and made available by SOAS (School of Oriental and African Studies, London). Obvious scanning errors were corrected. Also, clear errors in original print text were corrected. However, nonstandard spelling was not corrected, if it was possible to assume that the writer intended to write in the way it was done.

The file follows the original pagination. A page in the original publication is a page in this file. Page numbering is continuous from year to year, and it is printed at the top of the page.

This file contains the text of year 1891.

MSIMULIZI. 1891

Imepigwa chapa Kiungani, Zanzibar,
katika "Universities' Mission to Central Africa,"

HABARI ZA NYASSA.

Katika mwezi wa October nimesema nipo pa Mataka tunajenga nyumba na chuo ya kufundishia watoto wa hapo, kwani tangu zamani,

¹ The text is issued under licence CC BY-NC

wao hawajapata Mwalimu. Bassi hiyo nyumba panapo mwezi huo wa Oct. ikaisha, tukaanza kazi ya kufundisha watoto.

Hatta panapo mwezi wa Nov. bwana kasisi Johnson akaja akasema, nimepata habari yakuwa ipo njia ya kuweza kupita, bassi nyie wawili D.S. na W.E.K. nawatakeni mwende Mlikoma mkafunge vitu vyenu, kwenda Unguja. Bassi tukaja zetu Mlikoma tukafunga vitu vyetu, hatta panapo Nov. 7, tukatoka Mlikoma pamoja na watoto wanne wa huko Nyassa. Bassi sasa labda nitapenda ginsi tulivyowaacha wenzetu katika kazi zao.

I. **Likoma** - Baada ya kutoka Archdn. Maples, bwana Johnson akawa mtu wa kuja Likoma kukaa. Kwani hamna Padre mwingine awezaye kushika kazi ya bwana Maples, bassi yee akawa mtu wa kufanya kazi ile, ndio kuwafundisha waanafunzi, wasikiaji (Hearers) na Wamasihya, na kutwaa darasa za watoto wa chuoni pia, waliobatizwa na wasiobatizwa. Tena akafanya shauri na waalimu ya kuwa hawa watoto wa mahali pote tufundishapo, wengine hawataki kuja chuoni, wengine huja hukaa siku mbili ao tatu marra hukimbia, bassi mwaonaje? Mimi naona yafaa tukipeleka watoto wajuao vizuri A.B.CH. Kwenda kwa killa mji wao kuwafundisha wale waliokaa na wasiohitaji chuo kwa saa moja tu marra kurudi. Wakitoka 6. 15. a.m. na kurudi 8.0. a.m. kwa mafundisho yao wenyewe. Kwani ikiwa hivi ndio itazuia watoto kutoroka, na itahifathi chuo kurudia nyuma tena; kwani kwanza mtoto akifundishwa labda anajua A. B. CH.

MSIMULIZI. 377

zote na mwingine anajua Maandiko Matakatiifu kuyasoma, bassi hutoroka, huthani ameisha jua, bassi huenda kwake hukaa mwaka, ao miezi mingi tena hurudi chuoni, ameisha sahau, tena hana buddi mwalimu kuanzisha A. B. CH. bassi vile ikawa kazi sana kwa waalimu. Lakini sasa kwa kupeleka watoto katika miji yao na kuwafundisha wenzao, pale ajapo chuoni, hasumbui tena kwani ameisha jua A. B. CH. ao masomo mengine. Hivyo ndivyo tulivyofanya kwa killa mahali penyi School zetu na penyi watoto wajuao kusoma kidogo. Bassi watoto wale wenyi zamu yao, na kwani killa mji mmoja labda una watoto wawili wafundisha.

Siku yao hutoka huenda, na hurudi saa mbili - tayari kwa saa tatu, kwenda chuoni mwao.

Habari za ginsi kazi ya Mission ilivyo:

Humo **Mlikoma** wamo wengi sasa watakao kujua yaliyo kweli ya dini yetu, wanawake wengi huja siku ja Juma a pili pamoja na waume pia, kusikiliza mahubiri, tena wapo wake wengi kuliko waume wameingia uwanafunzi, ndio kupewa Msalaba, na waume wanaongezeka pia. Kitu kinachowazuwua sana sana ndio ya kuacha mke; na kuwa na mmoja, ndio wengi hawataki, husema, Ah, utawezaje kula vizuri? kwani mke mmoja ndio kuchoka kutupu na njaa pia kwani atakuwa akichelewa kupika, bassi wee mme utakaa pasipo chakula, heri wawili ao watatu. Ndio vema; na aliye tajiri atwae zayidi, Jumbe atwae apendavyo. Bassi hapo ndipo shughuli hatta ukawaambia je husema ah, nyie mna desturi yenu naswi yetu bassi wacheni tu; atakaye hayo maneno atakuja.

Bassi kwa jambo hilo la wanawake ndio wanaona ni kazi sana kuliacha. Wallakini hatta hivyo hutaka wengi kuingia na kupokea Msalaba wa Bwana.

Naona Xmas hii ya 1890, wamebatizwa watoto wa chuoni

MSIMULIZI. 378

na watu wa nje wengi. Hizi ndizo habari za Mlikoma.

Na zingine ndio tumeacha wanafanya njia tangu juu kwenyi nyumba hatta huko pwani kwenyi maji, na wanakusanya matofali ya kujengea Kanisa, kwani Kanisa liliopo sasa ni la miti na matete na mianzi tu bado kujenga la mawe. Kisiwa hiki cha Likoma chote kimezungukwa na vijiji vingi, na killa kijiji kina mkuu wake wa kukata maneno yaliyo madogo, kama hapo bandarini petu ikaapo S. S. Charles Janson pana kamji jina lake Mbamba hapo akataye maneno ni Adende babaye Tito Kungurukutu na mwingine Amzenje, hao ndio wakatao maneno ya hapo; bassi hivyo killa mahali. Na lugha ya humo Mlikoma kwa asili wana lugha yao sio Kinyassa, maneno yao hunena kama Kinkamanga, lugha ya upande wa pili wa bahari hiyo, lugha yao kama hivi: Mnyassa husema "Ndipache ndiwo" (nipe kitoweo,) Mlikoma atasema, "nipase dendi," tena Mnyassa "Ijani kuno," Mlikoma "Azani kuno," maana yake "Njoooni huku." Mnyassa "Iwe wakala bwanji?" Mlikoma "Aimwe mwachaa uli?" ndio "Ewe umekaaje?" bassi hivyo ndio tofauti ya maneno, lakini siku hizi wanachanganya, na cha ng'ambo ndio Kinyassa na cha Kunkamanga ndio upande wa pili wa bahari. Bassi naona baadaye maneno ya Mlikoma yatakwisha. Sasa tutoke Likoma twende kwa magaribi tutakuta kisiwa kingine jina lake:

II. **Chizumulu.** Labda mwakumbuka katika Msimulizi wa sita nilivyosema ya kuwa pana kisiwa kingine upande wa magaribi, ndio Mchizumulu humo anakaa Mr J. W. Williams, yule alikikaa Masasi, pamoja na mwalimu wa huko huko Daudi Kaingainga: naye mwalimu hodari kwa kufundisha, hatta akiwa hajahitimu kama nyie wa K. M. lakini anafanya kazi vizuri sana. Bassi habari za humo ni njema kwa kadri yake; watu huja kwa siku ya Juma a pili, wengi hujionea kama upuzi, kwani ndio kwanza

MSIMULIZI. 379

nza wasikie maneno hayo. Watoto wa chuoni wamo tele Wanaenda chuoni si wengi sana, na watoto wa humo wana akili sana kwa kusoma na Maandiko pia wanafahamu sasa, hatta kwa kujibu yale waliofundishwa wanafahamu sana. Na Mwalimu wao ni mmoja tu Daudi: pamoja na Bwana Joseph Williams. Na lugha yao ndio Kinkamanga kama vile cha Mlikoma, lakini humo hamna kuchanganya sana, kwani ni hao watupu, namo pia mna wakuu wao, lakini atawalaye visiwa hivyo viwili ni Chiteji na Mataka; hao ndio Mafumu wakuu; Humo hamna kuni wanatumia mabua ya mtama kwa kupikia, lakini vyakula vyao vinaiva upesi kama wanapika kwa kuni nzuri. Kazi ya watu kuvua samaki kwa majarifa, sawa na wa Mlikoma kazi yao ni hiyo kufanya nyavu. Hizi ndio habari za Mchizumulu, kisiwa kidogo lakini kina udongo mzuri na hutoa nafaka tele kupita Mlikoma. Kwani Likoma ni muhogo na njugu mawe tu na mtama mwekundu, lakini Mchizumulu mtama, mpunga, mawele, viazi, miwa, mihindi pia hupatikana. Sasa tutoke twende turudi huku nyuma upande wa mashariki tena, wallakini tuvuke kabisa mpaka upande wa pili kwa upande wa juu, huko aliko So Songolo panaitwa

III. **Likumbi** akaapo Mfumu Mapunda, hapo tangu pale zamani bwana Johnson alikuwa hajampata mwalimu wa kumtia, bassi safari hii So amekwenda hapo yee na mkewe, nyumba yake tulianza kujenga mwezi wa August 1890, naona sasa imekwisha kabisa. Kwani ilikuwa shidda sana kujenga upesi kwani miti na mianzi ilikuwa haipatikani upesi. Sharti mwenyewe So aende mwituni mbali kukata miti na mianzi kuja kujengea nyumba yake na ya Chuoni.

Watu wa hapo ni Wanyassa, lakini, pana mto unaitwa Unga kwa kaskazini ya mji, na upo tena mji mwingine

MSIMULIZI. 380

unaitwa Ngofi, huo unajulikana pote, hatta watu hawasemi naenda Lukumbi; lakini naenda Kungofi kwani ni mji wenyi kabila peke yake, maneno yake sio ya Kinyassa, kidogo kama Kibiza, hatta hivyo hayasikilizani, ndio ajabu ikiisha bwana wapo karibu kabisa kabisa, kama mji mmoja illa kwa sababu ya mto huo Unga ndio nayo lugha ikatengana. Bassi toka hapo kama ukishika njia ya kwenda kaskazini utaona lugha ngeni kabisa walla si Kinjassa tena, lakini sisi turudi kwa chini, tutoke kwa So ndio Likumbi, tumwache anaanzisha chuo yake, kwani adio kwanza aende huko, watoto anao labda 30 ao zayidi na wanafunzi anao pia wallakini si wengi sana.

Sasa tuende kwa inchi kavu tukipita pwani pwani, kutoka Likumbi tunakuja Pamvumu, tena Panakombo, tena Panasimba, tena Palunguwa, tena Pamlanje - ndipo akaapo mtoto huyu tuliye naye hapa Kiungani, Barnaba Uledi — tena Pauchesi, tena pa Amlekelela na mwingine pia hatta tunafika Pachigoma pa Chiteji akaapo mwalimu wetu Richard Kanyema na mkewe pia. Mle mwote nilimotaja, hamna watu wa kufundisha, watoto wamo wengi, lakini bado kupata Mwalimu. Sasa tusikie habari za Mwalimu Richard udio pa Mfumu Achiteji panaitwa.

IV. **Pachigoma**, yeye mwalimu Richard nyumba yake amejenga upande wa kaskazini wa mji ndio nyumba ya mwisho ya nje ya boma. Habari zake naona si nyingi, kwani ndio kwanza aje: watoto wa chuoni anapata wallakini si wengi hatta watoto wake pia anapata, na Waanafunzi ndio kwanza apate; kama vile mzee So. Watu wake wazuri wanatawaliwa na mafumu mawili mmoja ndiye yule mliyejua jina lake tangu zamani Achitedzi ao Achiteji, na wa pili ndiye Amkongojo babaye Mattayo Waya na Danieli Wino; watoto wasomao Likoma, Mattayo mpiga Chapa. Lakini mafumu hayo wote wazuri pia hukata

MSIMULIZI. 381

maneno kwa haki yao kama kwa kadiri walivyo.

Sasa tumwache Richard tupite njia pia ya pwani ao ya juu pia ni sawa tunavuka mto jina lake Kobwe, marra tu, tunaingia mji wa Mataka hapo walipokaa Denys S. na W. E. K. walio Kiungani sasa, bassi habari za hapo pa:

V. Mataka ni hizi nazo si nyingi sana kwani ndio kwanza waingie Waalimu kama vile Kungofi na kwa Achigoma. Mwezi wa August na Sept. nyumba ilijengwa, ikaisha, wakaanza kufundishwa watoto, watoto wa Chuoni walipatikana 38 ao 40, wajao siku zote, wengi wanatoroka hawataki kufundishwa, wala kujua. Watu wazima walipatikana kama kumi kwa kufundishwa waanafunzi. Habari za Watu njema pia, angalia Msimulizi wa kumi na tano, "habari za Mataka:" ginsi walivyo watu wake. Hapo pa Mataka wapo napo mafumu mawili, mmoja ndiye huyo Mataka na wa pili Azumani. Huyu Mataka siye yule wa tangu zamani, ni wa sasa kwani wa kwanza amekufa, lakini kwa sababu ya jina lile ndio huitwa Amataka, jina lake halisi yee mwenyewe ni Anamtungwi; ana wake wengi sana kwani ameingia urithi mali zote. Sasa tutoke tukipita pwani kwa pwani tutaona miji mingine ipo karibu karibu, kama vile pa Achimundu ni mji tena Msilila, tena Pachilola anapotoka mtoto huyu Benyamin Mtepa aliye hapa Kiungani, tena Pakango tunaponunua kuni killa siku kwa mashua yetu "Charlotte" na stima pia hununua hapo: tena mji mwingine Pautonga, napo pia pana kuni tele kwa stima, na pana Waanafunzi wa bwana Johnson, lakini mwote humu hamna watu wa kufundisha bassi apendaye Anjili hapa afanye ngesi aende. Majina haya niandikapo naona mmepata kufahamu katika Msimulizi wa sita. Bassi ukitoka Pautonga unakuja Marra, tena Mbweka, ukitoka hapo, haya nenda weeee hatta ukifika Pangoo ao pa Malila nkandwe.

MSIMULIZI. 382

bandari nzuri sana haina mawimbi makuu. Napo hapo pana Waanafunzi wa bwana Johnson, na bandari hiyo naona sasa ameisha kuinunua iwe mali ya Mission pamoja na pengine pengine. Hapo karibu kabisa na mji wa mwalimu Paul W. Mambo, haya twende tukamwone Mwalimu.

VI. **Chisanga** - Jee mwalimu Paul u hali gani? njema? jee School yaendelea sasa? Ah, vema bwana, karibu bassi hapo pana mwalimu Paul pamoja na mkewe na School yake na nyumba yake; mahali hapa pale pale alipokuwapo Aruffo Tungani na mkewe. Sasa anakaa mwalimu Paul Watoto wa chuoni si wengi sana, kama thelathini na tano tu, nao kama hawapendi kusoma, kwani hawafanyi bidii sana, hatta bwana Johnson afikapo akiwafundisha marra huuona uchungu kidogo, sababu ya watoto hao, Waanafunzi wapo wengi kidogo, mji mkubwa watu wengi ndani yake. Chini ya Makwangwara kama miji mingi mingi. Sasa tuondoke; tuzidi kwenda upande wa chini, tunafika mji mmoja mkubwa sana tuliousikia tangu zamani unakwitwa Pachia ao pa Maendaenda.

VII. **Pachia** - Jee pana waalimu? Ah, usiseme saaa? pana wawili wote wema na wazuri na wake zao pia. Ndio nani hao? Ndio Eustice Marisawa na Aruffo Tangani tuliyemthani atakuwa mpishi, wallakini sasa anafundisha sana. Jee wapo watoto? Ah, bwana, wapo tele, killa mwalimu ana watoto hamsini na zayidi wapendao kusoma na wajuao kusoma pia wamo wengi, hatta wangine wanawafundisha wenzao. Waanafunzi wapo tele na Mmasihiya mmoja (naona sasa zayidi ya mmoja) jina lake Andrea mtu mzuri, kijana swafi, hana ndevu bado. Watoto wa Chuoni wanaendelea sana, kwa kadiri wanavyofundishwa. Na watoto wanawake pia wanasomeshwa na hao wake wa Waalimu, na watoto wa kike wanajua

MSIMULIZI 383

kusoma pia kwa upande wao. Na habari za watu wa mji njema, na wenyi heshima, hawana uthia sana kwa Waalimu hao wakao hapo, illa huwasayidia kidogo kwa mambo mengine ya mji. Napo watu wengi sana wapo hapa. Ndizo habari za hapo Pachia. Sasa tutoke hapo tuzidi kwendelea mbele kwa chini, ndio mwendo wa saa mbili hivyo tunafika mji mmoja jina lake Msumba sasa tusikie habari zao.

VIII. **Msumba**, Nani anakaa hapo? Mwalimu Augustine Ambali na Daudi Benyamin na Philip E. Yabom. Jee Murphy M. yuko wapi? Ah, bwana, amepanda juu kule kabisa upande wa Likoma anakaa mji ule ulioachwa na akina Denys, bassi yee kaenda kukaa hapo kwani D. S. na W. E. K. wameenda zao Unguja kusoma tena. Bassi ndivyo hivyo yee akaletwa hapo, mahali pake ao ameingia P. E. Yahom. Mwalimu je Augustine anafanyaje? Ah bwana kazi nyingi, yee ndiye adumuye katika kazi ana Wamasihya wa hapo. Bassi yee Augustine kazi yake ndio kufundisha watoto wa chuoni na watu wakubwa Wamasihya na watakao kuwa Wamasihya; tena huenda huko na huko katika mji, kuongea na wakubwa wa mji. Hapo pana mafumu mawili na zayidi walio wakubwa, wa kwanza ni Mfumu Masumba lakini huyu hamjui vema kwani jina lake halitokei nje kama la huyu wa pili Amasanche anayeangalia sana Mission yetu na waalimu wote wamjua yee sana, tena yee si mkubwa kwa kimo wala kwa ufumu wake? lakini anajulika pote sababu ya ukali wake na anavyojua kukaa vema na watu sana. Mwingine wa tatu ni Amchakeni naye huyu naona karibu mtamfahamu sana, kwani ni mtu wa moyo swafi na anapendana na mwalimu Augustine. Habari za watu wa mji hodari sana nao hupigana kwa mishale na pindi tu, huwashinda Wangoni Makwangwara marra kwa marra. Hatta kuwa chini ya

MSIMULIZI. 384

Makwangwara wanakataa sana, sijui siku hizi labda Watakubali, kwani Wangoni wamenyang'anya watu wengi sana waliokwenda mashambani na mweituni kukata miti ya nyumba, ndizo habari. Bassi miji yote hii niliyotaja ni ya Wanyassa watupu isipokuwa ule wa juu kabisa wa Kungofi ndio wa kabila mbali. Lakini hatta hawa wakiwa Wanyassa watupu usithani kama ni sawa kabisa, la, yamo maneno mangine yasio sawa sawa: yanaachana kwa harufi na pangine kwa maana yake pia yanaachana.

Sasa tukitoka hapo tutaona miji gani? Miji ya Wayao isipokuwa Mluluke na Lusewa ndio ya Wanyassa, lakini Mtengula, Chikole, Ngolokolo, Mapanje, Makanjila, Makandanje na Mponda akaaye mlangoni mwa mto Shire, hawa wote ni Wayao, na Wanyassa wamo lakini si wengi sana. Na kama ukitaka habari zake soma Msimulizi wa sita ukurasa wa 84 - 88, utaona habari za killa mji ya hii niliyotaja. Miji hii yote ni ya upande wa mashariki wa bahari hiyo ya Nyassa; ndio habari. W. E. K.

HABARI ZA PA MATAKA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi Salaamu. Kweli usithani nimekusahau wee ndugu yangu Msimulizi, la! Wala sijakusahau illa sababu ya kuwa si mtu wa mahali pamoja. Panapo mwezi wa August hatta Oct. tulikuwa, tukijenga nyumba kwa mfumu mmoja jina lake Mataka ng'ambo hii ya bahari ya Nyassa. Bassi nyumba hii ilikuwa zamu kwa zamu kwa kujenga, Juma moja D. S. na C. Kathibeni; na Juma ingine Philip E. Yahom na William E. Kanyopolca. Bassi ndio ikawa shughuli kuandika barua kwani hatta dakika hapana ya kuenda huko na huko sikupata kwa sababu ya uthia wa watu wa kujenga kwani wakaidi, hawafanyi kazi haraka. Hatta Bwana Johnson

MSIMULIZI. 385

akaona uchungu kwa nyumba kuchelewa. Bassi ndugu wee Msimulizi ntajaribu safari hii kukupa habari kidogo za hapa pa Mataka.

Watu wake hodari kwa kuoneana wenyewe, lakini kama akija aliyewazidi mashauri mia mia. Leo hivi Oct. 13, 1890; simba ameingia katika matete, na simba huyu usithani kama wa leo ao jana, ni wa siku zote. Anakamata ng'ombe, mbuzi, watu, killa ghasia apatacho machoni pake. Bassi leo hivi amekamata mbuzi zizi zima kama asharini ameziua na amekula tatu tu, akaja hapa petu, ng'ombe ameikata shingo inazimia moja ameichukua akaingia nayo mateteni. Bassi asubui huu watu, haya twendeni kumsaka, wapi bwana hawakumweza. Tukaingia mateteni, nyama ya ng'ombe tukaikuta nzima; illa moyo na maini amekula, bassi tukamnyang'anya, yeye mwenyewe akaingia mateteni, Haya jamani twendeni, ah, wapi bwana, nami nikajaribu kuwashawishi, wapi bwana vile vile, A-h, illa nussu tukaenda nao, hatukumwona. Bassi tangu asubui hatta sasa jioni hii jua linaingia naye simba yupo papa hapa mateteni hatta kumwingilia tena hawakumwingilia, kwa woga wao. Na leo hivi milango itafungwa mapema, sababu ya simba huyu kuwa papa hapa: ndio habari za hapa petu.

HABARI ZA MAGILA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi Salamu. Baada ya salamu nakuarifu kama mtapenda kusikia habari ya mtu mmoja Mwenyi Hatibu. Kwanza mtoto wake akaleta barua hapa (anakaa Mwarongo) ya kusema kama ataka asayidiwe sana, kwani yeye ni mzee na mali yake ni mengi; aogopa Wadachi labda hawatamsayidia kama akinyang'anywa mali yake, ao wadeni wake hawatamlipa, bassi watoto wake akiisha kufa watataabika na mali yake

MSIMULIZI. 386

yatapotea. Bassi wakaambiwa ni heri waje siku ingine ajapo Padre Woodward (alienda Nkologwe), ndipo atafanyia mashauri, lakini hana budi atasayidiwa kwani yeye ni mtu wetu.

Baada ya siku nane nathani ikaletwa barua kama yule mzee amekufa. Ni mtu aliyekuwa kiongozi zamani wa kuleta Wapelekwa huku Bonde katika hao walioanza: tena ni rafikiye sana Bwana Askofu Steere, alikuwa hodari sana kuleta watu huku, hatta wakati huu uliopita amesayidia sana katika Upelekwa, marra nyingi huleta zawadi kwa Wazungti hatta watoto, ikiwa chakula ao mavazi pia; hatta katika mambo ya Wazungu walioleta kwanza upelekwa huku limo jina lake "Mwenyi Hatibu."

Katika Dec. 1, Siku kuu ya Andrea tukatawanyika wote. Wangine wakaenda Misozwe ha Bwana Boberts, wangine wakaenda Mkuzi pamoja na Bwana Bore, wangine wakaenda kwao; jioni wakarudi wote hapa. Dec. 16 Akaja Bwana mkubwa wa Pangani aitwaye Yohanis na wenzake wawili na askari haba. Assubui akaingia School yetu na kuangalia kazi wasomazo watoto, tena akaenda zake Pangani.

Dec. 19, Assubui ya leo tumebadili nguo zetu, wote tukashika njia na Mwalimu wetu Bone kama mwendo wa mayili tatu, tukampokea Bwana Askofu tukaja naye kwa furaha na nyimbo: watoto wakacheza sana tinge, tukapata siku nzima ya kucheza tu kwa kumfurahia Bwana Askofu. Katika siku kuu yetu ya Uzaliwa ilitawi sana. Sala ya Usharika Mtakatifu walishariki watu 85, bado wangine hawakuja. Sala ya pil, Loooo! watu wengi sana. Watoto wake walijipanga na kuchukua bandera yao, wakaingia kanisani wakiimba "Njoooni furaha" &c. Na watoto waume pia wakaingia wawili wawili wakatoka School: Kanisa lilijaa kabisa hatta tukazidisha meza zingine. Siku ya pili

MSIMULIZI. 387

yake ndio Ijumaa tukaenda watoto wote kushinda mahali pengine pengine, ndio mto Mnyodo lakini kwa juu kabisa upande wa mangaribi.

Dec. 27, ndio Juma a mosi. Watoto wote wa School za nje na wa hapa wakakusanyika hapa, waume na wake, kama Potwe, Zimbili, Kiole, na hapa; wakaja asubui wakiimba nyimbo: wengi sana. Kwanza wakapelekwa mahali pa mpila wakashindana zawadi, hatta wanaake pia. Athuuri wakarudi nyumbani kwa karamu yao. alasiri wakarudi killa mtu kwake. Dec. 29; Watoto wote wakapewa ruhusa kwenda kwao asubui, wakakae killa mtu siku nane.

Katika Jan. 2, akaja Padre Davies akitoka Unguja, anakaa hapa sasa, akaja pamoja na mwalimu Samuel Sehoza ajaye kutembea kwa mwezi. Jan. 4, Juma a pili hii walitiwa mikono watu 13, wake sita, na watoto wa hapa nyumbani watano na watu wawili tena: watoto wa nyumbani ndio, John L. Mwaimo, Edward Kingodi, Mikael Mfuko; Herbert Mkande, na Nikolas Mhina. Jan. 5, Watoto wakarudi hapa tena, wakitoka kwao.

Katika siku kuu ya Wonyesho, ikafanyika Sala ya Ubatizo asubui mbele ya Usharika Mtakatifu, wengi waliokuja kushuhudia. Watu 20, watoto wa kike wawili, na waume 18: na hawa mna watoto wetu wa nyumbani, ndio Yakobo Chamdangwe, William H. Chala, na Alfred Chambo tena ikafuata sala ya Usharika Mtakatifu.

Katika siku kuu hii ya Wonyesho athuuri ilikuwa karamu kwa waalimu wote wa Bonde waume na wake: kwani wote waliitwa na Bwana Woodward. Karamu hiyo nathani mtacheka kidigo. Ginsi ilivyo na vitu vingi na sio kula kwa vidole illa Kizungu, na ginsi watu walivyo wengi, bassi mwenzetu mmoja akaiita "A wonderful feast."

Jan. 7, Padre Woodward na Bwana Mallender wakatoka

MSIMULIZI. 388

hapa assubui kwenda Unguja. Padre Woodward atafika Hindi, atarudi tena; lakini amechukua watoto 13 atawaacha Kiungani wasome kwa mwaka tena warudi. Pamoja na mwalimu Archie A. Semanyi na Alfred Juma waliokuja kutembea tu kwa mwezi, sasa wanarudi tena kusoma.

Katika kazi ya Masisters wamepata waalimu wawili sasa, mmoja niliyemtaja zamani Josephine Mamkuna, na mwingine ndio Elizabeti Nkunde.

Nathani mtapenda kusikia habari hii, kama Bwana mkubwa wa Pangani Yohanis anapenda killa Msimulizi. Jan. 14, Bwana Askofu akaenda kumtia Mikono Elizabeth Madelu kwenyi kijiji chake; kwani yeye ni mzee sana hawezi kuja hapa Kanisani.

Jan. 21, Akawasili Bibi mwalimu Bonde akiletwa na Bwana Faulkner, pamoja na Mwalimu Wilfred Madudu. Jan. 26, Bwana Faulkner na Wilfred Madudu wakarudi tena Unguja. J.B.M.

HABARI ZA MISOZWE.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi Salamu. Baada ya salamu nakuarifu habari chache za thaifu zetu.

Hapa ilikuwa mashindano ya michezo kwa watu wawili, moja Wila na moja Kidatu, mkuu wa Kidatu Arthur Kimwaga, mkuu wa Wila Kakucha, na mashindano yote burre tu, hapana jawabu lolote illa sifa tu. Bassi wakaendelea na mashindano yote kwa siku 21, na hao wakuu wao wamepata sasa madeni mengi ya vyakula vya watu walivyokopa kuwalisha watu wao. Hatimaye akaja baba mmoja wa Wila akasema, sitaki watoto wangu washike mashindano wa kipumbavu kama huu, bassi sitaki, Kusema hivyo akamtwaa mwanawe, mashindano ndipo tena yakavunjika illa fayida hapana wala chochote.

MSIMULIZI. 389

Tena ilikuwa karamu ya Kanisa letu Luka Mtakatifu, Walikuja watoto wa Magila 40, Mr Roberts na Mr Bone. Assubuhi wangine Wakaenda tembea Tanga na kati yao watoto wangu wawili Hiza na Senkalekwa. Mwombeni Bwana wa Mavuno apeleke watendao kazi mavunoni mwake.

Otc. 29, siku hii tukasikia jambo la huzuni siku nyingi hatupati mvua, Wabondei wakafanya shauri kwenda kwa mlima ule Mlinga ndio walioamini zamani wakaenda watoe sadaka wakachukua pamoja nao ng'ombe 7 na kondoo 2 watoe sadaka wapate mvua, mahali pa kumtafuta Muungu wa kweli;

Bassi kazi yetu kwakumbuka watu hawa si kosa lao illa wanapapasa tu bassi. Bassi mvua ikanya ilianza siku ya Simani na Yuda Mit. Adui zetu wa mwili wamepata njia yao ndio simba na chui hatukulala hatta kidogo kwani wakati wa mvua ndipo huja karibu na mji hulia.

Siku ile ile sehemu ya juu ya majani ya kanisa letu lilioezekwa kwa majani tangu hapo ikaanguka usiku saa 9. Siku moja akaja Mdoicha mmoja aitwa Oswald, alijia kusudi kwenda Mlinga, naye mtu wa upole sana.

Assubui akapanda Mlinga saa 5 akarudi saa nane unussu akaenda zake, akawapa Watoto wa hapa killa mmoja pesa 12.

Mwakumbuka mateso ya Misri, mangapi? 10, bassi lile la 8. Tena mwakumbuka askari wenyewe wa Muungu walioenda kumtesa Farao askari washujaa sana ndio nzige hawaogopi hao hodari sana.

Leo hivi athuuri inapiga sawasawa twaona hewa yote imefunikizwa nao hujui waendako, marra wanaanza kutua mlima wetu wote na mipaka yake yote imefunikwa

MSIMULIZI. 390

nao tunao; illa wanaanza sasa kula nafaka yetu kwani sasa tumepanda. Ndio viyoga vingine vikubwa bassi watu Ah furaha borra hatta vijana na wazee assubuhi wamejaza makapo, furaha bora hiyo, M. F.

TOKA KIUNGANI KUFIKA UYAO.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi Salamu. Baada ya salamu nataka kukuarifu habari ya safari yetu. Tuliingia ndani ya meli ya Wadachi kutoka Unguja, tukafika Saadani, halafu tulitambaa pwani kwa pwani tukaiona Bagamoyo kwa mbali. Tukafika Daressalaam saa kumi unusu, na mahali hapa ni pazuri sana kwa bandari yake; kwani merikebu zafika pwani kabisa. Tukaiona nyumba ya Mission ya Wafransa, juu yake ina misalaba miwili. Tukalala, assubui tukatoka tukafika Kilwa, tena tukatoka tukaendelea mbele hatta tukafika Lindi, tukawa na furaha sana kwani ni njia ya kufika kwetu Newala.

Bassi tulipoingia mashuani, mashua yetu ikakwama penyi fungu la mchanga, lakini hatukupata hasara kwani maji yalikuwa yanajaa ikatoka. Na tulipofika kule Lindi tukamkuta Dr. Smith hajarudi kule alikokwenenda kutembea, tukawakuta watu watatu wa Mlolela waliokuja hapa kufanya kazi kwa Mdachi, ndio Isaak Asasu, Sulemani na Kaupunda, hawa wakatueleza habari za uthia ginsi ulivyokuwa mwingi kama Machemba anazuia njiani, na akiiona safari ya Mzungu ataipiga. Dachi aliopo Lindi akatukataza tuisafiri mpaka arudi Dr. Smith, na kusikiliza kwanza habari zilivyo huko alikokwenda. Marra Edwin Ramathani akaja akitoka Masasi pamoja na wapagazi wachache, halafu wapagazi wakaenda zao pamoja na Yustino Mkandu; Mr. Taylor akabaki hapa pamoja naswi. Jioni tukaona meli ile ile tuliyoingia inakuja ikitoka Mikindani

MSIMULIZI. 891

imempakia Dr. Smith na askari zake waliokwenda naye kutembea. Sisi tulikuwa forthani, tulipoinua macho tukamwona mfungwa mmoja amechukuliwa na askari, tulipozidi kumchungulia marra tukamtambua ni mtu wa kwa Chisanga, ndiye aliyeanza kuwafanyia ujuvu Wadachi, jina lake Lochela. Siku ile ile Dr. Smith akaingia melini akaenda zake Unguja.

Juma a pili Mr. Taylor akawahubiria watu wa Lindi kidogo Mabaniani na watu weusi.

Tena Edwin Bamathani akatujia na wapagazi, tukapata ruhusa ya kwenda, tulipokwenda mwendo wa saa sita tukamkuta Daudi Chiwelime na wapagazi wa Mlolela, tukafika Suwala tukalala, assubui tukatoka, tukamkuta P. Kamdaya anarudi Masasi kwani alitumwa na Mr. Taylor aende alete wapagazi wa Newala na Mlolela wachukue mizigo yetu. Tukafika Lilonga tukapika chakula cha athuuri. Tukaondoka tukaenda tukafika mahali pa hatari ya Machemba, ndipo walipowapigia bunduki Madachi alipokufa Charles Sulemani, lakini hatukukuta hatari. Usiku tukafika mto Sukulezi tukauvuka na mienge yetu tukalala. Juma a pili tukafika Sikolombe tukashinda hapo Juma a tano Daudi akatukuta akitoka Lindi aenda Mlolela. Bassi nikamwomba Bwana Taylor nifuatane naye mimi na Barnaba Mtaula na Arthur Kasembe, kwani njia ya Mpatila haina hatari sasa. Akatupa, bassi tukaenda, tukalala Mpatila. Assubui tukatoka tukafika mto Chitangali tukaoga, tukaenda tukamkuta mtu jina lake Makusanya na bunduki yake, alipelekwa na mzee Barnaba Nakam, kama akituona apige bunduki, ndio ishara kama tunakuja. Bassi alipotuona akapiga bunduki yake, tukamkuta wa pili ana bunduki yake, jina lake Wemba, naye pia alipelekwa, kwani Barnaba Nakam alipita njia ingine kuja kutulaki. Na huyu Wemba akaipiga bunduki yake.

MSIMULIZI. 392

Barnaba Nakam akasikia, akatujia tukakutana naye, ikawa ghasia nyingi sana ya watu waume na wake wakija kutulaki, na bunduki zapigwa za furaha. Tukafika nyumba ya Mission, Bwana Cecil akatukaribisha, na Alhamisi Artliur Kasembe akaenda Newala. Bwana Cecil ameanza Station ingine ndio Miwa, anakaa Mikael Hamisi, na mimi napelekwa kukaa pale pamoja na Mikael Hamisi. S.H.C.

HABARI ZA MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu kama mwezi wa November 30 tumepata Bibi mmoja aliyekuja pamoja na Bwana Askofu, naye ni mganga kazi yake, tumefurahi mno kwa kupata mganga hapa, aitwa jina lake Miss Margaret Caffin.

Siku kuu ya Kuzaliwa Bwana December 25 siku ya Alhamisi hatukwenda mahali tulikaa papa hapa, furaha zetu tulifanya hapa tukifanya Sala kubwa, na watu 159 wakashariki Kanisani mwetu. December 27 Juma a mosi tukaenda Kiungani kushinda; saa nane tukaenda Mnazi Mmoja kutazama mashindano na michezo mingine kiisha tukarudi killa mtu kwake.

January 1 Alhamisi kulikuwa michezo hapa petu na pamoja na kuimba wakaja Wazungu na Waalimu wa Kiungani kutazama.

Na siku hizi twawatazamia Miss Ruth Berkley na Blandina, nao wameingia marikebuni January 19, tukafurahi kusikia kama wanarudi tena Unguja twapenda kuwaona.

January 6, siku ya Juma a nne Wonyesho wa Bwana, tukaonyeshwa sanamu, mahali anapomiliki mfalme Victoria, na Victoria mwenyewe, sanamu za kuchekesha zingine. December 8 tumepata habari za safari ya ndugu yetu Kathleen na watoto wake na wengine waliosafiri kwenda Nyassa, walipofika Kumpea ametuambia hivi. Walipata

MSIMULIZI. 393

mwendo mrefu sana, Jumaa pili mchana kutwa walipata mvua mashuani walifika mahali anapokaa Mhindi wakatua mashua zao wakashuka, wakaenda pa Mhindi, akawakaribisha vizuri akawapa nyumba, wakakaa. Marra yule Mhindi akaja tena akawafukuza mvuani akafunga nyumba aliyowakaribisha wale. Mr. Lewis akamsihi wakae akakataa akawafukuza marra tatu kwa mwisho akatoka Mr. Lewis na wote pia, wakaingia mashuani vile vile; na mvua yao siku ya pili wakafika Kumpea. Tena January 22 tumempata Shemasi mmoja jina lake Mr Carnon, twafurahi mno kupata Mngoje mgine hapa kusayidia kazi kwani hatuna wengi illa Wangoje wawili. R.W.

HABARI ZA KIUNGANI.

December 24, Tulianza kupamba nyumba yetu, tangu asubui hatta athuuri; na alasiri ikawa kazi ya kusafisha Kiungani kwa kufagia na kulima majani ya njiani. Saa kenda unusu tukaenda kanisani kufundishwa nyimbo hatta saa kumi urobo tukaisha.

Jioni ikawa sala kubwa ya siku kuu ya Kuzaliwa Bwana wetu.

December 25, Kuzaliwa kwa Bwana wetu, ndio siku ya furaha kuu, kwanza sala za ibada yetu zilitendeka papa hapa wala hatukuenda Mkunazini. Saa kwanza kengele zikapigwa, ziliponyamaza, tukaingia kwa shangwi ya kumsifu Muungu kwa kuimba; kiisha ndipo ikaanza sala ya taratibu ya Usharika Mtakatifu, hatimaye ilipoisha tukatoka. Tukapewa chakula chetu cha asubui, tukaenda kucheza. Halafu saa nne kengele zikapigwa tukaingia kanisani tukiimba, halafu ndipo ikaanza sala ya Assubui, ikaisha. Athuuri tukapewa chakula chetu, tulipokwisha tulikaa papa hapa wala hatukujinyosha mahali.

December 26, Siku kuu ya Stefano Sh. wa kwanza, tulikaa papa hapa, hatta saa nane tukaenda Ziwani mahali

MSIMULIZI. 394

tunapochezea mpila: ndipo siku hiyo tulijiweka tayari kwa mashindano ya Mnazi Mmoja; kwanza tulishindana kupiga mbio, tena kurusha mpila kwa teke, tena kuruka; nao walioshinda walipewa zawadi: Kiisha wakachaguliwa watu sita watakaoshindana kwa mbio Mnazi Mmoja, tulipokwisha tukarudi hapa.

December 27, Siku kuu ya Yohana Mtume na Mwanjilisti, ilikuwa mkutano hapa Kiungani, wageni wengi wakaja, hatta saa tano tukapewa chakula chetu, tulipokwisha tukakaa kidogo. Saa nane kengele ikapigwa, wote toka hao wageni hatta nani, wote tukakutana Mnazi Mmoja, na watu walijaa wengi wengi, na palikuwa na kibanda kikubwa kwa upande wa kilimani chenye milingoti mitatu Mngereza, Mmarikani na Seyidi Ali, nako huko ndiko kwenyi kikao cha watu wenyi cheo. Siku hiyo Barozi mkubwa wa Kiingereza alikuwapo, na Bwana Seyid Ali. Bassi mashindano yakaanza, nayo yalikuwa ya Wazungu na mengine yetu sisi watoto wa Mission, na mengine ya askari wa Sultani. Nayo yalikuwa kupiga mbio, kuingia ndani ya magunia, kukimbia miguu mitatu, kuruka, mashindano juu ya punda, mashindano ya killa namna kama bata, kuku, paka, mbwa, &c., kuvutana kamba, mashindano ya Waarabu kuendesha mbio frasi, tena Industani juu ya frasi, tena Wazungu, na mashindano yalianza tangu saa nane hatta saa thenashara. Bassi halafu wote walioshindana wakapewa thawabu kubwa, na aliyezigawa ndiye Bibi ya Barozi mkubwa wa Kiingereza. Kiisha ukapigwa ukelele Hip! Hip! Hip! Hurrah! marra tatu. Ndio mwisho.

December 29, Juma a tatu tukaingia chuoni. Tena alasiri Archdeacon Jones-Bateman akaenda kukaa kwa barozi kubadili hewa kwa siku tano. Tena December 30, Amesafiri Mr. Davis kwenda Magila pamoja na Samuel

MSIMULIZI. 395

Sehoza na C. Janson Mkumbukwa; usiku Mr. Madan alituonyesha sanamu za taa chuoni.

January 1, 1891, ndio siku ya Tohara ya Masiya, tulifurahiwa papa hapa.

January 6, Siku ya Wonyesho, tulianza kufunga safari ya kwenda Mkokotoni; bassi makasha na vitu vingine vya Wazungu vilitangulia kwenda pamoja na wapagazi. Bassi usiku tukalala upesi tupate kuamka na mapema kwenyi mzinga wa saa kumi. Kwanza mbele ya kwenda kulala wote tuliokwenda Mkokotoni tulikuwa jumla yetu watoto 35, tukapewa pesa thenashara killa mmoja ndio chakula chetu cha njiani. January 7, saa kumi ya alfajiri tukaamka, tukala chakula chetu, na Wazungu tano tulioenda nao wakala; nao ndio, Archdeacon, Mr. Matthews, Mr. Dalebrook, Mr. Viney, na Mr. Beetham. Bassi tukaondoka saa edashara kunakuwa kweupe, na tulichukua mikeka yetu; na akina bwana wangine walipanda punda, kwani tulichukua watatu. Tukaenda - weee, tukapita Mtoni, shamba la Ali bin Sudi, marra tukaliona jua linapanda; tukaendelea hatta shamba la Chuwini. Tulipoendelea kidogo tukavuka kijito cha maji karibu na shamba la miwa; tena tukaingia minazini, tena ndipo tukaingia mikarafuuni weeee. Wakati huu tena jua kali, tukaisha mikarafuu, ndipo tukashika njia ipitayo miembeni, na tena njia yenyewe mchanga mtupu na jua kali hapo. Tukatarajia kupumzika wallakini tukaona si vema, sharti tuendele mbele hatta tuonapo mahali tuwezapo kupumzika tupate nafuu. Marra tukaufikia mto na maji yake mengi yafika mpaka kifuani, wallakini tukavuka, tukaenda mpaka karibu na mto mwingine waitwa Mwana Kombo, bassi tukapumzika hapo sana, tukatafuta chakula tununue tusipate hatta kidogo, kwani watu hapana wamekwenda kulima, na wangine wametukimbia kwa hofu.

Bassi tukataka madafu lakini wenyewe hawapo, ndipo

MSIMULIZI. 396

tukayapandia tukayaangusha chini, nussu wakatwaa Wazungu na mangine tukagawana. Tulipokwisha tukawa watu wakucheza tu na kutembea huko na huko. Bassi mimi nikaenda peke yangu nikitarajia nivuke mto, Mwana Kombo, kwani tangu penyi kituo chetu hatta huu mto ni kama mwendo wa dakika kumi. Nami nilipokaribia mto, marra nikastushwa na mama mmoja wa Kimakua, kwani alikuwa amejikunyata penyi kichaka, na aliponiona mimi mtu wa Mzungu akanirukia akanishika: Nami hamuuliza, Je! mama una nini? asiweze kunijibu marra moja kwani anatetemeka. Baadaye akasema, Je! baba nasikia huko utokako si kwema, kwani nasikia kuna majeshi mawili ya Wazungu na watu wao; na killa wafikapo hukamata watu. Nao huuliza, Nyumba yako wapi? Yuko wapi mumeo? Na watoto wa wapi? Nikamjibu, Mama unajisumbua burre nafsi yako, hapana hatari yo yote, hawa ni Wazungu walio waalimu, tunakaa nao sisi mjini; bassi leo tumekuja nao illi kutembea tu. Akanijibu, Si amini, baba, kwani assubui leo amepita huku kijana atokaye huku amesema, Kuna jeshi la Wazungu linakuja kukamata watu, bassi sharti mjihathari nafsi zenu. Nami nilitaka tangu assubui kupita lakini marra niliposikia habari nikawa mtu wakujificha hapa kichakani kusudi nisikamatwe. Nikamjibu, Ee mama niamini mimi kwani ni mwanao, wala siwezi kukuhatarisha, kwani nami ni mtoto wao, nakaa nao, napewa chakula, na nguo na killa nitakacho, wala hawanithulumu kitu; kiisha nao ni Wazungu watano tu na sisi ndio wengi, tumekuja tembea tu. Tena akanisadiki lakini si sana akatoka alipo akashika njia, nami nikaenda hatta penyi mto nikauvuka, nikashika matembezi ya ng'ambo ya pili.

Nikamkuta mama mmoja tena analima, marra aliponiona akaniita, akaniuliza, Je! habari za ng'ambo hiyo utokako kwema? Nikamjibu, Kwema. Akasema, Ati baba, leo amepita hapa kijana amesema huko ng'ambo ya mto huu kuna majeshi mawili ya Wazungu hukamata watu, bassi.

MSIMULIZI. 397

ameniambia sharti nijihathari nafsi yangu nisikamatwe. Nikamwambia, Matua hapana chochote cha kukuthuru, wala Wazungu hawakamati watu, tena nao ni watu watano tu na sisi ni wengi, tumekuja kutembea tu. Bassi kama kunisadiki ao sio sijui illa mimi nikazidi kuendelea mbele, nisimkute hatta mtu. Ndipo harejea njia ile ile, hamkuta yule mama mwenyi kulima, akaniuliza, Mtapita sasa hivi? Nikamjibu, Ndio. Tena nikavuka mto nikafika kituoni nikawaarifu wenzangu yaliyonipata. Bassi Wazungu wakasema watapumzika mpaka saa tissa unussu, na sisi yafaa tutangulie kufika Mkokotoni. Bassi tukaondoka saa sita unussu tukashika njia pamoja na Mr. Matthews; na watoto sita wakabaki na Wazungu kwani wamechoka. Tulipofika mto Mwana Kombo tukaoga kiisha tukaendelea mbele, marra tukafikia sehemu kubwa ya inchi sawa, na watu wengi wanalima. Hawa watu walipotuona walitupa majembe wakaenda mbio waume kwa wake, wangine hujificha mnamo vichaka. Bassi sisi tukawa watu wakucheka tu, hatta mwisho tukawapigia makelele; tukaenda mwendo wa saa nzima katika inchi sawa, na watu hutukimbia tu. Halafu tukafika mashamba ya Mwanda, tukaona ni heri tufikie mjini Mwanda. Tulipofika Mwanda tukanunua vifao vitakavyotufaa Mkokotoni, na ndipo penyi maduka ya samaki wengi; tulipokwisha tukashika njia ya Mkokotoni. Kama mwendo wa nussu saa toka Mwanda hatta Mkokotoni; tukafika Mkokotoni, tukavuka mto Magi, halafu tukaingia ndani ya nyumba ya Mzungu Fraser, ndimo alimotia mashini ya kufanya asali na sukari. Tukakaa kama robo saa tu, tukapewa madafu tukanywa, tulipokwisha tukatoka kwenda nyumba ya Baniani iliopo kilimani ndipo tulipokaa, tukafika kama saa kumi. Tukawa watu wakutembea huko na huko, halafu jioni tukala chakula chetu, tukalala. Jan. 8, Alhamisi tukaamka, tena ikawa shughuli yetu kutembea na kucheza ovyo, tukapika chakula chetu cha athuuri

MSIMULIZI. 398

tukala, tulipokwisha tukaenda nyumba ya Mzungu Fraser, bassi Archdeacon Jones-Bateman akatuonyesha hiyo mitambo mikubwa ya kufanyia asali na sukari, naye akatuhadithia habari nyingi ya mashini haya. Tulipokwisha wengine tukaenda Mwanda kununua samaki kwa kitoweo chetu, kiisha tukarudi nyumbani. Tukapika chakula cha jioni, tukala; marra tena tukapika chakula tayari kwa assubui ya Jan. 9, sababu tutatoka assubui na mapema. Tukalala, assubui na mapema tukala, tukafunga mizigo yetu tukatoka ndio safari ya kurudi hapa petu.

Lakini kwanza pana habari kidogo ndio hii. Tulichukua nasi njiwa wawili toka Kiungani waliozoea kurudi zao kwao wakichukua barua, bassi wakafungiwa barua kule kule Mkokotoni, wakaachiwa wakashika njia marra ya kurudi Kiungani, hatta walipata habari kama tuko salama Mkokotoni.

Bassi tulipokuwa tukirudi tulifika shamba la Chuwini kama saa sita, tukapumzika hapo sana, halafu sisi pamoja na Mr. Matthews tukatangulia kurudi, na Wazungu wengine walibaki wanapumzika hatta saa kenda unussu kwani jua kali. Tukafika hapa saa kenda, na Wazungu waliosalia nyuma wakafika saa kumi pamoja na wapagazi.

Marra saa kumi unussu tukamwona Mr. Mallender ametoka Magila anakuja hapa, tukafurahi. Tukapata habari kama wageni wengi watokao Bonde wamewasili Mkunazini pamoja na Padre Woodward; wengine wetu tukaenda kuwalaki njiani tukawaleta hapa kwa furaha sana. Majina yao ndio Paolo Dezu, Lawrence Mmaka, Mikael Mfuko, Edward Kingodi, Yakobo B. Koti, John H. Chahwi, Luke F. Mhilu: Nicholas Mhina; Daudi Mbwana, Robert Kapala, Mkiva, James Chuma, James Mwaimu na John Mwaimu. Pamoja nao mwalimu Archibald A, Semmanyi na Alfred Juma.

Jan. 10, Assubui wametuasilia wageni wengine watokao Nyasa, ndio mwalimu William E. Kanyopolea, Denys

MSIMULIZI. 399

Sayito, na watoto watatu Benjamin Mtepa, Barnaba Mtepende, na Simeon K. Mjeleka; hii ndio furaha iliyotupata kwa kupata wageni wengi wajao kusoma hapa. Tena siku ya pili yake wakaja hapa watoto wawili wa Miss Mills ndio William Asilimani na Filipo Segesela, tena Jan. 18, ametuasili mtoto mmoja wa Miss Mills ndiye Paul Tuagonge; bassi siku hizi nyumba hii imejaa watu.

Mtg.

HABARI ZA SHAMBA LA MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi Salaamu. Baada ya salamu nakuarifu habari za hapa petu. November 27, alibatizwa mtoto wa Gilbert Kanyama mthamini wake Diva Dimwendi na jina lake Samuel Diva. December 4 Bwana Matthew alikuja kutazamia kusomuakwa watoto wa Suhool ya Nicolas Faraji, nayo ilikuwa siku ya Alhamisi, na katika hawa waliojaribu William Kingango na Ibrahimu Jabu. Katika darasa ya kwanza na ya pili Ramathan na Alan Juma; ya tatu Almasi na Kajoka December 13 mke wa Baruti amepata mtoto mke. December ile ile Bwana J. K. Key amepeleka watu wawili Pemba kwenda kutafuta ndugu zetu waliopotea wakati wa vita ya Mdachi na Bushirif na majina yao Filipo Kanama na Sidney Nayuma.

Siku ya Juma a mosi tulikwenda Kiungani, alasiri tukaenda Mnazi Mmoja kwa machezo, tukatazama mashindano hatta tukatoshewa tukarudi. Juma a pili ilikuwa ubatizo wa mtoto wa Baruti na jina lake Susane Luisa. Siku ya Tohara hatukwenda mahali. Tena twafurahi sana ya kuwa yule Mwarabu msimamizi wa Bibi mwalimu amempeleka mwanawe Chuoni kusoma. Siku ya Wonyesho tulikwenda Mwera kushinda pamoja ha Bwana Key na alasiri tukarudi.

Feb: 3, Mwalimu Hugh P. Kayamba amepata mtoto mwanamume. N.F.

MSIMULIZI. 400

HABARI ZA MASASI.

Habari za huzuni sana nakuarifu Mtengenezaji. Ah! hatuna habari nyingi zayidi, kwa huzuni siwezi kukupasheni kwa kusikitika sana. Bassi tangu kuturudia Bwana Taylor hazikupita siku nyingi. Bassi amefika hapa Masasi, na amewatuliza moyo wengi wa ndugu zetu waliopo hapa, hatta marithawa kwa kuja kwake wengi wamefarajika na hatta washenzi vivyo. Lakini hatimaye siku hizi akashikwa na homa kidogo wala si kama siku zingine inapomshika siku saba.

Lakini leo hivi Feb. 26, Alhamisi ilimshika homa hatta, Juma a pili March 1, saa nne kassorobo akafariki. Bassi tukatuma mtu kuwapasha habari Wamasihya na Waanafunzi, kwani kwa siku zile mbili ilikuwa hapana mafundisho. Marra waanafunzi wote walipopata habari wakaja upesi, wakaandikwa majina kukesha kanisani, na jioni kaburi likachimbwa. March 2, Juma a tatu karibu saa ya pili assubui ikawa maziko. Bassi ndio huzuni iliyotupata, P.K.

HABARI ZA NEWALA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Baada ya salamu nakuarifu habari za hapa nazo ndizo hizi. Siku hizi twalipata hatari ya jua, hatta vyakula vyetu kama mihindi imeharibika kwa jua kali; lakini tukadumu katika sala kanisani. Hatta kunako March mvua ikaanza kunya hatta leo. Tena kunako February 26, Alhamisi bwana Matola alifunga safari ya kwenda kuwinda pande za Rovuma pamoja na watu zayidi ya arobaini.

Nao wamepiga nyama kumi na tatu, na mzee Matola mwenyewe akamwokota tembo amekufa, lakini nyama imekwisha kuoza, bassi wakachukua pembe zake mbili tu

MSIMULIZI. 401

wakaleta hapa mjini. Siku hiyo ikawa shangwi sana, tukatengeneza barazani, watu wangine wakalima njia kuu, waanawake wakafagia njia mpaka msituni.

March 4, Alhamisi ndio mzee Matola akaja mjini akatwaa pipa la baruti zima akatupa, tukapiga bunduki kwa furaha. Jioni ikawa machezo mengi, Wayao Kikorowe, Wamakua Kimakua ndio Likwata, na Wanyasa wakacheza Masauga.

Bwana Porter amekwenda Masasi kumsayidia Bwana Smith, kwani Bwana Taylor amefariki kwa ugonjwa wa siku tatu, tangu Alhamisi hatta Juma a pili akafa. Bassi Bwana Porter aturudi Juma ijayo. B.M.

HABARI ZA NYASA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu habari zetu. Tangu tulipokuwa waalimu wanne, hatta mwisho akabaki mmoja tu hapa Likoma.

Bassi tukajipanga zamu mbili kwenda kufundisha mahali paitwapo Kukobwe ndio kwa Amataka. Bassi tulikuwa watu wa kuendaenda baharini kwa majira ya miezi mitatu; na pamoja naswi mwalimu Richard na mwalimu So, nao walikuwa watu wa shughuli ya kujenga nyumba zao lakini sasa wamekwisha, wanafundisha watoto. Twatumaini sasa watoto wao wanaweza kusoma Masomo ya kwanza, mahali tulipokuwa tukifundisha tulikuwa na watoto 801. Kwani waliona kusoma imekuwa kama kitu cha tunu wasichokiona bado, wala si hawa watoto 80 tu, lakini na watu wazima pia wenyi ndevu na mvi pia, hatta na mfalme mwenyewe alikuja pia, kusudi waone nini kusoma. Bassi mimi nikasema "A," watu wote pia watoto na wazee hunifuatisha vile vile, nikajaribu kuwakataza wale

MSIMULIZI. 402

watu wazima hawakubali. Mwisho nikashindwa nikawaacha wachanganyike wote pamoja. Nilipowatazama kwa kubahatisha labda watu 200 pamoja na wale watoto 80. Lakini tulipokwisha kujenga chuo chetu ndipo tulipoweza kuwazuia wale wazee wasije lakini ilikuwa kwa shidda sana. Watoto wetu walijua kusoma Masomo ya kwanza, lakini hatimaye waalimu wote wanne tukatengwa killa mmoja mbali mbali: kwani waalimu wawili William na Denys wamekwenda Unguja pamoja na watoto watatu. Philip E. Yahom amekwenda Msumba mahali pa Murphy; kwani yeye yupo sasa pa Matika, mimi na Henry F. Shame tupo hapa Likoma. Bassi sasa nitawapasha habari za mahali wanamokaa waalimu.

Pa Mataka tulipokuwapo, jambo lililosifikana hapo ni simba, pana siku hupita mlangoni petu wenyewe tukilala. Kweli mnyama huyu ameisha vitu vingi; amekamata watu, ng'ombe na mbuzi. Kuna siku anakuja na mtumwa wake chui wakuokota makombo.

Siku ilipokunya mvua alikamata ng'ombe wawili zizini, lakini mmoja alimwacha. Siku hiyo watu hawakutoka nje kwa sababu mvua ilikunya mpaka saa nne. Halafu ilipokwisha watu wakatoka nje wakamfuata mzee simba, wakamkuta amekwisha kula lakini sasa amelala. Marra alipowaona watu akawa akirukaruka huko na huko, watu wakimwendea mbele, yeye hurudi nyuma, wakimrudia nyuma, yeye huenda mbele, ikawa hivyo hatta saa zikapita na watu wakachoka kwa kumtafuta, wakarudi mjini.

Pachia wanapokaa waalimu wawili Eustice na Aruffo kulikuwa na uthia kidogo hatta watoto wao waliogopa kuja kusoma. Pana siku watoto wakipiga kengele watu wanakuja kuinyang'anya huitupa majini, kwani watu hawa wajinga husema, Ah! kengele inamwita simba, na tena inaleta ugonjwa ndio maana tunakufa. Lakini waalimu.

MSIMULIZI. 403

husema, Siyo, mbona watu hufa tangu kiasi, na watu wengi wamekufa tangu zamani na huyu simba?

Mtu mmoja aliyetoka Nkamanga alidanganya watu akawaambia, kama mkinipa pima mbili ya nguo nitawakamatieni huyu simba, na asubui mtamwona akinifuata kama mbwa. Watu wakadanganyika wakampa, lakini hatta leo hajamkamata kumfanya mbwa. Sisi sote huku tu wazima sana, lakini mkewe Augustine hawezi kifua ndio ugonjwa wa pande za chini.

Sept. 28, Maryamu aliyekuwa kwanza mtu wa school sasa ameolewa na mfalme, naye pia amezaa mtoto mwanamke, amebatizwa Nov. 16, jina lake Helena. Oct. 20, Daudi Benyamin amepata mtoto mwanamke. Nov. 5, Ruth Neema mkewe Daudi Kaingainga amezaa mtoto mwanamume, alibatizwa Nov. 13, jina lake Robert James. Tena Anne Hathaway mkewe mwalimu So Songolo amezaa mtoto mwanamme. Mama mwenyi mtoto alipopata afya na mtoto naye, aliona ni heri amwendee mumewe sasa kwenyi aliko. Furaha gani aliyokuwa nayo baba kwa kumwona mtoto na mamaye!

Lakini masikini kitoto James Lewis hakupata kunyonya kwa siku thenashara huko alikokuwa, walikuwa na huzuni sana baba na mama kwa ajili ya mtoto. Ilikuwa shidda sana kutafuta mtumbwi wapate kuja huku Likoma apate kutazamwa mtoto na bibi mganga. Siku ya pili ilienda stima ikawaleta hapa. Kweli tulipomwona mtoto alikuwa hana mwili; bibi akajaribu kutafuta dawa, mtoto akapata hajambo kidogo akajaribu kunyonya. Masikini baba na mama hawakulala kwa siku kathawakatha mchana na usiku kumngojea mtoto hatta alipotoa roho.

FURAHA YA SIKU KUU YA KUZALIWA.

Twalifurahi sana kwa mambo yaliyotendeka; Juma a tano

MSIMULIZI. 404

Dec. 24, 1890, stima ilienda chini kuwabatiza watoto hawa wa Msumba, bassi Ubatizo ukawa Dec. 25, waliobatizwa ni hawa: Musa Isaak Akombe, William Yona Kangoma, Yohana Mefu, Mattayo Kalyozi; Henry James Mpila; Samuel Nicholas Chapchapu, Barnaba Tomaso Wantuomwewa, Stefano Leonard Paonanga na Paolo Labuda. Tena siku ile ile walibatizwa watoto wa Likoma ndio hawa Musa Mnjima, Alban Mwanza, Edward Chiwanga, Sulemani Chilimani; Joseph Chitemba, na mtoto mwanamke Tabitha Potanjila.

Dec. 26, walibatizwa watoto wa Pachia, ndio, Leonard Mattiya Kamungo, David Amini Kalaode, Michael Chikokota na Bernardo Mkaki.

Tena iliyo furaha sana ndio Dec. 26, waalimu wote tulikusanyika wote pamoja hapa Likoma, na ndio kitu cha furaha kuonana uso kwa uso, kwani kwa muda mkubwa sana hatuonani. Bassi Dec. 29, tulifanya siku ya furaha ya rohani (retreat) hatta Juma a tano Dec. 30 asubui. Halafu tukatengana waalimu wote, wengine wakaao ng'ambo ya karibu wakaenda zao Alhamisi January 1, 1891; lakini wakaao mbali wakaenda January 3.

Dec. 29, tulifanya mchezo kama tulivyoweza, lakini tulipokuwa katikati ya mchezo, tulipotupa macho kwenyi makutano ya watu watazamao mchezo, alionekana mwanamke mwenyi "Chasuble" amemfungia mwanawe mgongoni: Marra hiyo mchezo yakavunjika wala hatukucheza tena illa kidogo tu na watu wachache, yule mwanamke alipoulizwa akasema, nimeazima tu kwa jirani yangu; wengine wakasema, imenunuliwa Lindi. Kwa baadaye ikajulika kama ile nguo ya kanisani imeibiwa huku kwetu; mwanamke akashikwa siku kathawakatha, na mfalme Chitesi.

MSIMULIZI. 405

Nathani mtafurahi kusikia kama mahali akaapo mwalimu Richard, ndio Kukobwe pa Chitesi, watu watatu wamekuwa waanafunzi wamepokea msalaba. Walipewa misalaba mbele ya mfalme wao, kusudi wasithani kama wanadanganywa juu ya dini yetu.

Tumepata habari kidogo kama simba aliyekuwa akifanya uthia pande za ndugu zetu amepatikana kwenyi anakokaa ndugu yetu mwalimu So ndio Kungoffi. Tumepata habari zake hivi:

Alikuja kama saa a tatu ya usiku kuja kukamata ng'ombe; lakini mtu mmoja aliondoka akachungulia kwenyi alikoendea huyu simba, na alipotupa macho akamwona ameingia paangoni, akawaita wenzake wakakoka moto wakalingojea mpaka assubui kama saa a tatu ya mchana wakaleta nyavu za kukamatia nyama. Wangine wakaingia ndani kumsaka akavumbulikana alipojilaza akapigwa bunduki akafa.

Naswi twafurahiwa ya kuwa ameuawa labda halafu tutasikia kama yupo mwingine.

Tuna habari kidogo tu za kukuelezeni. Kwani siku zote hizi zilizopita tumemtazamia Msimulizi wa 12, 13, 14, lakini bado hatujapata miezi yote iliyopita.

January 5th, 1891, s.s. "Charles Janson" ilishuka chini kwenda kuwatwaa Wazungu tunaowatazamia, lakini haikuwaona kwani walikuwa njiani bado hawajafika Monkeybay. Twasikia kama Makanjila alikwenda kufanya vita Pemba. Naona hamjui ginsi ya kupigana kwa huku, kwa falme zilizo kubwa. Ngojeni nikuelezeni. Kwanza humpelekea pipa la baruti adui yake &c. na yule mwingine humpelekea mchanga au hesabu. Kama Queen alivyomfanyia mfalme wa Wazulu Kechwaya ahesabu nywele za kondoo, kama angeweza kuhesabu bassi ndiyo ameweza kuhesabu jeshi la Queen; kathalika na huku vile vile, Bassi

MSIMULIZI. 406

Makanjila alimpelekea huyu Pemba mapipa 2 ya baruti na maneno mangine ya kutakana shari; Bassi ile baruti aliyompelekea ndio hunena, Twaa baruti hii, mimi ninakuja na vita yangu, nakuletea usipate kusema sina baruti. Naye Pemba alipoona vile akasema, Hii ndio baruti ya vita, hii ndio barua ya vita. Bassi yeye hakuweza kukataa, akatwaa mchanga akampelekea Makanjila, ndio kusema akiweza kuhesabu mchanga huu ataweza kuniharibu na ufalme wangu pia. Tena ule mchanga maana yake ya pili ndio kusema, Njoo mimi tayari baruti yako wewe uliyoniletea ndiyo nitakayokuharibu nayo. Bassi Makanjila akatwaa vyombo vyake vitatu na majeshi yake na yeye; mwenyewe wakavuka hatta upande wa pili. Twasikia kama ilikuwa vita ya siku 3. Bassi siku ya tatu Makanjila akakamatwa akauawa, naye huyu Makanjila ndiye yule yule aliyemsumbua Baba Johnson, sasa ameuawa. Twasikia kama watu wa Pemba waliouawa walipata 60 na wa Makanjila hesabu hawana.

S.S."Charles Janson" baharini ilipokuwa ikienda chini wakaona vyombo vitatu vinarudi vitani lakini mfalme hamna ameuawa. Bassi Baba Johnson alikuwa kwenyi chumba cha ndani, asijue kama kuna vyombo, lakini Captain Sheriff aliviona pamoja na Mr William mfunguliaji mitambo, Captain akamwambia Andrea mshika sukani akasema, Pindua sukani tuwatazame ni nani hawa. Bnssi akapindua, steamer ilipofika karibu na vyombo ikawa kazi yake kuvizungukazunguka tu, lakini watu waliomo wachache sana na wenyi hofu, nussu Waswahili. Halafu wakaviacha vile vyombo viwili wakakiendea kilichokuwa nyuma nacho kidogo ndani walikuwa watu 9 tu. Bassi Captain pamoja na Mr. William wakakishika chombo wakakifungasha sana hodari, wakaulizwa Nani ninyi? mwatokapi? na mwaendaapi? Wale watu kwa hofu na kutetemeka wakasema, Sisi watu wa Malkiya Akuluunda, kwani Akuluunda mwanawe Makanjila aliemzaa; lakini Makanjila

MSIMULIZI. 407

humchukia mamaye, bassi mamaye akaenda kujenga mji wake ng'ambo ya pili ya bahari akastarehe. Bassi wale watu wakasema ni watu wa Akuhiunda wapate kuachwa, kwani walijua kama Akuluunda hana shari na Wazungu. Lakini yote matupu, watu wale walithani watauawa kwa maana watu wa Makanjila walimsumbua Bwana Johnson. Bassi wakawa kama watumwa tu, wakiambiwa, fanyeni hivi hufanya, lete hiki, huleta, pinda mikono tukufunge hupinda. Marra Baba Johnson akatokea akawaambia maneno tena akasema, Shukuruni sana kwa kuwa mmeokoka mikononi mwa Wazungu. Bassi Waswahili waliokuwa mle wakashukuru sana sana. Halafu Stima ikaja hapa pasipo Wazungu wala barua January 24. Jan. 26 ikaenda pande za juu kwa watu wa kabila lingine waitwa Wampoto, nako kuna Waswahili wengi. Bwana Johnson akashuka pwani kusema nao pamoja na mkalimani wake jina lake Achibowa. January 30, ikarudi ikaleta mbuzi zapata 3 pamoja na ndege nghwali kama kuku. January walibatizwa wanawake wazima kenda.

25th January, akabatizwa mtoto wa Marko jina lake Cecil. Feb 3, s.s. "Domira" ilifika hapa jioni tulipokuwa kanisani, filimbi ikalia wangine wakasema mbu, wangine hivi na wangine hivi. Bibi Miss Woodward akathani kinanda kimeharibika. Lakini tulipokwenda pwani tukaona Domira imekuja pamoja na Wazungu 4, na mpiga chapa mmoja jina lake Nicholas na mkewe na watoto wake 2, na mpishi mmoja Gilbert. M. na mwalimu mmoja Austin T. M. Nalifurahi sana kumwona huyu mwalimu kwani nipo peke yangu. Siku alipotoka mwalimu Henry F. S. kwenda Msumba ndiyo siku alipokuja huyu mwalimu na wenzake, s.s. "Charles J." s.s. "Domira" hazikukutana njiani zimepishana njia, kwani Charles J. ameondoka kwa kusudi hili hili kwenda kuwatwaa hawa Wazungu. Mwenzangu niliyekuja naye huku kwa kazi moja

MSIMULIZI. 408

Philip E. Y. sinaye yuko kwenyi mji wa peke yake ndio Patsapa, karibu na Matope. Masikini Bwana Ellis Viner yu wapi? Tumesikia kama amekufa habari zimetufikia Feb. 3, kama Bwana Ellis Viner "amelala." Ndugu zetu salaam sana.

Mtasikitika sana kusikia kama ndugu yetu Richard K. aliyetenda kazi vizuri sana na kuwafundisha waanafunzi wake watatu pasipo kuchoka, atendaye kazi kwa bidii sana. Lakini sasa "amelala," amekufa kwa amani Feb. 6, 4.0 am.

Ugonjwa wake kwanza ulikuwa kitwa, halafu akaugua tumbo. Aliugua kwa Juma nzima, lakini hakujua kitanda alifanya vile vile kazi yake. Ijumaa Feb. 6 ulimzidia lakini hakulala, alikuwa akitenda kazi. Saa a sita ugonjwa ulimzidia akaenda kulala. Watoto wakajiingiza chuoni kusoma, Mkewe alipoingia ndani akamkuta karibu atakata roho, hakuugua hatta kidogo lakini alikufa kimya, akapumzika kidogo kidogo kwa dakika zapata 5 akakata roho. Masikini bibi Clara anajiona sasa yu peke yake.

Palikuwa na watu si wengi wakimsayidia kushika kazi yake ya mwisho na kumngojea, alitenda yote awezayo kutenda, akakaa akingojea habari zitokazo Likoma, kwani alituma mtu. Zikatufikia habari hizi 6.30. a.m. marra tukatafuta watu katika vijiji vilivyo karibu yake. Tukampeleka Charlie Nasibu na Petro Chibwana kwenda kutafuta watu asharini wawezao kuvuta kwa kafi upesi upesi kwenda kuleta mwili wake huku pamoja na bibi mjaani na mtoto masikini.

Bassi wakapatikana wakafuatana nao Charlie Nasibu na Harry Tumani aliye nahotha wa mashua iitwayo Charlie, bassi watu wakaingia humo upesi upesi wakavuta hatta wakavuka. Walipoingia ndani wakamkuta mkewe amekaa peke yake na mtoto chumba cha ndani, na waliomsayidia wakakaa chumba cha nje, bassi akawaita kwenda kumtazama, akawafunulia wale ndugu wawili kwani alimfunika. Ndugu wakatwaa Bible wakamshikisha mkononi, wakatengeneza

MSIMULIZI. 405

zayidi kidogo, wakafanya haraka sana usiku kwa usiku wakaingia wote mashuani wakavuta upesi upesi wakafika hapa asubui. Walipokuwa wakija baharini nikaajabu sana kuwaona watu wa huku wanaimba wimbo wa huzuni. Bassi Juma amosi ndio leo tukaenda pwani wawili wawili, kama kwa dakika 7. Tukashusha mwili ndani ya mashua, tulichukua pole pole, hatta tulipofika kaburini, tukafanya sala tukamzika. Rafiki yangu aliye mkubwa amepumzika katika kazi yake; nani atakuja kuitimiza kazi yake? Kwani ilikuwa ikiendelea na ikisitawi. Lakini amelala Feb. 9, &c. Nyumba mbili za mwalimu Murphy ya kulalia na School zimeungua, mwenyewe alipokuja hapa kwa maziko ya ndugu yetu mkewe alisalia kuko huko. Bassi alishikwa na ugonjwa hakuweza kurudia kwake akakaa hapa siku 3. Akasikia kama nyumba zake zimeungua. Bassi alikuwa hana buddi kwenda, alipata barua kwa mwalimu So. Kwani yeye So pia alikwenda Kukobwe kwa maana alisikia mwalimu Richard amekufa. Akatoka upesi pwani kwa pwani kwa miguu lakini hakuwahi; akasikia kama watu wamekwisha uchukua mwili kwa mashua hatta Likoma. Bassi akaenda mwendo wa nussu saa kwenda kwa mwalimu Murphy, marra alipofika akaona nyumba zinaungua akafanya haraka kumsayidia mke wa Murphy sana kutoa vitu lakini hawakuwahi kuvitoa vyote, vikaungua. So akaandika barua upesi kuja hapa akawapa watu wa mtumbwini kuleta, marra akaenda zake Kungofi. Tuna huzuni na mashaka sana siku hizi. Sasa S.S. Domira inatiwa mizinga ipate kuwa ya vita. C.K.

HABARI ZA SHAMBA LA MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu habari za hapa petu. Mwezi huu wa March tunahuzunika sana kwa ndugu zetu waliotuacha: kwanza Matengenea akaugua siku si nyingi lakini alidirikiwa

MSIMULIZI. 410

kubatizwa Jan. 28, Alhamisi usiku alipewa jina Nuhu Matengenea. Feb. 1 Waanafunzi walipewa misalaba siku ya Juma a pili, nao watu kumi na tano: wanaume 8 na wanawake 7 majina yao wanaume Mpabeni, Selenge, Saadi, Piwale, Ndonde, Chimasi, Saliboko, Ramathani, na wako Masele, Nijamisi, Apewaje, Hednya, Hedaya, Atakaje. February 2, alikufa Nuhu Matengenea siku ya Juma a mosi Feb. 7, nalikwenda Ndiyani karibu na Dunga, hatta alasiri nikawa mtu wa kurudi hatta saa ya pili usiku nikawasili Mazizini.

Zungusho la Watumwa - Kufika tu Mazizini nikaambiwa kama watumwa wapo nyumba moja, nikauliza mwanzo na mwisho, watu wakaniambia sisi tunataka ukamwambie Bwana kwani haifai watumwa hawa waende zao utumwani kwani tumemwambia Diver hatujui shauri lake, kwani hatta mimi nilimkuta asiniambie neno liwalo lote. Bassi nikampa Diver punda aende naye Mbweni akamchukua. Nami nikaokota karatasi nikaenda kuwachokoza wenyi watumwa, nikaingia nikauliza, Mkadamu yuko wapi? wasinijibu, kwani wakawachukia watu wa Mbweni kusudi wasiseme kwa Bwana Key habari za watumwa. Nikawaambia, Barua hii nimepewa na Bwana wa Mbweni, mnipe watumwa. Marra wenyi watumwa nao wakasimama kwa ushujaa na panga na bunduki zao, wagombane nami watetee watumwa wao. Nami nisiwasikie, wala sikuwa na kitu chochote mkononi.

Nikajibu nikawaambia, Kama hamnipi, angalieni, barua hii naipeleka kwa Bwana Barozi, niliposhindana nao sana hatimaye wakaniambia watumwa wamekwisha kwenda kwa Bwana Seyidi pamoja ua watu wa Mbweni, ukitaka na wewe fuata. Kumbe ni hila tu kusudi wanidanganye. Marra anatokea Nokoa Saadi, nikamweleza, naye akakana, nami nikamsuta tazama ukubali kwenda ao ukatae, akasema

MSIMULIZI. 411

mimi sisemi illa twende kwa msimamizi Mwarabu. Tukaenda, wakaungama wakisema kweli tumewaficha tulikudanganya tu. Haswa wenzangu walisumbuka mno kwani walipokwenda wasimkute yule Diver nao walidanganywa wakaambiwa amekwenda pamoja na msimamizi kwa Seyidi, nao wakafuata hatta mjini kwani imekuwa magari wakakaa nyumbani pa mfalme wakathani Diver na watumwa wamo wanahukumiwa, wakakaa hatta saa pili za usiku zikapiga, nao wakarudi. Nami nikashindana nao wakaahidi kuwapeleka kwa Seyidi, nikawaambia msipowapeleka angalieni barua hii napeleka kwa Barozi, nikaagana nao. Juma a pili tena wenzangu wakawatia shindo, na Bwana Key alipopashwa habari akazidi kumpeleka Diver kwa Barozi, na sasa Bwana Barozi ametoa zawadi Rs 50 kumpa Diver March 10, tulifiwa na Marko Msoma naye alidirikiwa kubatizwa. March 15, alibatizwa mtoto wa Mwalimu Hugh P. Kayamba jina lake Hugh Martin Thackeray. March 21, ilikuwa harusi ya Ethel na Ramathani ikawa siku ya Juma a mosi. Nicholas Faraji na Titus Mataula wamepata watoto, Titus mtoto mwanamme Nicholas mtoto mwanamke, na walibatizwa, Juma a pili March 15; majina yao wa Titus, Constantino, wa Nicholas, Alice Kuth. Tena ikapigwa mbiu kwao wanaouza tembo, marra wakaja watu kumi wakashitakiwa kama wanaouza, Bwana Clarke akawasamehe akawaambia wasiuze tena. N.F.

HABARI ZA MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu ninakuarifu ya kuwa mwezi wa Feb. 21 wametuasilia hapa watu watatu ndio Rev. H. Clarke na Miss Ruth Berkeley na Blandina, naswi tumependezewa kuwaona ndugu zetu tena na kutufikia salama.

Tena Feb. 27 ameondoka hapa bibi yetu mmoja naye

MSIMULIZI. 412

Miss Emily Woodward yule aliyekuwa akiwaangalia watoto wa nyumba ya kazi, amekwenda kuangalia jamaa zake labda baadaye twatumaini atarudi tena, kwa siku nyingi hatutaonana naye twasikitika sana, kazi yake ameingia bibi mwingine aitwaye Miss M. A. Berkeley na ndugu yake Miss Ruth Berkeley anamsayidia kule.

Ametuasilia tena mwalimu mmoja aliyekaa pande za Masasi Feb. 28 ndiye Harry Mnubi na mkewe Louisa Mnubi naye anakaa hapa Mbweni.

Tena Mr. Key anaondoka hapa ikiisha Pasaka anakwenda zake kwao, atakaa hapa mahali pake Mr. Clarke. R.W.

HABARI ZA PACHIA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu kama hapa Pachia pana uthia wa simba anatuuthi sana hapa mchana ua usiku, akipatacho chote kile hukamata akala, siku moja ng'ombe wawili, siku ingine akakamata watu wawili na mmoja humtupa, nayo simba huyu anadumu katika kula watu na nyama zetu. Hatta katika miji mingine hutenda vile vile, bassi Pachisanga anapokaa mwalimu Paul W. Mambo wameuawa simba wawili, na Panchesi ameuawa simba mmoja, Kungoffi ameuawa simba mmoja: bassi hatujui kama wamekwisha ao bado.

Hapa wamefanywa Waanafunzi watu wazima watano, na watoto wa chuoni kenda. Wengi wasikiaji (hearers) bado kupokea misalaba, lakini wakubwa na wazee vigumu sana kusikia, bado kuamini, tunatumaini kama wataamini kwa rehema za Muungu.

Habari ingine za siku hizi ndio vita ya Wayao imeingia kijiji kimoja jana Feb. 23, jina lake Sisokono, amekamatwa mwanamke mmoja amepigwa kisu cha mgongo wakamwacha. Bassi huu ndio uthia wa hapa karibu na Msumba

MSIMULIZI. 413

na Pachia. Tena mkuu wa hapa ni Maendaenda wa pili jina lake Tanglamula, lakini ni mzee sana lakini ana watu wengi sana, lakini hawamheshimu hatta kidogo. Hapa kwanza tulijenga mbali mbali, lakini sasa School yetu tunajenga moja tu kwa waalimu wawili, mimi na Aruffo Tangani mahali pa mwalimu Paul W. Mambo kwani sasa anakaa Pachisanga. Bassi sasa mimi na Aruffo tunafundisha pamoja, watoto hukusanyika pamoja wa kusini na wa kaskazini. Juma a pili tunakusanyika papo hapo kuhubiri Anjili. Tunasikitika sababu wakubwa hawaji kusikiliza, illa vijana na walio wastani tu ndio huja, lakini twatumaini kama halafu watakuja.

Tena inaanza kazi ya kufundisha watu pande za chini ya ziwa hili, katika miji iliyo kando kando ya mto wa Nyassa mpaka mji mkuu jina lake Chigalu. Bassi ndio kazi ya killa mwalimu kwa mwezi mmoja kwenda pande hizo, bassi nitajaribu kukuambieni killa mji tunaopita. Bassi tukitoka Monkey-Bay twapita kwa Mponda na Mpinga Njila hatta kupita Nyanja ya Malombe. Tena twafika mahali jina lake Pamvera, Zamani ulikuwa mji mkubwa lakini sasa ni poli tu, tena twapita mji Makuya kwani wamekimbia vita ya Mponda, na mtoto wake jina lake Chigwarugwaru, mji wake umekua upande wa Mashariki; lakini upande wa Mangaribi hapana mji hatta kwa Lionde, ndiye rafiki yetu hatujagombana naye bado. Tena twapita Akasapa, tena Mposa, na Pamsala wapo Waanafunzi wawili, tena twazidi kupita miji hii Akupinda, Akamalawi, Kalichenga, Agwaza, na wa mwisho Chigaru ndio Matope. E.U.

HABARI ZA MISOZWE.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Wa baada ya salamu nakuarifu habari zetu chache tu na thaifu pia. Siku kuu ya Uzaliwa tulikuwapo wote Lapa, Bwana

MSIMULIZI. 414

Salfey alikuja kutoa Usharika Mtakatifu hapa petu. Watoto wa hapa walipata siku arobaashara za kucheza. Dec. 27, alikuja Bwana Askofu akitoka Msaraka na pamoja naye Andrew Abdallah.

Dec. 29, akaja Makange kumwamkia Askofu na kumwaga kusema anaenda Makanya kutembea, na Makanya ndio inchi aliyokaa zamani, alitolewa kule na Mbaruku yule aliyekuwa akipigana na Seyid Barghash mwaka wa 1884. Bassi kumbe vile Makange alimwambia Askofu naenda tembea kumbe amewapeleka watoto wake Galoni pamoja na nduguye Kinyassa. Hatimaye akiisha kuagana nao, bassi Askofu na Bwana Woodward wakaenda zao Magila. Tukasalia mimi na Makange; na alitoa neno la kuchekesha sana, tulipokuwa tukiongea, mvua ikanya kidogo, bassi Makange akasema, Ah! mwalimu nimeita mimi mvua hii kwa siku kumi na nne, kwa leo ndio siku ya hamstashara, najua kama ndugu zangu Wakilindi wamenipita kwa dawa, wanaizuia mvua waona kama kwangu yanya kidogo tu.

Nikamjibu, je! kumbe mvua yaja kwa dawa ao amri ya Muungu? akasema, Ah! sisi tunajidanganya moyo tu. Jan. 18, usiku saa a tatu urobo tunazungumza wote tuliona hofu ghafula hiyo, kwani chui alilia karibu yetu kabisa.

Tena mwezi wa January nguruwe wa mwitu, ah! wengi waliharibu mazidi yetu.

Jan. 21, akaja Bwana Salfey na Bwana Brough kutazama kazi ya kanisa, assubui yake Bwana Brough akarudishwa na Bwana Salfey kwani alikuwa ana homa. Siku ile ile Jan. 22, nalikuwa assubui saa a tatu nipo chuoni pamoja na watoto wangu, nasikia mmoja wa watoto asema unaitwa Mwalimu na watu wawili, nikatoka niwaone nikawauliza habari, wakasema, Tuna habari yetu

MSIMULIZI. 415

kubwa, nikawaambia, semeni; wakasema, twataka karatasi tuna mtu mgonjwa sana kwetu. Nikawauliza, ya nini karatasi? Wakasema, Ni ya kutukana pepo atoke katika mtu wetu. Nikawauliza, mwakaa wapi? wakasema, mji uitwao Bagamoyo ya kwa Kituruturu, nikawaambia mwambieni Kituruturu, Mwalimu kasema, karatasi moja reale sita, wakanisihi sana niwape; wakiona naenda zangu Chuoni wakasema, mulungwana nkatama uyu, maana yake mngwana huyu hafai kitu.

Feb. 9, alikuja Bwana Brough na watoto watano wa sermala kuchonga boriti za kanisa letu. Mwezi huu wa February Wakamba wengi wamekuja Bonde wanauza ng'ombe na mbuzi, watu hawa wanatoka karibu ya inchi ya Wamasai kwa kaskazini.

Feb. 13, Akaja liwali Abdallah kwa gulio letu kutengeneza, kwani wanauza ndivyo sivyo. Feb. 16, alasiri akaja kunitazama, kwani alilala Rangaiya mji chini ya Mlinga umbali wake mayili moja tu, alikuja saa kumi unussu alikuja na askari 60. Feb, 17, Abdallah liwali akaenda Gonja ndio inchi iliyo karibu na Misozwe illa ni Sambaani, umbali wake mayili themintashara.

Feb. 23, Akaja Bwana Brough pamoja na Arron Amwitamno kupika, na Peter Salimu kwa kazi ya miti ya kanisa. Ndio siku ile ile Arthur Kimwaga alipoacha kazi ya hapa.

Feb. 24, Assubui mapema saa edashara unussu naamka, loo! nikastuka kwa ngurumo ya simba. Siku ile ile akaingia Mr Robert, na Andrea Lukindo, wanaenda kununua ng'ombe kwa Wakamba waliopo Kumba Mtoni, nikaondoka nami usiku saa ya nane kwenda gulio Mambo Sasa, kwa vifao.

Feb. 26, Tumepokea mvua ya mwaka. March 2, akaja Bwana Brough tena ana watoto kwa kazi ya miti, Ambrosio

MSIMULIZI. 416

Omali, Andrew Nyange, Yohana Mdimu. March 5, akaja Bwana Salfey kutoa Usharika Mtakatifu, siku ya Alhamisi akaondoka asubui.

March 7, akaja Askofu na Arron Amwitamno, na Bwana Brough. March 8, Juma a pili wakapokezwa, watu misalaba, vijana wanaake wanne majina yao, Ntukano, Manguto, Makibaha, na vijana watatu wanaume Tenya, Kilua, Mhina na Semtibu, siku ile ile Juma a pili alasiri Bwana Askofu akarudi Magila. M.F.

HABARI ZA KIUNGANI.

Jan. 29, tumeanza kufanyiwa Examination, tumetazamiwa akili kwa siku nne.

February 9, imetangazwa, nao waliotokea wa kwanza katika darasa ya kwanza ndio: 1. George J. Swedi, 2. Arthur Mvenya, 3. Daudi Machina. Katika darasa ya pili, 1. Benedict Madalito, 2. Willie J. Swedi; Katika darasa ya tatu, 1. Lawrence Mmaka, 2. Petro Kilekwa. Darasa ya nne, 1. Luke F. Mhilu, 2. John H. Chahwi; katika darasa ya tano, 1. Yohana Akupata, 2. Marko Fikilahi, na darasa ya sita, 1. Sauli, 2. Nyange.

Feb. 7, wamesafiri Wazungu watatu wakienenda Membei, ndio Padre Woodward, Mr. Matthews, na Miss Mills.

Feb. 10, tumehuzunika sana kwani ndugu yetu Mikael Mwichande amefariki, Muungu amependa kumtwaa astarehe.

Feb. 19, wametuasilia wageni wetu sita wakitoka Uingreza ndio, Mr. Clarke, Miss R. Berkeley na kasisi mgine Rev. H. Edwardes, Mr. H. Lister, Mr. F. A. Ford na Mr. E. St. C. Henriques, na Blandina Mwamkwama, tumefurahi kuwaona. Bassi Mr. Clarke, Miss R. Berkeley

MSIMULIZI. 417

na Blandina wanakaa Mbweni; Mr. Edwardes amekwenenda Magila, Mr. Lister anakaa Mkunazini; Mr. Ford anakaa hapa, anafanya kazi ya kupiga chapa, na Mr. Henriques anafanya kazi ya udaktari, naye amekwenda Magila. Feb. 24, kimewasili hapa kinanda kitiwacho Piano, kinakaa sebuleni.

Feb. 26, Mr. Davies kasisi aliyekwenda Magila, lakini akawa hawezi sana, bassi akashushwa hapa Unguja, na leo hivi amesafirishwa kwenda Ulaya.

Feb. 28, wametuasilia hapa wageni sita watokao Newala, ndio Mwalimu Harry Mnubi na mkewe wanakaa Mbweni, na Mwalimu Sipriani H. Chitenje, Arthur Kasembe, Yustino Mkandu wanakaa hapa, na Enoch Mtaiwa akaaye sasa Mkunazini akiwa anajifunza kazi ya uhunzi wa chuma.

March 4, wameingizwa watu watano katika Uwalimu ndio hawa: Benedict Madalito, Yustino Mkandu, Willie J. Swedi, Antonio Misimile na Karlo Mwaimu. March 5, ametuasilia hapa mwalimu Hugh Mhina akimleta nduguye kusoma ndiye C. Janson Mkumbukwa, lakini sasa Hugh Mhina amerudi Magila kufanya kazi yake.

March 28, tulipamba nyumba yetu, na kuitengeneza pia, saa kenda unussu tukaenda kanisani kuimba. Jioni saa thenashara unussu tukaingia kanisani kwa sala ya jioni, tukaingia tukiimba nyimbo za Pasaka. Tena palikuwa na Ubatizo wa watoto watatu ndio, Karlo Mkiva, Bernardo B. Mfalme na Albano Nyange.

March 29, siku ya Pasaka, saa kwanza ya asubui ikawa sala kuu ya Usharika Mtakatifu. Tena saa nne kassa robo ikawa sala asubui pamoja na mahubiri, na Mwalimu Hugh Kayamba akahutubu.

March 30, saa kwanza sala ya Usharika Mt., halafu ikawa machezo tu bass. Tena iliwasili meli ya Ulaya

MSIMULIZI. 418

pamoja na Mr. Wilde ua Miss Townshend, tumefurahi kuwaona tena. March 31, ikawa kama March 30, kucheza, saa saba unusu tukaenda chuoni kupokea zawadi. Tena ikaja mashua kubwa zile zinazochukua mchanga na mizigo forthani.

April 1, tukaanza tangu assubui kuipamba mashua, kwanza ndani yake tukatia mibao tukafanya sitaha. Tena tnakajenga kibanda juu yake, na pande zote tukatia fito, bassi tukatia bendera nyingi sana killa mahali, na tukatia makuti ya minazi yalio mabichi. Hatta saa mbili unusu usiku darasa nne zikaenda mashuani kujaribia nyimbo za kuimba (Blackbird).

April 27, saa tatu tukaingia mashuani wote pamoja na akina bwana wanane na mabibi wawili. Ikaja mashua ya moshi ikatufungasha tukaenda zetu, na tulichukua mizinga asharini (fataki kubwa) killa tuendapo twaipiga na tukiimba nyimbo za furaha. Hatimaye tukawasili rasi Shangani tukamsalimia balyozi kwa fataki zetu; tena tukamfikia H.M.S. "Conquest" tukampigia mizinga ya salamu na tukamwambia "God save the Queen." Tukawasili kisiwa cha makaburi kiitwacho Chipwani kama athuuri tukashuka na vitu vyetu vyote, tukala chakula chetu cha mchana. Tulipokwisha tukaanza kazi ya kuwinda paa, tukapata paa wawili tu. Alasiri saa edashara tukajipakia ndani ya mashua ndiyo safari ya kurudi zetu, saa thenashara tukawasili Shangani tukawashusha Wazungu watatu, wawili wa Mkunazini na mmoja wa katika nyumba ya simu. Saa thenashara unusu tukatoa mapambo yote ya katika mashua hatta saa ya kwanza tukawasili bandari ya Kiungani tukaiambia "Utenzi wa Kiungani" tena "God save the Queen." Tukashuka pwani tukaingia zetu ndani, tukaingia mezani, tulipokwisha tukaenda kanisani tulipotoka tukaenda kulala.

MSIMULIZI. 419

April 3, amewasili hapa Unguja Bishop Tucker akitoka Uganda, wallakini hatukupata kumwona kwa maana siku ya pili yake akaingia melini akaenda Mvita na tena kwenda zake Ulaya. April 4, tulikaribishwa Mbweni wote saa kumi unussu na kutazama mipila ya theluji, tena tukapewa vibahasha vya sukari na mua na ndizi &c. Tukaja zetu hapa.

April 9, amerudi Mr. Matthews akitoka Bombay. Tumeambiwa kama Balyozi mkubwa harudi tena hapa, amepewa kazi kubwa zayidi pande za Moroko.

Penyi mwezi wa May Archdeacon Jones-Bateman atakwenda Uingereza kubadili hewa, na atamchukua naye Samuel Sehoza aendaye kusoma huko kama Peter Limo.

April 9, Saa kumi jioni askari walikuwa forthani wakitazamia mwezi wa Ramathani, na walikuwa na mapipa 3 ya baruti kama ukionekana mwezi wapige bunduki. Kumbe palikuwa na mtoto mmoja anavuta sigileti palepale, alipokwisha akaitupa juu ya pipa la baruti. Marra mapipa yote yakapasuka, na mlango wa Seyid wa nyuma umevunjika, na nussu ya nyumba; wamejeruhi watu 25, nao hawajulikani kama watapona, na watu 14 wamekufa.

April 10, ametuasilia Bwana Askofu akitoka Bonde, pamoja na watoto chache wa Magila Wajao kusoma hapa. Walishukia Mkokotoni jana wakaenda usiku kutwa hatta leo assubui saa ya kwanza wamefika Mkunazini. Mtg.

HABARI ZA SHAMBA LA MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Baada ya salaam nakuarifu habari za hapa. Mwezi huu wa May, tumefiwa na ndugu yetu Andrew Mawali. Juma a pili ya Mitende assubui tulilizunguka shamba kwa nyimbo, hatimaye tukaingia Kanisani. Alasiri watoto wanaake walio Waanafunzi walipewa Misalaba, na majina yao Kambachocho, Fitina, Kizuza, Tatu, Asumini, Makamba, Kidala, Ralia, jumla yao wanane. Siku ya Pasaka assubui ilikuwa furaha kuu; kanisani tuliingia kwa nyimbo za furaha wakawa watu Wamasihya waliopokea Usharika

Mt. 168, hatta alasiri ulikuwa Ubatizo wa Waanafunzi kumi na wawili. Waanaume watatu majina yao Charles Parajala, Blasio Juma, Arkipo Kalumpa, na wanaake Azubar, Simtu, Suzani, Siwapibu, Mariyamu, Sitaimili, Hanol, Hidaya, Elizabeth, Mama Mtiti, Evan Staimili.

May 12, alibatizwa mtoto wa Charles Farajala. April 28 ilikuwa harusi ya waalimu watatu wa Kiungani. May 10, mke wa Isaak Chimwai amepata mtoto mwanamme akabatizwa April 28, na watu waliotiwa mikono wanaume 8 na wanaake 19. May 15, amesafiri Bwana Askofu pamoja na watu wa Mbweni. May 23, mwezi ulipatwa, watu walituuthi sana kwa kupiga matini na majembe, mwezi upate kutoa nuru yake tena, ndio dawa yake kwa kuupigia makelele. N. F.

HABARI ZA MSARAKA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu. Baada ya salaamu nimekuarifu ya kwamba panapo March 17, ndiyo Juma a nne, kwa jioni waalimu wote twalikutana

MSIMULIZI. 421

Magila kwa Retreat na ilimalizika Alhamisi assubui, ndipo killa mtu alirejea kwake saa thenashara nussu.

March 27, ndiyo Jumaa Kuu. Bwana Edwardes, ndiye aliyekuja kwa sala ya siku ile pamoja na Daktari, saa kumi ya mchana alipofika Msaraka kutoka Umba kwa sala jioni aliingia Mkumbi kuhubiri. Juma a mosi, ndiyo March 28, saa ya pili ya assubui twalikwenda Umba tayari kwa Pasaka. Lakini bwana Mr Edwards alipatwa na kitwa, sala za jioni hakuweza, bassi twalimtazia assubui ya Juma a pili naye alijitahidi kutusharikisha kwa chakula cha Rohoni, lakini hakuweza. Kwa hiyo Daktari aliona afathali kuchukuliwa hatta Magila. Na mwalimu Henry alifuatana nao hadi Magila, kusudi kumsayidia Daktari, kwa maana wale waliomchukua mgonjwa hapana hatta mtu mmoja ajuaye neno moja la Kingereza la kuombea maji. Lakini siku ile ile kwa alasiri alitokea bwana Mr. Dale kwani alimwambia na huyo Mr. Edwards kuja apate kutufanyia Usharika Mt. Juma a tatu.

Feb. 7, mwalimu H. Andrew Abdallah, ndipo alipoozwa katika ndoa ya Kimasihiya. Panapo March 23, ndipo alipomaliza kuo kwa Kibondei. Kama mnavyojua nilikuwa naye hapa Msalaka kwa kunisayidia kwa kazi ya kusomesha watoto, lakini sasa sinaye, kwani ameambiwa itafaa aende Zungu, na kufanya chuo kule, ndipo alipokuwa mwalimu Lawrence Kombo akifundisha kati kati ya Umba na Mkuzi. Kijana mmoja jamaa yetu wa Umba siku hizi yuko Tanga anamsayidia mwalimu wa Kidachi kufundisha, jinale ndiye Charlie Kadu.

Habari ya Siku kuu ya Pasaka sina habari nyingi. Tumefurahi kama tulivyojaliwa, wala hatukupata siku mbili ao tatu za kucheza, kwani Bwana Askofu ameona heri watoto wasipewe kucheza, kwani wakati wa miezi ijayo kama June, July, watoto itakuwa shidda kupatikana, kwani

MSIMULIZI. 422

killia mwana hana budi kuitwa na mama ao baba kwa kulinda ndege, nami nimeona vema mno. Lakini ijapo tumewaza hivyo hatta uthia unaanza, ndio kufukuza tumbili katika mashamba yao, halisi tangu March 22, kwani ndipo ilipopiga sana mvua; nawaambia, ukijaribu kwenda katika vijiji vilivyo karibu, ndani ya kijiji humwoni mtu aliye mzima, labda mgonjwa, wote hurejea wakati wa jioni. G.N.

HABARI ZA MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu, nakuarifu ya kuwa mwezi wa March 29, ameondoka hapa kasisi wetu Rev. J. K. C. Key amekwenda Magila kukaa kwa muda wa wakati, baadaye atakwenda kwake. Siku kuu yetu ya Pasaka, ilikuwa furaha pia, na watu waliopokea Usharika Mt. walikuwa 166; na hatukwenda mahali po pote tulikaa papahapa, illa Juma a tatu tulikwenda kwa Shamba la Bibi Mwalimu kama saa 9 alasiri, tulifanyiwa karamu huko, vyakula vya ginsi yote vilikuwapo.

April 8, kulikuwa na kusanyiko la Chama cha Mchungaji aliye Mwema, na wakaingizwa watu wawili, Keziah Shikalako na Emma Nyawela. Twafurahi sana kwani Chama tumeongezeka.

April 25, Siku kuu ya Marko Mt. Juma a mosi tulikwenda nussu yetu Kiungani kusikiliza kuimba, nazo nzuri sana.

April 28, Juma a nne kulikuwa na harusi Leonard Pesa na Emma Nyawela, William Edward Kanyopolea na Monica Hurumanani, Wilfred Madudu na Rhoda Voholiwa, nayo ilitawi sana.

May 10, watu 8 walitiwa mikono ndio hawa Rose Nakali, Maryamu Msekwa, Alice Hasina, Emma Kabutu, Joanna W. Mwatakaje, Ruth Agnes Mayufi, Alethia Yasumini, 01ivya Mary Atimjawe.

MSIMULIZI. 423

May 11, kulikuwa na michezo na nyimbo wakaja Wazungu wengi kuangalia na kusikiliza.

May 12, ameondoka hapa Shemasi yule aliyekuwa akikaa hapa Mr. A. H. Carnon, anakwenda kukaa Newala kufanya kazi huko.

May 13, wametoka tena hapa Watoto wawili ndio Florence Flower, na Harriet Mona, wanakwenda kuwatazama wazee Wao. R.W.

HABARI ZA MASASI.

Salamu kwa mpenzi Mtengenezaji. Baada ya salamu mpenzi Panapo siku kuu ya Pasaka naam tulifurahi mno, tukiona na mwaka huu tumejaliwa kukaribishwa na Bwana tena. Naona kama watu arobaini tuliokaribishwa. Hatta juma a tatu ilikuwa "Home" kwa watoto, nami pia nalikwenda Chitangali kwani Bwana Cecil aliniletea neno, kama yafaa kuja tuonane hali. Nami naliona lazima kwenda, hatta zikiwa za mvua siku zenyewe. Bassi naye Bwana Smith kwa wema wake, aliniazima uliokuwa wa marehemu bwana Taylor. Bassi tukatoka kama saa ya kwanza, mimi na mke wangu na mtoto na William Mandanda na wapagazi wawili ndio Tupa na Akucbilanga. Bassi tukaenda hatta pa mzee Chiwalo, halafu tukafika Mapale kwa Mgole tukapita pale mwa mlima wa Chipolombe tukaingia milima ya mwanzo ya Wamakonde bassi ndio mwanzo wa shidda, kupanda kushuka kupanda kushuka vivyo hivyo hivyo saa zikapita. Bassi tukafika mto Lufyajile tukaoga sana tukaisha, tukashika njia yetu tukaenda weeee hatta magharibi, na Wamakonde kisilani sana hatta njia hawataki kutuonyesha ya kunyoka, na killa tumwulizaye huyu hunena hivi na huyo anena vile hivyo hivi vile vivyo. Bassi na mvua nyingi sana yatupiga, hatta saa

MSIMULIZI. 424

kumi na moja tukajificha kidogo katika nyumba ya Mmakonde, lakini hatta warobo saa haikutimia tukauliza maji, akaleta maji husemi kama ya mwaka jana kwa kunuka vibaya, lakini si wengi walioweza kunywa, kwani wao wenyewe wamezowelea kuweka maji sana. Kwani wakati wa Kaskazi maji shidda sana; kwani kutoka kama Chukwani mpaka mtoni kwa Ali bin Sudi, hapo ndio kama karibu sana bassi, ndio maana yafika pengine wakati wa mvua; nao maji hutunza sana kama kitu cha tunu sana, maana ya kupotea wakati huu, huchimba mashimo mwangoni pake kuteka maji, killa karibu ya nyumba pana shimo mlangoni pake. Hatuna buddi bassi kwenda mbele tu killa mtu hutwambia mji uko mbele yenu nendeni tu.

Tukafika mji wa mwisho tukafikia panapo baraza wenyewe wanena mashauri, akatokea mfalme wa hapo akatupa nyumba na maji mengi sana. Tukalala hatta juma tano tukatoka na mfalme mwenyewe hutuonyesha njia, hatta saa apili tukaingia Chitangali. Tukafurahi mno kumwona Bwana Cecil. Tukakaa hatta jumaa na mapema akatupa vifaa vya njiani, akanena kwani hatta huwezi kukaa bado? Nikamwambia sina buddi kukimbilia kusoma juma a tatu, labuda tukijaliwa tutaonana tena. Tukaenda hatta Wanguuwe tukamwona Msagula mtu wa mzee B. Nakam. Tukalala wote pale juma a mosi nikajaribu kuwinda lakini nyama wamekimbia mbwa wa mwitu, bassi tukarejea kambini tukataka kwenda kulala Wolombo; juma pili tukafika kwetu salama salimini. Tukamkuta Bwana Hainsworth na watoto 17 amekuja tembea.

Tamaa mbele, mauti nyuma.

Bassi niwaarifu habari za mtu aliyefathiliwa sana siku hi zi nayo kwanza ni sababu ya Makwangwara. Bassi inchi hii kweli hapana subiri hatta marra moja, killa neno huona

MSIMULIZI. 425

ndio kweli, likiwa kweli ao likiwa uwongo pia husadiki tu, marra watu wamepandilia mbali mlimani, hatta hawawezi kwenda kuangalia kama wakisikia Makwangwara yapo mahali fullani, wao kazi ndio kuupandia mlima tu bassi. Waima siku hizi palikuwa ghasia mno sababu wanena Akuchalawe, mtu aliyekaa Majeja, amechukua vita lakini hajui pa kwenda nayo, bassi watu ndio maana ya kukimbia, hunena labuda watakuja usiku tumelala. Hatta watoto wetu zayidi ya kumi na mbili wametokelea mbali. Mission wakija baba zao kuwatwaa, nao hukata tamaa pia ya kuja kusoma. Bassi siku hizi ndipo bwana Smith akawapa wapagazi mizigo. Ilikuwa April 17, jumaa watu wanne walitoka ndio Samwili Raha na Matawale na Kaukutu na Kapichila. Bassi nayo mizigo minne, ndiyo mitumba ya nguo miwili na masanduku mawili yaliyotiwa ndimu ndani, bassi. (Bassi mitumba na masanduku kupeleka Newala kwa bwana Porter.) Wakatoka, wakapita Nilombo hatta wakaja kwa Chisanga kama juma amosi jioni, wakalala palepale pa Salimu mtoto wa Chisanga. Bassi jioni wakaongea nao hivi. Ah! hivyo mwaenda wapi? Kwa Matola Newala. Ahsante ah! Jamani hamtapasulia mkono mmoja naswi tupige winda kwani siku hizi shidda nguo. Ah! wazoe, ni mali ya watu; aka! nani nyama? Bassi hatta ndimu moja hamtupi naswi tutowe matowo, zimefungwa na misumari hatta hatuwezi kufungua. Ee wallah. Bassi naye mwenyewe Chisanga alikuwapo wakati huu, akawaambia, "Kule Masasi Matola jeuri na amempita Msusa." Bassi maneno haya yote ndio kama mafumbo; akiyatambua mtu anaweza kukimbia, akiwa mjinga bassi baadaye hushikwa. Bassi usiku wakakamatwa wanne na mizigo pia, wakatwaa makongwa waliowafungia wapagazi wa Dachi, wakawaambia Haya haya tumewafungia wenzenu watumwa wa Dachi, na leo twawafungia ninyi pia, na baadaye watu wa Mtenga. Assubui akamfungua Samwil kuwaambia kama tumekamatwa

MSIMULIZI. 426

njiani sababu ya Matola anayekaa Mkomahindo. Akanena bassi Mkuti mfalme kwa Samwil, Mwambie bassi Akumbemba na Mzungu aje tufanye maneno ya watu wetu na mali yake. Akumbemba akamwambia bwana Smith, Jee twende kunako lukambi (ndio baraza ya mfalme wasemapo maneno yao.) Akamwambia, Sio kazi yangu, na kama huyo Matola sisi tulipotoka Mkomahindo yeye alikataa kutufuata sisi, bassi tukamwacha, hatta sasa si chini yetu; bassi ninyi wenyewe wafalme ndio kazi zenu kufanya haki, na kama mali yangu mimi haithuru, mimi masikini si nguvu. Kama angekuwa mfalme mkuu inchi hii ndio ningeweza kumwambia maneno yangu anitozee ao zayidi, nami mali si yangu, ya (sirikali) Mission.

Wakaenda hatta kwa Matola, wakamwambia Watu wetu wamefungwa kwa ajili yako, naye akasema Lakini mimi si kosa langu; watu wanatoroka huko na huja kwangu, nao wenyewe hufuata kuuliza pengine, mimi huwapa wenyewe. Bassi na yeye kwa nini asifuate, angeona kama ningemnyima. Bassi mkaulize kwanza kwani nasikia kama amesema mimi na Akumtenga. Kesho watatoka, kwenda kuuliza. Leo hivi Filipino Nditi na Hamisi wamechukua mitumba miwili na barua kwenda Newala, lakini njia ya Chitangali. P.K.

HABARI ZA MKUZI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Na baada ya salamu nitakuarifu habari za hapa petu.

Siku ya Alhamisi, February 5, Bwana Askofu amewatia mikono watoto watatu hapa Mission, ndio John Mbwana, Frederick Mwakusega, na John H. Sehiza.

February 18, Bwana Askofu tukamwona hapa Mkuzi anatoka Magila naye amechukuliwa katika wavu, kwani alikuwa mgonjwa na kwa hiyo alikuwa akija zake Unguja,

MSIMULIZI. 427

Lakini alipofika hapa Mkuzi, aliona vema akae, na kwa siku chache akapata kuwa hajambo. Na sasa amerudi tena Magila. Feb. 20, Heath Mtwana na H. Chechande na George Fereji wakatuwasilia hapa kutoka Unguja, nao wamechukua na barua zetu; sasa wote wako Magila.

Siku ya Juma a nne Feb. 24, akaja hapa Wilfred Sezua kutoka Magila kuja zake Kiungani, pamoja naye mtu mmoja jina lake Reale, yeye alikuwa akichukua barua kuja nazo Unguja. Bassi walipofika hapa, Bwana Rev. G. Dale akawaambia kama wangoje hatta siku ya pili, kwani alikuwa bado kuandika barua zake, na sisi pia tukapata nafasi ya kuandika. Na Alhamisi Feb. 26, usiku wakatoka kuja zao Unguja.

Hatta siku ya Juma a pili nathani kama saa kumi na moja kengele za kanisani zikilia, tukawaona ndugu wawili wakituwasilia hapa, nao wanakuja zao Kiungani. Ndio majina yao Charles J. Mkumbukwa, na pamoja naye Hugh Mhina. Siku hiyo hiyo ndio aliokuja Liwali Abdallah Gugu, pamoja na watu wake na askari pia, wakiimba nyimbo zao, wakaingia mji mmoja, jina lake Hemwale. Bassi watu wake wakacheza pale, na mwenyewe, akaletewa kiti akakaa. Kiisha watu wote pia wakakaa.

Bassi wakaja watu wawili, mmoja ana mtoto mume, na mmoja ana mtoto mke. Bassi watoto hawa waliposana hatta wakaoana. Hatta kwa mwisho mwamamke akamkataa muumewe, bassi yule mtu aliye na mtoto mwanamume akaja kumshtaki aliye na mtoto mke kama hivi ao kwa maneno kama haya; na watu pia wamejaa.

"Ee Bwana, sikia maneno yangu. Mtu huyu ana mtoto mke na mimi nina mume, bassi wakaposana hatta wakaoana wakakaa, hatta kwa mwisho mtoto wake akamkataa mtoto wangu. Bassi sasa hivi namwia anipe mali yangu niliolea, mtoto wangu alipooa mtoto wake. Naye hataki kunilipa, bassi nami nimeona heri kwenda kumwambia

MSIMULIZI. 428

Liwali. Haya, ndio maneno yangu.

Yule aliye na mtoto mwanamke naye akaanza kusema. "Mtu huyu hivyo alivyosema ni kweli. Wallakini nimemwambia marra nyingi kama aniwie polepole nitamwishia pia. Lakini mimi sikukataa kulipa. Ndipo Liwali Abdallah akasema, Mwiteni huyu mke tumwulize kama kweli amkataa mumewe. Mwanamke akaja akaulizwa na Liwali, Kweli wewe wamkataa mumeo kwa kweli? Akasema, Kwa kweli namkataa. Liwali akasema, Jee wanitaka mimi? Akajibu, Hatta wewe sikutaki. Bassi baba wa mtoto mke yule akasema akamwambia mwanawe, Piga chuma, mwanangu! Liwali akasema, Unamwambia kama mwanao apige chuma azidi kukataa? Akajibu, Siyo, lakini nimemwambia makusudi asione haya kwani amezungukwa na waume. Liwali akasema, Sio hatta kidogo! Liwali akasema tena, Wewe mtoto mwanamume, njoo umtwae mkeo. Naye akajibu, Ee wallah! Ee wallah! Akamtwa mkewe kwa nguvu nyingi, mke yule akaenda kwa huzuni na majuto, kwani mume hampendi. Pamoja na hukumu nyingine akazifanya siku hiyo. Bassi waonaje, ndugu? jambo hili amelihukumu kwa haki?

March 5, siku ya Alhamisi jioni tulipotoka kanisani tulianza kuimba nyimbo zetu na kucheza; bassi tulipokuwa tukicheza kurube mwanamke mmoja ameumwa na nyoka. Naye yuko mlangoni karibu kwa mwalimu John Swedi, marra tukanyamaza kwani hatukuwa na habari, illa twaliambiwa. Bassi mwalimu John akaenda kutwaa dawa, akaja akampa, akapata nafuu kidogo, akaondoka mtu mmoja kwenda kuwaita waanawe wakaja wakamchukua wakaenda naye mjini kwao.

March 7, siku ya Juma a mosi nathani kama saa kumi wakafika Wazungu wawili wanaotoka Unguja wanakwenda

MSIMULIZI. 429

Magila wakawa na wapagazi wao, mmoja kasisi na mmoja mganga.

March 11, Juma a tano tukawaona bibi wawili ndio hawa, Miss Smith na Sister Elizabeth wakiwa wametoka Unguja. March 15, tukamwona mwalimu Hugh Mhina akiwa anarudi Kiungani na hapa amefika alasiri, imepita kidogo. Bassi akalala hapa hatta assubui saa kumi na mbili akaenda zake Magila. March 17, Rev. G. Dale, na Rev. John Swedi, na Henry Nasibu walikwenda Magila, kwa Retreat. Wakarudi siku ya Alhamisi, March 19.

March 27, ikawa ndio siku ya Jumaa Kuu. Assubui saa kumi na mbili unusu tukaingia kanisani ikawa sala ya Usharika, lakini Usharika hapana hatta saa tatu tukaingia tena na aliyehutubu ni bwana Rev. G. Dale. Hatta saa sita tukaingia tena mpaka saa nane. Aliyehutubu ni Revs. John Swedi na G. Dale. Mar. 28, ndio Juma a mosi, tukafanya kazi kufagia kuutengeneza mji, na tena tukapamba kanisa letu kama tuwezavyo? March 29, ndio siku kuu yetu ya Pasaka ikawa Usharika Mt. saa kwanza. Na tena saa tatu ndio sala kubwa ya wote, na bwana Rev. G. Dale ndiye aliyehutubu. Bassi kama saa tano ikaletwa barua inatoka Umba, ikasema yule kasisi Mr. Edwardes alizimia kanisani wakati wa Usharika; bassi bwana G. Dale akaenda naye huko Umba. March 30, Juma a tatu tukawa na furaha kwa killa mtoto, kwa maana tulipewa ruhusa ya killa mtoto kwenda kwake, Na siku hizi kanisa letu limeendelea sana, mafundi wamekwisha kutia mabati, na sasa wanachora. Rev. Key amewasili hapa March 30, kutoka Unguja. Y.M.M.

HABARI ZA CHITANGALI AO MLOLELA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu. Baada ya Salaamu, nakuarifu habari za siku hizi. La kwanza,

MSIMULIZI. 430

nasema miezi mitatu hii hatujapata barua zetu za Unguja, na kama zinaletwa zinachelewa wapi sijui! kama baharini sijui, bassi nakuarifu habari kidogo za hapa. Siku kuu ya Paolo Mt. alibatizwa mtoto wa Daudi Kiwilime, jina la mtoto huyu Amy Ester. Tena Feb. 9, palikuwa harusi ya Mattiya Sayitia amemwoa mwanafunzi jina lake Akivindika. Feb. 22, mzee Maruchila alitoka hapa asipomwaga mtu yeyote, alitoka na mtoto mmoja, akatoka usiku wala hapana mtu akaenda kwa Mchemba. Bassi kulipokucha tukakaa, na kwa sababu mtu mwenyi majumba mengi na mji wake mkubwa, killa mtu kusema, bwana yuko kwa mwenzangu ao labuda yuko kule. Hatta Feb. 23, ndiyo tukapata habari kama mzee Maruchila hayuko kwake amepotea. Bassi palikuwa kishindo cha kumtafuta watu wakaenda huko na huko kumtafuta Masasi, Newala, miji ya Kimakonde mwote humo kumtafuta, ila mji wa Mchemba hawakupelekwa watu. Baadaye Feb. 26, tukasikia kama mtu huyu mnayemtafuta yuko Mchemba, tukapeleka watu watatu, Akumbemba, Kikombe, Mbela, baadaye watu hawa wakarudi jioni. March 2, tukasikia kama bunduki moja marra vigelegele, tukajua kama mzee Maruchila amerudi. Nasema watu walipiga bunduki nyingi sana sana toka jioni aliyofika hapa usiku kucha, na kucheza michezo mingi kumfurahia mfalme wao.

March 12, mtu mmoja alitoka alikuja Mlolela humu, jina lake Msaku, atoka Mitema akawakuta watu akamkamata mwanamke mmoja, na huyu mwanamke akalia ngondo! marra aliyemkamata akakimbia akamnyang'anya nguo, marra mume wa hapa akakimbilia wakamkuta alipofika mjini amechubuka sana. Tena walikusanyika wengi kama Mnazi mmoja siku ya siku kuu, mume na mke, akapigwa mtu huyu hatta amekaribia kufa, kufa kukaribu

MSIMULIZI. 431

kwake. Kwanza mtu huyu alikwenda Masasi, akaiba mwanamke akatoroka; alipokuwa akienda njiani kurudi kwake, marra watu wawili wenyi mtumwa yule wakamfuata wakamkuta njiani, mke huyu ametangulia. Bassi ikapigwa bunduki ikampiga mtu huyu wakamwacha mtu ameanguka chini amekaribia kufa, wakamchukua mtumwa wao, wakarudi Masasi. Hii ni marra ya pili kukamatwa hapa Mlolela; angalikuwa mtu mwema tungalisema atakufa, lakini mtu mbaya huyu atapona madonda ya Masasi na ya Mlolela yamechanganyika pamoja. Yule Mchemba ameangukia miguu sasa kwa Madachi, sasa tunapita njia yetu ya zamani, twaenda Lindi pasipo hofu; siku nyingi amefanya uthia kuvizia njiani, kunyang'anya watu mizigo yao, sasa asema ametubu.

March 15, Padre wetu akapata mtoto mwanamume, hatta March 22, jumaa pili ya Mitende akabatizwa jina lake John Majaliwa, jina la Shemasi wetu akaaye Mkuzi. March 18, Padre wetu alimwona mtoto aliyekuwa akisoma, bwana wake akamuza mtoto huyu akaenda inchi mbali, Padre wetu akawatuma watu kumtafuta, sasa amekombolewa yupo hapa. Alipotea mwaka 1889, ameonekana 1891. M.H.

HABARI ZA NYASSA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Baada ya salaam, Naam shekh! Likoma siku hizi haina mwenzake, illa labda hapo Kiungani. Lakini labda mwakani tutakaribiana. Lakini kwa sasa aha! mmetupita. Kwaje? Tazama katika Msimulizi ya ix ya mwalimu W. E. K. utaona imeandikwa, "Chapa yetu ya hapa Likoma inaendelea kidogo kidogo" &c., Yeye anasema kidogo; lakini mimi nasema inaendelea sana siku hizi, kwani tumepata fundi halisi, hatta "maprende" akitaka tutampa kwa kazi yake. Nathani vitabu vingine vya Msimulizi

MSIMULIZI. 432

wetu vinafika huko. Kama vimefika ninyi akina baba mliouona, je! umekuwaje? Naona karibu tungemvika joho la samawati naswi ati. Blantyre wanaye Msimulizi wao jina lake Kalilole Kioo. Bassi tunashindana naona ati akina bwana, mh! Anayetaka kupokea alete jina tumkandike kitabuni. Lakini naye pia ana gharama yake pesa 1 tu maana hamjui chikwetu, mngejua tungekutozeni pesa 2 killa Mtenga watu. Mkikubali, na mkidumu kupokea Ahaa! bwana labda tutaongeza gharama yake. Kanisa letu bado kuanza, latafutia mali, wallakini je! akina bwana huruma hapana? Hamwezi kutujengea, mchange fetha? Bibi mkubwa wa hapa Miss S. O. Mc. Laughlin anaenda zake Ulaya labda atapitia huko na kutazama inchi nyingine nyingine, hivyo twatumaini kupeleka pamoja naye wetu wa huku waende Unguja kusoma kwa kadri wawezavyo kusoma. Ndio Yakobo Chidumaye, James H. Mpila &c.

March 25, stima Charles Janson ilikwenda kuwatwaa Waalimu wote waje huku kwa siku ya Jumaa kuu &c. Twalifurahi sana kuonana tena. Siku ya Juma kuu walikuja watu zayidi ya 158. Siku ya Pasaka waliopokea Usharika Mtakatifu walipata 58 na zayidi. Bassi shekh, wasikia alichinjwa ng'ombe ambao ng'ombe hayumo katika &c.

Tena upande wa kaskazini ni ufalme wa Wangoni. Bwana Johnson alikwenda kutazama kule. Bassi aliporudi akakaa huku muda wa mwezi unussu na zayidi. Marra twalionga Wangoni watano wakaja kwetu siku hiyo hiyo ya Pasaka March 29, 1891. Mmoja jina lake Homahoma mkuu wa Wangoni, akaleta ng'ombe na mkuki, akasema. Amepeleka mfalme wetu, ndio barua kusema, Mimi sikatazi waalimu; ukitaka lete wasomeshe.

Sisi sote wazima killa mtu na afya zake.

Habari za Pachia ameniletea Eustace na Arrufo, kusema kama simba yule ameuawa, ameuawa kwa njia hii.

MSIMULIZI. 433

Walimtega kama walivyokuwa wakifanya Masasi. Walimwambia mfalme Maendaenda kama watajaribu kumtega.

Bassi wakatega bunduki zao 5 wakazifungia mtini, na tobwa mdogo juu ya bunduki. Ilikuwa March 6, jioni. Bassi mzee simba kwa tamaa ya nyama, akamrukia mbwa, kutaka kumvuta tu, loo! babaa bunduki zimekwisha lia, bunduki mbili zalimpiga, zingine zilimkosa. Na zote zalimpiga miguu ya upande mmoja. Mzee simba akaguna weeeee hatta akajificha akaacha nyama yake. Hatta asubui walipokwenda wakaona damu imefukilika na mchanga wakaifuata weeeee, ile damu wakamwona amejilaza. Walimpa nazo weeeee, naye pia mwenyewe alikuwa akifanya kiume halafu akalegea, akauawa. Na jino lake moja lo! wasalale. Mtu akikuambia hili ni jino la simba hutaamini ukiwa mjinga kwa ukubwa, baba. Bassi sasa mzee Eustace amepewa jina la Makanjila kwa kuwa ametoa akili njema, tangu leo March 29, 1891, aitwa Eustace Makanjila.

Na. Pachisanga pia Paul W. Mambo ameua simba, si peke yake lakini na watu wengine. Alichomoa panga lake akampiga wa shingo. Sina habari nyingi juu ya Pachisanga kwani sikupewa habari nimesikia njiani, lakini ndio kweli, illa habari zake juu ya Msimulizi huu sikupata.

March 31, Stima iliwapeleka So na Murphy kwao, kwani karibu si kama kwa wengine. Sheikh, tulipowapelekeza bandarini kuingia loo! mtu hatasema barra illa Uzunguni. Kwa nini? Tazama wee. Palikuwapo mashua zote mbili. Moja Charlotte na Ousel, zote zilikuwa hapa, moja ya steam na moja ya matanga. Na kampuni lao Charles Janson, pamoja na mashua yake ndogo. Bassi watu wote walikwisha kupakia, karibu itang'oa nanga. Kwanza ilitangulia ya matanga, ikatweka kwenda kutembea tu baharini, kujaribia kama itaenda vema

MSIMULIZI. 434

Bandawe, kwenda kuchukua matofali ya Kanisa. Halafu ikatoka ya moshi wee ebu utazame mambo pa kwenda. Lakini ilikuwa ikienda Mchizumulu. Halafu akang'oa nanga baba yao ndio nini? kama mshale, baba. Alikwenda akawapeleka waalimu na kurudi.

April 1, Waalimu wakao chini wamepelekwa, ndio leo pamoja na watoto wa school yangu ya hapa, kwani wanaenda kuwatazama wazee wao na kurudi tena. Twatumaini wengine hawatarudi illa watapitilia moja kwa moja mpaka Unguja. April 6, bibi Miss McLaughlin aenda Ulaya. C.K.

HABARI ZA NEWALA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu. Baada ya salaamu nakuarifu habari za hapa. March 29, ndio Siku kuu ya kufufuka Bwana wetu, na Juma atatu palikuwa mashindano ya watoto wote wa Rikado wakaja, na wa Filipo pia wakaja. Na mashindano yenyewe ndio kupiga mbio, kuruka, ndio bassi. Na Juma a nne Bwana Porter aliwafanyia watu sanamu za taa. April 1, Juma a tano watoto walipanga safari yao kwenda pande za Masasi. Na wakina Gilbert Yohana Mpalila, na nduguye Francis na Isaya Nanguje, walikwenda zao kuangalia jamaa zao. April 2, Alhamisi Bwana Hainsworth aliwafuata watoto wake Masasi. April 6, mzee Matola alifunga ya kwenda Kiporumbe kumwangalia mtoto wake anayekaa huko, alifuatana na 26 waume na wake, naye akatufanyia heshima na kutukaribisha vema. Na Bwana Watson alikwenda kuwinda Ruvuma hakupiga nyama nyingi, illa swara 2. Na Tito na Rikado walikwenda kuwinda pia, Tito aliua mbango, na swara, na Adamu aliua mbango 1, na swara 2. Na wakati wa kurudi Rikado Sulimani alipatikana na ugonjwa sana.

Hatta kwa kuzidi ugonjwa wake hakuweza kwenda mwenyewe, wakamchukua. Mattayo akarudi huku mjini

MSIMULIZI. 435

akatangaza habari ya kuwa Rikado hawezi, illa yeye akatangaza habari za uwongo akasema, Rikado hawezi nduwi. Hatta washenzi kwa woga hawakwenda kumchukua. Bassi wangine wa huruma wakaenda ndio hawa Leonardo V. Liwenga na Bartolomayo na jamaa wakaenda kumtwaa. Nao ugonjwa si nduwi illa uwongo, na ugonjwa wenyewe ndio tumbo na kitwa, naye sasa hajambo.

May 8, jumaa wamekuja Wadoicha 2 na asikari wachache, naye Mr Porter amewakaribisha, hatta leo wapo. May 6, Juma a tano Bwana alifanya Sala ya kumwomba Muungu atunze chakula chetu kipate kukomaa; tena atulinde katika hatari za vita. Tukatembea kuzunguka mji wetu. Leonardo V. Liwenga alitangulia pamoja na msalaba na kuja Choir na wakina Bwana na tena kuja Wamasihya wote. Ndiyo habari. B.M.

HABARI ZA MISOZWE.

Nakuarifu habari za hapa chache tu na thaifu pia.

Mar. 16, walikuja hapa Bwana Brough yule Msimamizi na Mganga. Mar. 17, nalienda Magila kwa Retreat ya Waalimu. Mar. 19, nikarudi nikamleta Bwana Brough mgonjwa sana, akaingia Mr. Bone akaniambia, Tupatie wapagazi hima tuende Magila, kwa shidda sana nikapata wapagazi 7, kwani siku mbele yake walikuwa wamegomba kwa kukosa kusikizana maneno.

Mar. 22, akaja Askofu kwa msaada wao waliotaka kuwekea tayari. Mar. 23 ndio juma a tatu akatoa Usharika Mtakatifu assubui. Hatta saa 9 u nussu wakaenda zao Magila Askofu na padre Salfey. Mar. 24, juma a nne jioni saa 12 unussu padre Dale akafika hapa kwa msaada wao waliokiwekea tayari Pasaka wasiojua Kiswahili. Mar. 25, juma a tano saa a kwanza Usharika Mtakatifu hatta saa 9 u nussu akarudi Magila. Mar. 27, Juma kuu. Alikuwa padre Salfey ndiye aliyefanyizisha sala zote. Sala ya

MSIMULIZI. 436

Athuuri si watu wengi waliokuja, wachache tu pamoja na Wamasihiya na waanafunzi. Sala ya watoto wadogo ilikuwa saa 3. Hatta siku ya Pasaka ndio furaha kubwa. Watu wengi kupita Juma kuu walikuja. Wamasihiya walioenda kwa Meza ya Bwana ndio 23 waume na wake, ndio kama Wamasihiya wote wa hapa Misozwe. Mar. 81, usiku saa ya 2, wale adui wa mwili wamekuwako tena ndio chui, akalia hatta saa 7 anazunguka mji wetu.

April 20, ilikuwa saa 9 urobo nikatazama nje nikaona watu wote wa vibarua wameshangaa tu kazini nikatoka nami nione ni nini? Nikaona miti yote ilio mikubwa na juu ya vilima vyote vinang'aa, miti kama imevikwa shera na vilima kama vimevaa vilemba vikubwa; kumbe vyote hivi ni wale wadudu Kibondei huitwa kumbikumbi, naona Waswahili hawana jina nazo. April 22, akaja hapa mwalimu wa Msaraka kutuamkia yeye na mkewe, akakaa hapa siku tatu, kiisha akarejea kwake. Siku hivi kanisa letu limetengenezwa boriti vizuri. M.F.

HABARI ZA KIUNGANI.

Siku kuu yetu ya Pasaka hatukupata kustarehe mahali illa twalipata kwenda kisiwani kushinda, kwa sababu twalikuwa tukimngoja Bwana Askofu, kwani alikuwako pande za Bonde. Bassi alipotufikia ndio mwezi wa April na ndipo siku kuu ilianza kufikiriwa. Na siku kuu ikawa April 14, watoto wote wa Kiungani na mjini twalikusanyika Mbweni, na jioni tukarudi.

April 25, palikuwa na mchezo hapa petu uitwao Mchezo wa Kuimbato maana yake Michezo na kuimba pamoja. Bassi watu wakatujia kama saa edashara unussu, na wanaake wa Mbweni wapata kumi na kenda, na usiku twalikula nao pamoja, na panapo saa ya kwanza unussu ya usiku ukawa muda wa furaha na kupiga makofi. Michezo ya

MSIMULIZI. 437

zeze, filimbi, ngoma, zomari, na nyimbo zingine za "Black Bird" na mabibi wawili walipiga piano moja kwa mikono miwili miwili. Na panapo saa a tatu wakatawanyika. Bwana Askofu pia alikuwapo na siku ya pili yake ndio juma a pili April 26, alitia mikono watoto watano hapa petu majina yao Karlo Mkiva, Alban A. Nyange, Bernardo B. Mfalme, Yakobo Koti, na Filipino Segesela.

Apr. 28, kulikuwa harusi Mbweni ya Waalimu wetu watatu, watoto wote tukaenda illa wasiobatizwa. William na Leonard wanakaa Mbweni, na Wilfred amesafirishwa Bonde. Jioni ya siku hii ya harusi Wazungu walikusanyika hapa pamoja na Bwana Askofu kufanya (Retreat) "Kufunga kwa rohoni" ilianza saa ya kwanza ya usiku mpaka juma a mosi saa ya kwanza ya Assubui. April 30, akawasili Padre Woodward akitoka Bombay.

Siku ya Filipino na Yakobo Mitume walitiwa watu wawili kuwa Wasomaji ndio Mr. Matthews na mwalimu Denys Sayite.

May 4, amesafiri baba yetu mkuu tumpendaye Arch. P. L. Jones-Bateman kwenda Ulaya kupunga upepo kwa kuwa hana afya sana, akimchukua pamoja naye mwalimu Samuel Sehoza kwenda kusoma zayidi. Labda tutampata tena mwisho wa mwaka huu.

May.15, wamesafiri waalimu watatu Archie Semmanyi, na Wilfred Madudu na mkewe, na Nicholas Kusi kwa kutembea, na watoto wawili Karlo Mkiva na Alban A. Nyange na Padre Woolward kwenda Bonde.

Siku ya Kupaa twalienda mjini kwa Usharika Mtakatifu kwa sababu petu hapakuwa na Kasisi. May 15, saa ya pili twalienda mjini pwani kumwaga Bwana Askofu, pamoja naye waalimu wetu wanne, watatu wakiendea kazi ya Upelekwa pande za Newala ndio Hugh S. Mtoka, Daudi Machina, na Leonard

MSIMULIZI. 438

Mkwasomba, na mmoja pande za Nyassa ndiye Reginald H. Songolo. May 18, watu wa kazi wa hapa walienda kushinda kisiwa cha Bawe pamoja na Mr. Mallender, na Mr. Kick. May 19, ndio katika siku za Pentekote twalienda kushinda Mwera na kuvua samaki, jioni tukarudi zetu. Mto umejaa maji kwa mvua hatta migomba ya mtoni yote imelazwa chini. Jee ndugu! Masika jee anawaamkieni vibaya ao vema siku hizi? Juma a pili ya Utatu ndio May 24, twalikwenda Mbweni kwa Usharika Mtakatifu kwa sababu Kasisi mmoja tu siku hizi hapa Unguja, wawili hawawezi Rev. Weigall na Rev. Edwardes, amesalia Rev. Clark tu peke yake; twatumaini wataondokea tena.

May 26, Basil Mhada ametiwa kuwa mwalimu, twafurahi mno kwa ajili yake.

Maajabu ya Walimwengu.

May 25, saa tatu waliletwa Wahindi wawili na mtoto mdogo wa miaka minane ao kenda wapate kuja kufanya maajabu yao. Lakini kwanza twalienda chuoni saa tatu unusu tukatoka saa nne wa robo tukakaa karibu na mwango wa mezani. Bassi nao wakaja pamoja na majamanda yao matatu madogo na moja kubwa na wakafanya maajabu mengi sana hatta sikumbuki yote; illa nitawaelezeni mawili matatu mpate anga na ninyi kucheka kidogo. Watu 2 mmeja hupiga kijigoma na mmoja afanya maajabu yake, yakaendelea hivi.

Alitwaa rupia mbili mkononi, na akatia mkono wake puani na tusizione tena, na akazibua pua yake rupia zikatoka. Na akashika moja mkononi akaivuta zikatokea tatu, akampa mwalimu Connie akamate akamshikisha shikisha masikio, pua, uso, halafu akamwambia, Zitupe chini. Alipotupa anaona moja na pesa tatu. Akamshikisha

MSIMULIZI. 439

tena zikatokea puani. Akampa akamate tena kiisha akamwambia, Fumbua, wakatokea kaa wa pwani ndogo wala sizo rupia tena.

Tena alitwaa fimbo yake akapiga piga akaifunika kwa nguo na alipofunua akatokea njiwa, njiwa na uzima wake, kiisha akamfunika.

Na lililo kuu sana ndilo hili. Watu hawa wamekuja na mtoto, bassi wakamtwaa wakamfungia ndani ya wavu wakafunga kabisa, kiisha wakamtia ndani ya jamanda lao wakamfunika kwa nguo wakaimba imba hapo, kiisha wakaondoa nguo waliyomfunikia yule mtoto. Na tazama wavu upo chini na kofia ndani yake wallakini yule mtoto hapana, amekwenda wapi sijui. Wakalikanyaga kanyaga lile jamanda na wakachocha chocha kwa fimbo hayupo mtoto, kiisha akakaa mwenyewe ndani yake jamanda tupu kabisa hamna mtu ndani. Na wakaanza kuimba imba pale na wakafunika nguo juu ya jamanda wakamwita mtoto akaitika ndani ya jamanda, kiisha wakamtoa kama alivyokuwa kwanza. Hatta wakaotesha mwembe na embe zake, tena mchanga kuwa bisi za mtama.

Jee Bwana yale majamanda madogo jee? Sijaisha ati bado nikali nasimulia yale madogo majamanda, katika moja wapo kubwa kidogo mlikuwa na joka, babu, naona mguu wako huo, bwana, mwembamba sana, mzaha mbali! joka ambao joka kulishika tu la ogofya, kisha tumeambiwa kama meno yake yametolewa, lakini kwa ginsi lilivyo haligusiki kama mtu amepata kumwona "Chatu" lililopea ambao kupea, bassi ndio mfano wa joka hilo, halisahauliki kwa mtu aliyeliona, wanaliambia nyimbo linatambaa tambaa huko na huko; Kiingereza jina lake (Bock snake). Na yale mawili mlikuwamo nyoka wa Hindi, wale wakali kabisa, hatta kwa dakika tano huishi kama akikutafuna. Namna yao kama mkono ukiuweka sawa pasipo kukunja konde,

MSIMULIZI. 440

vivyo wao wamepanuka sana kwa juu na wanatoa pumuzi kama za bata. Maji, baba, bakuli zima yanatiwa jichoni, kiisha yanarudi tena yamejaa vile vile ao puani, ao sikioni pia yakawa vile vile yamejaa tu, hatta yakimwagwa pia akitia mkono juu ya bakuli hujaa tena. "Waana a Adamu chini ya jua hutaka killa mtu kumpita mwenziwe kwa werevu, apate killa mtu kufayidiwa na mwenziwe." Watu hawa walipewa Rs. 14. kwa michezo yao hii.

Tangu kutoka Arch. P. L. J-Bateman kuiacha Kiungani kwenda Ulaya, hatujapata Kasisi Wetu, kwani Kasisi wetu angekuwa Rev. Weigall, lakini siku zote hizo tangu kutoka kwake Arch. alikuwa hawezi sana. Naye sasa amekwenda Mombasa kupunga hewa; akitumaini kutujia June 10, twataraja ndivyo itakavyokuwa.

Tena panapo May 26, tumejiwa na watoto sita watokao Nyassa majina yao Yakobo Kachanda, James H. Mpila, Leonard M. Kamungo, Barnaba T. Wantuomwewa, David A. Kalanda, Michael Chikokota.

May 29, wamewasiri hapa Rev. J. K. C. Key na Rev. G. Dale wakitoka Bonde pamoja na Mr. Brough kwa kutembea. Mtg.

BANDERA YA KWINI.

Hapa Unguja tumepata kumwona mtu mkubwa siku hizi, ndio Mr. H. H. Johnston, ametoka Ingereza amekuja mwenyi mamlaka kubwa; kwani Serkali ya Kwini amemtuma kwenda kutengeneza pande za Nyassa, na kufanya hukumu juu ya inchi zake. Jambo hili latupasa sisi sana kwani Likoma iko katika hukumu yake, na miji mengi yenyi waalimu wa Mission. Tena Blantyre na Zomba na Bandawe na Shire mpaka Ruo, hatta Zimbese ya chini pia. Bassi mtu huyu akifanikiwa katika kazi yake, twaona itafaa sana kwa watu wote wa asili na ndugu zetu pia. Bado kwanza kidogo. Haifai haraka. Halafu yake

MSIMULIZI. 441

twatazamia mambo mengi katika pande zile, biashara za utumwa kukoma, vita za burre kuzuiliwa, watu kupata hukumu ya haki, killa mtu kumiliki mali zake yeye pasipo hofu, biashara nyingi kufanyika, mashamba kuzidi, madini kutafutwa, njia kutengenezwa, watu wote kupita huko na huko salama salimini, hatta kutelemkia Kilimeni na kurudi upesi, barua kwenda upesi zisikose kufika siku zote, vitu vyote vya Ulaya kupatikana Nyassa, na vitu vya Nyassa, pamba, kahawa, pembe, ngozi, sukari, killa kitu kuuzwa kwenda inchi za mbali. Ndio kazi yake bwana huyu kazi kubwa, yenyi mashaka na hatari, pangine mazito kwa watu wa huko. Bassini? Hawajui afanyavyo. Lakini amepewa nguvu, si hukumu tu. Hukumu gani pasipo nguvu ya kufikiliza hukumu? Bwana huyu atakuwa na asikari zake na jemadari na Wazungu chini yake na mabarozi, si kusudi afanye ukali. Kutuliza na kutengeneza ndio kazi yake; ukaidi wa wajinga tu uzuiliwe.

Bassi kama ufalme wa Warumi ulivyotengenezwa sana, hatta siku ya Bwana wetu alipokuja, ulimwengu wote kama unakaa raha mustarehe chini yao, kusudi Anjili ya Masiya ipate njia ikaenee upesi pasipo mazuo mengi, ndivyo labuda kazi yake itakavyotufaa na sisi katika kazi yetu iliyo kubwa kweli kweli na bora zayidi, kazi ya kuuhimiza ufalme wa Muungu katika mataifa ya Afrika. A. C. M.

MSIMULIZI. 443

Ndugu, mwe rathi sana kwangu mimi hapa Msimulizi safari hii, mkiniona labuda kama nimekonda, ao kuendeleza vema kumekoseka mahali, ao vile vituo, ndio uthia sana, na mangineyo. Bassi nini ilionipata? Ah! Bwana, nionee huruma. Mtengenezaji sina safari hii, amekimbia kwenda kuamkia wazee, kucheza sijui, labuda amechoka kwa kunitunza mimi sana, ataka kupumzika. Bassi ndiyo hali yangu, kama peke yangu. Nifanyeje? Nivae nini? Niende wapi? Nikipotea je njiani? Bassi kumrathi sana. Nimesoma zile barua zenu za waletaji habari. Ah! Bwana, zimenishinda zingine. Vituo hapana. Bassi ni? hapana vituo barra? havipatikani? moja moja tu? Tena mwandiko kama wa haraka. Harufi hazinielei pangine. Nabahatisha tu. Na zile "Capitals" hazioti huko? Lakini najua mambo mengi barra. Wino, kalamu, faragha, nafasi, yote shidda. Illakini, ndugu, mhurumie Mtengenezaji wangu; labuda ndio amekimbia sababu mmezidisha kazi, nayo nyingi, kwani nimeona mwenyewe, na kitwa changu kinauma, kina kizungungu, na "salts" sitaki.

Haya! Nijipe moyo. Machozi ya kike. Neno moja nalishika. Nakaza bidii kutokea sawa sawa August 1. Sichelewi siku moja. Sijui barua zenu. Haithuru. Tena najaribu kujipamba kidogo kwa sanamu. Bassi nini? mzee ashindwe na mtoto? kwani mtoto ninaye jina lake "Mtenga watu," na yeye apiga fahari kidogo, ajitazamisha, ajitembeza, maridadi, hatta mimi mzee nifanyeje? Nampenda. Siye mtoto wangu? Siye mzuri? Lakini akumbuke kumheshimu baba. Na baba asimkasirishie mtoto. Amwonye tu. Labuda akiona sanamu zangu, atasema, kweli, mimi mtoto tu.

Kuaherini. Ukimwona yule Mtengenezaji wangu anatembea

MSIMULIZI. 444

tembea pande za huko Nyassa, Kepi, Misri, Ulaya, (sijui vema sana Jografia), umwambie namtaka, kwani peke yangu siwezi, kama sina nguvu, kama nimelala hivi.

P.S. (Msimamizi hapana. Usingizi mtamu!)

HABARI ZA NYASA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam, Baada ya salaam, ah! bwana, habari nyingi hapana. Tangu ilipokuja hapa Apr. 22 hatta sasa May 10 stima haijaenda chini kwenda kutwaa mizigo. Kwa maana Mr. Frere kasisi wa hapa Likoma hawezi, na yule Miss Fontaine naye hawezi pia, wala afya hawana wote wawili. April 23 S S. Charles J. imemtwa Mr Frere na Miss Fontaine kwenda Bandawe, kuuguzwa huko. April 24 S S. Charles Janson iliwasili hapa tena, ikashika kazi yake ya kuzungukazunguka hapa mwenyi miji ya waalimu kuwatazama wa hali gani, na kurudia hapa tena. Siku ngine ilikwenda tena Bandawe kwenda kuwatazama wale wagonjwa wetu wawili. Iliporudi, twalipata habari kama Miss Fontaine hajambo kidogo, lakini Mr Frere bado kupona. Labda watakaa huko mwezi, wakiwa wazima watatuwasilia tena hapa. Tumezidiwa bwana na makasisi huku. Na kazi ipo tele.

Pengine hatupati hatta Usharika Mt. kwa kuwa makasisi yetu wagonjwa.

May 6 S.S. Charles Janson ilikwenda pande za chini, kwenda kuwatazama waalimu wa huko. Kwani siku zote zilizopita ilikuwa ikiendaenda huku na huku papa hapa, kuwatazama waalimu walio karibu yetu. May 7 ilirudi hapa, kama 4.30. a.m. Tulipokaa kidogo tukaona S. S.

MSIMULIZI. 445

Domira inakuja, imeleta barua zitokazo huko pande za Unguja. Juma a pili May 10 twalimwona mwalimu wa Livingstonia, aliyefundishwa Bandawe, jina lake Albert.

Bassi twalimkaribisha tukamtaka katika kusanyiko la siku hii ya Juma a pili atueleze habari za upande ule wa pili wa bahari hii yetu. Alitueleza vizuri sana, na kwa taratibu.

Hatta ametuonyesha watoto wanne, alikwenda kuwatwaa kwa mfalme mmoja jina lake Mpezeni; wanaenda kusoma Bandawe, kwa miaka miwili. Kwani mwenyewe mfalme anawataka watoto hao wawe waalimu. Baadaye kidogo 1.30 p m. nalishikwa na nia ya kwenda kutazama mizinga iliyomo ndani ya S 8. Domira. Bassi nikaingia mashuani pamoja na huyu mwalimu, tukawasili hatta mwenyi merikebu.

Kwanza nalipata kuuona mzinga wa kuchoma mdogo; si mkubwa, urefu wake kama 3 feet. Halafu yake mwingine sio wa kuchoma, lakini wa kuzungusha tu. Mwingine sikupata kuuona kwani umefungwa kashani, bado kufunguliwa. Nimesikia kama unalia zayidi ya marra mia.

Bassi twalifurahi mno kuona stima zote mbili zipo hapa. Sisi huku, ndugu, tu wazima, hatujui ya kesho. Hapana maneno mengi, ndugu.

Halafu tulishika njia ya kwenda kwa mwalimu Murphy, hatukukaa sana, kwa muda kitambo tukarejea zetu hapa Likoma. Wote tuliowatazama wana afya zao kidogo si sana. C. K.

SAFARI YA BWANA ASKOFU TOKA UNGUJA HATTA UYAO.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu habari kidogo, ndizo hizi. May 15,

MSIMULIZI. 446

tukaenda bandarini pamoja na watoto wote wa Kiungani tukawaaga, Bwana Askofu na Mr. Carnon wakaingia katika meli pamoja na waalimu watatu ndio Daudi Machina, Reginald H. Songolo, na Hugh S. Mtoka, waendao kufanya kazi ya kufundisha Uyao, lakini mwalimu Reginald Songolo anafuatana na Bwana Askofu mpaka Nyasa. Tena tumefuatana na watoto wawili wa Padre wa Chitangali.

Saa nne unusu tukang'oa nanga, tukaenda hatta usiku pia, na mvua ikatupata panapo usiku wa manane. May 16, kama saa ya pili ya asubui tukawasili Lindi tukatia nanga, na mashua ya moshi ya melini ikaenda pwani ikafungasa vyombo vitatu vikaja kupakiwa mizigo. Hatta panapo saa nane abiria wote tukashuka pwani ya Lindi tukawaona Manjolinjoli, na juu yote tukawakuta wapagazi wako tayari. Bassi tukaenenda nyumba ya Baniani kukaa, wallakini usingizi wa taabu kwa sababu wadudu wengi wanauma, umbo lao kama chungu.

May 17, Siku va Pentekote, asubui saa ya kwanza ukawa Usharika Mtakatifu ndani ya hema; wakashariki watu 14. Saa nne ikawa sala ya asubui na mahubiri.

May 18, saa thenashara unusu tukatoka Lindi kuenenda kwa Selim, mizigo yote ndani ya mtumbwi pamoja na Wazungu, bassi tukavuta makasia tukifuata mto mpaka kwa Selim, na wapagazi wakaenda kwa miguu. Tulipofika tulikaribishwa vizuri sana, hatta Bwana Askofu akapewa mbuzi tukamchinja. Alasiri tukaanza safari yetu hatta jioni tukafika Mloweka, tukasimamisha hema, tukalala: na mpagazi mmoja wa Mbweni jina lake Farijallah akarudishwa sababu hana nguvu.

May 19, tukatoka Mlowaka tukafika Lilonga saa tano tukapumzika; alasiri tukatoka tukafika Lukulesi tukalala.

May 20, tukafika Mpatila tukaenda kulala pa Bwana Porter (hatta leo mahali alipopumzikia Mr. Porter bassi

MSIMULIZI. 447

panaitwa pa Bwana Porter. Bwana Askofu akawa hawezi kidogo homa.

May 20, saa tatu tukafika Maganga tukapumzika kwa dakika tano, tukaenendelea mbele mpaka pa Simba aththuuri, tukapumzika kwa saa nzima. Saa nane tukaenda hatta tukafikia mto Chitangali tukavuka, bassi tukawa tukipita katika mashamba ya Chitangali. Hatimaye tukawakuta watu wa Mlolela, marra walipomwona Bwana Askofu wakazipiga bunduki. Tena tukamfikia. Padre Cecil tukamsalamia, kiisha tukaingia mjini saa thenashara kwa vigelegele. Marra kengele ya Kanisani ikapigwa tukaingia Kanisani, kiisha tukaenda mezani. May 22 hatta May 27 Bwana Askofu alikuwa Mlolela, lakini mwalimu Daudi Machina akaenda Newala. May 28 Bwana Askofu akafunga safari kwenda Miwa, na siku ya pili yake akawasili Newala pamoja na waalimu. Hugh S. Mtoka alisalia Chitangali, lakini June 4 amekwenda Newala. June 8 Bwana Askofu ametoka hapa kwenda Masasi, tena mnamo jangwa la Mpatila Bwana Askofu alikuwa hawezi homa, na pia tulipofika Chitangali alishikwa na homa marra mbili. Bwana Carnon hawezi sasa homa hapa Newala. H.S.M.

HABARI ZA MKUZI.

June 1, 1891 Kwa mtengenezaji wa Msimulizi salamu, na baada ya salamu nakuarifu habari za hapa petu. May 27. Mr. Dale alifunga safari ya kwenda Unguja kwa afya yake akapitia njia ya Tanga. June 26. Padre wetu Mr. Dale alituwasilia tena hapa Mkuzi anatoka Unguja kubadili hewa kwa mwezi mzima. Wote tumefurahiwa mno kwa kurudi kasisi wetu. Tena tumefarijiwa sana naye.

MSIMULIZI. 448

June 29. Siku ya Petro tulikwenda Magila tukashinda huko tukalala hatta assubui tukurudi kwetu Mkuzi. Na mwalimu Henry Nasibu tulikwenda naye kwa safari yao ya Nkorogwe. Kwani wanasafiri kwenda Nkorogwe kujenga mission.

July 1. Walituasilia hapa waalimu wawili, ndio Hugh Mhina na Archibald A. Semmanyi, kuwa waalimu wa hapa badili ya mwalimu Henry Nasibu.

July 3. Walikuja hapa Wadachi wawili. Mmoja alikuja saa 10 akakaribishwa kunywa chaya. Kiisha akaenda zake Minyurani (mahali walipojenga kuwa mji wao.) Hatta saa 1 ya usiku tulipotoka kanisani, tukamwona Mdachi mwingine. Huyu tukamkaribisha akalala hapa hatta assubui akaenda zake Minyurani, kwani wote wawili wanatoka Tanga.

July 10. Wametuasilia hapa watoto wa mwalimu wetu, na tumefurahiwa sana kuwaona, ndio George J. Swedi na Willie J. Swedi.

July 12. Juma a pili ya nane baada ya Pentekote wamepewa misalaba watu 4 kuwa Waanafunzi. J.H.S.

MISOZWE.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu. Wabaaduhu ya salaamu nakuarifu habari za Misozwe chache na thaifu pia.

May 23 ndio Eclipse ya mwezi, bassi walinena watu, Ah! mzimu alienda mbinguni kumtazama Muungu juu. Wangine wao wametoa sadaka assubui yake, kwani ilikuwa giza ajabu giza nene kabisa, hatta watu hawawezi kuonana. Mimi mwenyewe nalikuwapo nje kuanzwa kwake, watu wa mji uitwao Rangaiya walitoa sadaka, na mji uitwao Mbalamo ya Mabungu pia. June 8 assubui ndio gulio la Kisinga.

MSIMULIZI. 449

Siku ile gulio lilivunjika kwa watu wasio na akili na walevi pia. Siku ile ile jioni ninaona watu wapo chini ya mlima wetu wanajenga kambi, nikaenda niwaone na niwauze habari zao. Kumbe nikifika ndio Wakamba, na mkubwa wao jina lake Kanyani, mtu hodari kwa kunena lugha.

June 10 akafika hapa Mdachi aitwaye Jaeger na pamoja naye askari sita na wapagazi wanane, na mpishi wake ni Leonard Mlawe mtu wa serkali yetu, na kiongozi wake Mwinyi-amani Msegeju tajiri sana na hodari kwa kusafiri, mwana nyumba kwake Ozomando mtu Mngazidja, niliyemwona zamani Unguja. Akashinda pale, siku ya pili akatoka kwenda Mlinga, lakini hakuweza kuupanda akarudi akalala; hatta assubui akashuka kwenda Tanga. M. F.

Kathi Thalimu na Mtu Maskini.

Ilikuwa mwezi wa August mwaka jana assubui mapema nimeamka nafanya tayari kwenda kanisani, nikaona watu watatu, mmoja aitwa Kubo mtu wa Misozwe, wawili majina yao ni sawa, Msumari (A) mwana wa Bori mtu wa mji uitwao Macholima, Msumari (B) mfuasi wa wa pili. Waliponifikia wakakaa, nikawauliza habari. Na aliyewaleta wale wawili ni yule Kubo. Wakajibu wale wawili, "Mwalimu, tumekuja twataka kwako mtu wetu, mwivi wetu." Nikawajibia, "Kwaje? mbona simjui. La! Mmemwona, mtwaeni wenyewe," Wakajibu wasema, "Kweli hapo hapa, ila kuwa naye hunaye?" Nikawauliza "Kwani?" Wakasema, "Sikia, mwalimu, ndio hivi." Mmoja wao asema, Msumari (A), "Hapa Hemkole pana mtu jina lake Ngoda, na huyu alikuja akafanya urafiki nami, tukachanjiana mimi naye. Mimi nalikuwa mshariki wa bithaa ya nguo pamoja na mtu aitwa Tofiki anakaa Mwakimba. Bassi na huyu Ngoda hunifuata

MSIMULIZI. 550

mimi, hatta siku hizo nikatimiza \$7 sokoni, nikaja nyumbani ndani ya jumba, na huyu Ngoda aliniona wakati wote huu.

Siku ya pili nikatoka kwenda shamba na Ngoda pamoja. Tukiwa kule shambani Ngoda akaondoka akarudi hatta nyumbani, akatwaa zile mali reale \$7, akaenda zake kwao. Niliporudi shamba haona palipokuwa mali ile. Ah! Hapana kitu hatta chochote. Hangoja hatta jioni nikithani labda Ngoda atakuja; hatta siku mbili pia, hatta ya tatu pia, nisimwone; hatta muda wa jumaa kupita nikasikia kama yu kwao Hemkole. Nikapeleka kumwita asije. Hatta marra mbili na ya tatu, asije. Nikajua wakati huo kuwa ndiye mwivi yeye. Nikaenda peleleza, nikaambiwa kama kawalipa wadeni wake wote. Bassi nikaja hatta pa huyu Kubo. Hiki ndicho kilichotuleta hapa pako" Nami nikatoka nikamwita A. F. Kimwaga, nikamweleza habari zote. Tena nikamwuliza habari za Ngoda kama azijua, akaniambia azijua na mtu pia amjua sana.

Tukafanya shauri tukaenda Hemkole mimi na A. F. Kimwaga. Tukifika panapo lango la mji tukasimama nje tu, tukaita wazee wote wa mji ule. Walipokuja wote nikawaambia habari ile yote, nao wakasema, "Ndio kweli. Yule mtu yupo hapa mjini nassi tumetafuta habari za mali tumeona kweli, kwani mkewe katwambia habari zote." Nami kawaambia, "Kwani msimtoe kwao mjini? Mmemweka hapa. Je? wale kama wangalienda kwa Liwali Mdachi naona mji wote huu nyinyi wazee mngefungwa; ndio sheria, kuonyana." Tena nikawaambia, "Bassi na atolewe, bassi hapa mtoeni." Wakasema, "Ah mwalimu, sisi twamwogopa, illa wewe mwondoeni. Ruksa kwetu mtoe." Na wakati huo yeye Ngoda yuko mjini, hajui habari. Nikawaacha wazee waende. Nikamwuliza A. F. Kimwaga kama yule mtu ni mjanja sana. Akasema, "Ndio." Nikamwambia, "Tukiwa

MSIMULIZI. 551

tumetoka mji, wewe salia nyuma nami nitatangulia tumweke kati." Bassi tukaingia mji A. F. Kimwaga akatangulia, kwani ndiye ajuaye nyumba yake, tukaenda tukabisha akaitika mke. Nikaingia nikamwambia amwite mume wake; amwita akaja. Bassi majira yale nafikiri nimfanyeje kwake. Nikamwambia kama hivi. "Wee Ngoda, mbona hukuja kuandikwa? ulikuwa wapi?" Asema, "Kuandikwa gani?" Hamwambia, "Hukusikia kama mimi. naandika watu siku hizi watu wote wa miji iliozunguka. Misozwe, killa mmoja na nyumbaye na jamaaze wote? Bassi naye akajibu akasema, "Mimi hapa na mke wangu tu. Sina nani wala nani, mbele ao nyuma." Nami hamwambia, "Kweli ila sharti uje kwangu niandike yote kwa utaratibu." Akasema, "Vema, mwalimu, twende zetu." Nikapanda naye: tukitoka tu lango la mji tukamtia kati, tukafika petu nikaenda naye faraghani, mimi na A. F. Kimwaga, mambo yote yale ya mali pia akakana. Nikawaita wale, nikamtoa kwao, wao wakasema, "Sasa twende kwa Liwali Abdallah." Ngoda aliposikia vile akaungama, kwani ajua kule watakakompeleka atakwa na kukatwa vikuu kupita yale ya Msumari. Akanisihi nimlipie, ni kazi ya kurudisha yale mali, lakini mimi naliisha ambiwa kama rususu huyo; bassi nikakataa. Wakamshika wamfunga wakaenda naye. Ngoda akifika kwa Msumari akamwambia, "Msumari, nipeleke kwa ndugu zangu, wao watanilipia mali." Msumari kampeleka. Alipofika kwa nduguye wale wakamkataa wakasema, "Hatutaki huyu, kaisha mali yetu vivihivi kwa kumlipia, naye hatubu. Bassi hatumtaki; mchukueni kwenu, mwuza, mwua; pia yote halali kwake yeye." Wakitoka pale, Ngoda akasema, "Nipelekeni kwa mama yangu anakaa Myindu," wale wasijue kama mama yake ametiwa utumwani kwa sababu yake. Wakaenda hatta kwa mama

MSIMULIZI. 452

yake. Walipofika kule mamaye akipata habari, akamwambia Ngoda, "Nimeona safari ya Ndugumbi (Mwarabu) yaenda Masai; katwaa mali uwe mpagazi." Akatwaa shauri la mama yake. Wakitoka kwenda njiani wakakutana na mtu jina lake Sendola, anayejua alipopanga. Bassi akafuatana nao kusudi apate pesa. Wakafika pale, wamtoa Ngoda kwa Ndugumbi naye akatoa mali R32 akampa Ngoda na akatoa R14 32 P. akamlipa Msumari. Ndugumbi akasema, "Ngoda akitoroka nimulize nani?" Sendola akajibu, "Mimi." (Bado kwisha hadithi)

HABARI ZA MLOLELA (CHITANGALI)

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu, nitakuarifu habari za hapa. Mwezi huu wa May 6 Muungu Mwenyiezi ametufanikishia mambo mengi. La kwanza Mmasihiya wetu Isaak Asasu na Sarah mkewe walitoka Lindi kurudi hapa; kwani walikwenda zamani kufanya kazi, wamekaa huko miezi 10.

Juma a pili baada ya Kupaa watu wakaleta mavuno yao ndio mahindi kushukuru kwa Muungu, si mihindi minne mitatu lakini nasema wanaleta katika makapo makubwa hujaa, kumshukuru aliyehifathi mbegu; hatta Juma a pili ya Pentekote wakaleta malimbuko ya mtama mbichi kanisani, kunde, njugu; nao watu wa hapa petu hawali chochote kitokacho mashambani wasipoleta kanisani kwanza, ndipo walapo kwa furaha; wakati wapandapo, hulima mashamba, humwita Padre kubariki mbegu, ndipo wapandapo mashambani mwao.

Bassi nimesema kwanza watu huleta mazao ya inchi. Labda wewe utauliza ile mihindi huifanyiaje? Sikia. Mihindi ile huuzwa hupata mapesa, halafu hutoa kwa watu wenyi kutengeneza kanisa. Usione, wewe umepata kanisa la mawe, huna taabu nalo wala kulitunza. La. Usisahau mambo ya barra, ndugu zangu mimi; miti na mianzi kama ujuavyo huku barra

MSIMULIZI. 453

mchwa hula kamba, hatuna buddi kutengeneza tena na tena, ao mahindi yale huwapa masikini wagonjwa waliotupwa, ao huwafanyia chakula watoto wa School.

Baada ya haya kiisha Juma a pili ya Pentekote ndipo tukaanza kumtazamia bwana Askofu. Hatta alhamisi asubui tukapeleka watu Chitangali, ndilo ziwa, kumlaki, tukawaambia watu wale wakimwona bwana mkubwa waanze kupiga bunduki, ndio May 21. Hatta aththuuri tukasikia bunduki, marra wapagazi, halafu akatokea Padre na mfalme wetu; bunduki zikazidi hatta wakiingia mjini, naam nakuambia bunduki hizo waanawake vigelegele kuimba kupaka udongo. Marra Askofu akikanyaga barazani (ndipo wachezapo watoto wetu) wengi sana wakaja kutamba na kupiga bunduki bunduki; hatta watoto wa nyumbani pia wakapiga bunduki, ndio mlangoni bwana mkubwa akiingia mlangoni wa uani karibu. Ndipo zikalia nyingi na waalimu wanne na shemasi mmoja na watoto wa Padre wamo pia, furaha ikazidi naam. Naam tazama watu wajao kumtazama punda, juu yote Wamakonde huja kumtazama punda mchana kutwa, huenda kwao usiku. Ijumaa bwana mkubwa alishikwa na homa, Juma a mosi akawa hajambo.

Hatta Juma a pili ya Utatu palikuwa ubatizo, saa nne unusu walibatizwa watu 10 waume 8 waanake 2, ndio saa ya ubatizo. Watu wajao kubatizwa wavaa kaniki wote, hatta halafu wakiisha kubatizwa huvaa nguo nyeupe na kanzu. Bassi wathamini husimama safu mgongoni mwa watu wanaobatizwa, killa mtu humchukua mthamini wake, humpeleka kwa Askofu, humtajia jina lake, halafu humvua kaniki killa mthamini, ikawa ndio kazi yake hatta kiisha watu wote. Halafu Askofu akawahubiria watu fayida ya kubatizwa. May 31 tukapokea waanafunzi 22.

Hatta May 26 watu hawa wakatiwa mikono pamoja na Mattayo Sayiti aliyebatizwa zamani. Watu wale ni Mackenzie

MSIMULIZI. 454

Changango, Adamu Twanje, Andrea Sawasawa, Benito Yosia Masanda, Stefano Asuni, Isaya Kipande, James Petro Malemla, Tito Namwangara, huyu ni Mmakonde mwema sana mwenyi imani sana sana. Waanawake Lea Agnes Akutwae, Ester Akundawaje, ndio waliopokewa katika Kanisa.

HABARI ZA MASASI.

Mpenzi mtengenezaji salamu sana. Baada ya salamu nakuarifu habari za siku hizi. Kweli ndugu zetu, kama mjuavyo, katika killa Station ya Upelekwa huu killa mwaka naumu kuna furaha kwa killa Mmasihiya, kwa maana jamaa zetu watakaribishwa katika Ujamaa ulio mkuu. Haitaji niunene, kwani mwajua vema sana maana yake. Bassi waima May tulimngoja Askofu kwa furaha nyingi sana, kwani tunazidi naswi kuzaliana katika inchi ya Masasi. Waima June 10 akawasili inchi yetu hii ya Masasi Askofu Juma a tano, Alhamisi siku ya Barnaba Mt. ukawa Usharika. Hatta Juma a pili June 14, ukawa Ubatizo tukapata ndugu zetu kumi na 'nne. Ndio hawa: Augustino Tomaso Chitenje, Benado Yusto Himili, Yakoko Beda Undani, Yona Albano Nang'ombe, Daud Marko Akuisombe, Kupriano Mkomola, Leonardo Mtanga (Almasi), Haruni Sulemani Kammanyee, Yohana Samwili Sonje, Isaak Yakobo Likumbi, Stefano Benardo Mpasanje, Charlie Akiba, Yuda Mikaeli Kamtaule, Barnaba Gayo Salitnu.

Hatta Juma a pili June 21 wakatiwa mikono, na kuwaaga watu wasikiao na waanafunzi kwa kuwaonya wawe siku zote na shauko ya kutaka nao kuingia katika kundi la Wamasihiya. Ilipokwisha, tukaitwa Wamasihiya wote na waanafunzi, akanena "Sasa hapa tunahama kwenda kukaa upande wa pili wa mlima huuhuu wa Mtandi upande wa mashariki, kwani sasa tunakaa upande wa magharibi;

MSIMULIZI. 455

kanisa sharti mjenge wenyewe kama zaka kwa Muungu, kwani nyumba ile ni yenu wenyewe kwa ibada yenu." Wote wakaahidi kama watasayidia wawezavyo. Na June 11 Dachini wawili wakaja na askari 15 na wapagazi wachache. Na Bwana Carnon akaja, amechukuliwa kwa machela, pamoja na Bwana Watson aliyemtunza njiani; homa ilimzidi sana njiani; alipofika Chimambo, akapeleka barua waende watu kumchukua. Wakatoka wapagazi wa Bwana Askofu kama wanne kwenda kumchukua.

Juma a pili June 21 Dachini wakaenda zao Lindi. Hapa walikuwa wakipita tu kutoka kwenyi makaa, moja fundi wa kuangalia vitu ndiye Dr. Lider. Na Juma a tatu 22 Bwana Askofu akatoka kwenda Nyassa, na Bwana Smith na watoto wakampeleka mpaka Chogawali jioni wakaachana nao wakaenda zao, na Bwana Smith akarudi. P.K.

HABARI ZA NEWALA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu, nakuarifu habari za hapa. May twalifunga safari ya kwenda Lindi kumchukua Bwana Askofu. Nao wakaenda wakamchukua mpaka-Mlolela. Wakamwacha huko illa mwalimu Daudi Machina akafuatana na wapagazi. Naye akatusilia hapa May 22 kwenyi Ijumaa. Na Juma a tano wakaja wapagazi wa Bwana Askofu pamoja na waalimu Reginald Songolo na Leonard Mkwesomba. Na May 28 akatusilia Bwana Askofu, kwani alipita njia ya Chisanga. Tukaona furaha sana kumwona, kwani miaka miwili imepita wala hatujamwona.

Tena furaha kubwa sana tumepata Juma a pili ya pili baada ya Juma ya pili ya Utatu. Kwani Mama yetu amezidisha sana watoto wake, na Mama ndiye Kanisa na watoto ndio waliobatizwa. Na jumla yao 14, na majina yao Patriki Mangame, Yakobo Akumtamba, Daudi Lusenga

MSIMULIZI. 456

Yohana Mapalio, Samwili Samwia, na Siprian Sua, ndio waume. Na wanaake, Emma Akwitendekanya, Anna Akuchiunda, Rose Aobiletana, na Margaret Alapisyeje, Luoy Akumilasi, Maryamu Anakolo. Na wangine Naome Fereji, na Neema. Na Juma a pili ijayo watatiwa mikono na Bwana Askofu. Na Alhamisi June 18 palikuwa mkutano, Bwana Askofu akawaita Wamasihiya na Waanafunzi wote walio waume. Akatoa maneno na mwalimu Daudi akawafasiria kwa Kiyao. Na maneno yenyewe ndio kuwasayidia hao mabibi wanaokuja, kwenda kuwachukua burre pasipo kutaka mshahara mwingi, Tena kuwarudisha mabibi wakiwa wagonjwa pasipo kuchelewa, kwani wale wanakuja kufanya kazi ya kutusayidia. Tena kujenga Kanisa pasipo mshahara na school. Yote watu wakaitikia kwa heshima. B.M.

HABARI ZA MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu ya kuwa mwezi wa May 16, alitufikia hapa bibi mmoja wa kusayidia chuoni naye afanya kazi ya kufundisha hapa, aitwa Miss H. L. Burke. Twapenda sana kumpata kwani awasayidia kazi ya chuoni.

July 2, Alhamisi kulikuwa na Chama ya Watakatifu wote, wakafanya kusanyiko siku ile wakaingia watu wanne ndio hawa, Miss Boyd, Miss Bennett, Helen Wakihatu na Kandake Kabutu.

July 9, palikuwa na kusanyiko la mwaka la Chama ya Mchungaji Aliye Mwema. Walikuwa kanisani kumi na watano wa chama, kwani watano wako bara. Ni desturi yetu kwa kusanyiko la chama kutoa pesa kununulia vitu wenzetu walioko barra, na mwaka wa juzi tulinunua vinara na vichupa vya mathabahu kwa kanisa la Chitangali,

MSIMULIZI. 457

na mwezi uliopita tukapokea barua hii kwa Rev. C. Majaliwa: Chitangali, June 2, 1891.

Salaamu sana kwa Chama cha Mchungaji Aliye Mwema. Baada ya salamu, shukurani kuu sana kwangu mimi na kwa Wamasihiya wa Kanisa la Chitangali, mliotuletea ukumbusho wa pendo lenu, vinara na chupa za Mathabahu. Tumevipokea kwa mikono miwili, tumeviweka mbele ya mathabahu Kanisani mwetu, Juma a pili ya pili baada ya Pentekote. Salamu kwa mikono yetu. Inatoka kwa ndugu zenu

Barnaba Nakaam + (mfalme) alama yake

Daudi Chiwiline + (mfalme) alama yake

Silas Maluwani + (mfalme) alama yake

Harun Boli + (mfalme) alama yake

Yohana B. Abdallah, Filipo Katembe, Samwil Sulemani, Barnaba Mtaula, Alfred Hugh Mipetula, Augustino Malemla. Oecil Majaliwa.

Mwezi uliopita Mr. Clark alituambia labuda itakuwa vizuri kachagua kazi ngingine kusayidia na sadaka zetu, akataja kazi tatu, ao kutoa pesa kwa kumlea mtoto mmoja Hindi, ao kusayidia kazi ya Sisters katika St. Raphael's, Bristol, ao kutoa pesa kwa kuwapatia watoto masikini wa St. Alban's, Holborn, chakula cha asubui (breakfast) Bassi wote tulifanya shauri na wote kwa nia moja walichagua watoto wa St. Alban's, labuda kwa sababu watatu wa waalimu wetu, Rose, Faith, na Blandina, wamefika St. Alban's, wakapata kuona kwa macho yao, umasikini wa huko. Baada ya dini tulipotoka kanisani, tulikaribishwa na Bibi Mwalimu kunywa chai penyi shamba lake.

MSIMULIZI. 458

HABARI ZA SHAMBA LA MBWENI.

Kwa mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu habari za hapa petu nazo zikawa za huzuni na sikitiko. Mwezi wa June 13, Juma a mosi tulifiwa na bibi yetu na mtabibu wetu mpendwa; hatta alasiri tulikwenda mazikoni. Juma a pili tukashinda hatta Juma a tatu usiku mtoto wa Nicholas Faraji alishikwa na ugonjwa wa ghafula usiotambulikana marra alifariki, sikitiko likaongezeka, siku ya Juma a nne jioni ulikuwa maziko. Alhamisi alizaliwa mtoto kwa Alfred Faraji, naye mwanaume, siku ya 18. Siku ya 28 Juma a pili akabatizwa, na jina lake Petro. July 3 tumejiwa na watu wa hapa waliosafiri safari ya Kongo, nao wametupa habari ya sikitisho sana, ya kuwa ndugu wawili wamefariki, Yakobo Kilindiza na Suwedi. July 17, usiku, tumefiwa na mtoto wa Titus Mataula, Konstantino; Juma a tano ilikuwa Usharika, kutoka tu marra maziko. July 12 ametufikia hapa ndugu yetu Palmer Majaliwa, asema wote salama sana. N. F.

HABARI ZA KIUNGANI.

Mmesikia kama katika mwezi wa May, baba yetu tumpendaye, Archdeacon P. L. Jones-Bateman, amesafiri kwenda Ulaya kwa kitambo. Bassi naye alipoenda, alituachia baba mwingine kutuangualia mahali pale. Naye ndiye Rev. S. Weigall, wallakini alikuwa hawezi: siku nyingi kidogo huko Mkunazini, hatta doctor amemwambia aende Mombasa kwa kitambo, apate afya. Kwa hiyo hatukuwa naye kwa kitambo.

Wallakini tulipata mtu wa kutusalisha na kutufanyia Usharika Mtakatifu, ndiye Bwana Rev. G. Dale, aliyekuja hapa kutoka Bonde mwezi huo huo kwa kupata afya kidogo. Sasa huyu baba tuliyemtazamia kuja kututunza,

MSIMULIZI. 459

ametufikia hapa katika June 14, akitoka Mombasa. Ah! Watoto wote tulifurahi sana kumwona, na tukampa mikono kwa furaha sana. Sasa bassi yupo hapa atutunza. Ameanza kazi yake June 14.

Katika mwezi huu walikuwa wagonjwa Wengi. Bibi Miss Shaw aliugua sana, akapelekwa Mbweni.

June 22. - Mr. J. Dalebrook aliugua sana. Hatta kengele hazikupigwa. June 27 akapelekwa Mkunazini kubadili hewa. Sasa yupo afundisha.

June 21. - Mr. J. J. Viney amesafiri kwenda Ulaya.

June 25. - Admeli na H. M. S. "Raleigh" amewasili Unguja..

Katika mwezi wa July 2, Mattayo Lamilako, Tomaso Kaponga, na Mackenzie Meweawa wametoka hapa kwenda Uganda, wakifuatana Wazungu wanne wapelekwa wa Mombasa.

Katika June 7 mwalimu Samwil Chiponde na watoto wa Newala, ndio Cecil Majula, Kolumba Y. Mzigala, Klement Mkajanguya, Daniel Usufu, Petro Musa, wameenda kwao kutazama jamaa zao, na Stefano Mteta, Yona Selenje, Karlo Lisomba, na Benito Nyalela, na Andrea C. Kapanda.

Katika June 8 waalimu George Swedi na Willie Swedi wameenda zao Mkuzi, kutazama jamaa zao, na kurudi.

Tena katika mwezi wa July, kama ilivyo desturi yetu, ilikuwa examination hapa. Waliotazamia ndio Rev. S. Weigall, Mr. Madan, Mr. J. L. Matthews, na Mr. King. Tulipata kuambiwa majina yao walioshinda. Walioshinda katika darasa ya kwanza: 1, George Swedi, 2, Samwil Chiponde; 3, Arthur Mvenya. Katika darasa ya pili: 1, Cecil Majula; 2, Yohana Chanamilaj 3, Alfred Juma. Katika darasa ya tatu: 1, Stefano Mteta; 2, Mikael

MSIMULIZI. 460

Mfuko; 3, Petro Sulemani. Katika darasa ya nne: 1, John Chahwi; 2, Barnaba Mtipende; 3, Luke Mhilu. Katika examination hii, walioshinda wamepelekwa katika darasa zingine.

July 20, Wameingizwa watu wawili katika waalimu, ndio Yohana Chanamila na Alfred Juma.

Katika siku hiyo hiyo, waliwaasili hapa watoto watokao Newala na Chitangali, ndio Barnaba Mtaula, Isaya Nauganji, Gilbert Yohana Mpalila, Yusuf Kasembe, William Mpagweje, Edward Lujenji, Tomaso Juma.

July 9 Julius Mkwaya ameenda Mkunazini kumsayidia bibi Miss Dean-Pitt kufundisha watoto, na kukaa huko.

June 25. Joseph L. Hapiuwa amekwenda Magila kufanya kazi ya kupiga chapa huko, akifuatana na Bwana Rev. G. Dale.

Katika July 8 ilikuwa siku ya kufungua Canteen kwa Bwana Said Ali Bin Said, iliyojengwa na Wazungu, watokao marikebuni, walipochagua kujenga nyumba, kama mlivyosikia kwanza. Na Canteen hiyo ni kama kibanda kikubwa cha miti na mabati, kimejengwa kondeni kati ya nyumba ya baruti na Mnazi mmoja, maana yake ni mahali pa kuja baharia wa manowari kutembea, na kuchezea michezo yao ndani na nje, na kujiburudisha wapendavyo kwa inchi kavu. Kwani zamani shidda kuja pwani, na mjini kuna ulevi tu na michezo hapana. Bwana Seyidi aliwapa konde, wakajenga.

Askari wengi sana walienda hapo, askari wa Bwana, na wa Kiingereza pia, ilikuwa mdundo sana wa ngoma. Tumesikia kama katika siku hiyo, Bwana Seidi alianguka chini, alipokuwa amerudi na kukaribia jumba lake, na ameumia mkono, na mguu. Hizi ndizo habari za huzuni na furaha. C.M.

MSIMULIZI. 461

FIKARA KWA BIBI MISS M. C. TOWNSHEND.

Ulimwengu wote chini ya jua, killa mtu hukaa kwa furaha na huzuni. Killa mtu huhitaji mwenziwe, awezaye kumsayidia katika huzuni ao furaha alio nayo. Bassi ikiwapo hali hii, haina buddi kuwapo mahali pangine pia siyo mahali pako tu - moyo ukiwa na hali hiyo ya kusayidiana. Bassi hii ni nini?

Tumekaa kimya, furahani na huzunini, tusipojua yajayo. Kumbe tumepata watu walioacha kwao kuhama hatta inchi ngine kwa kusudi hilo. Tumewaona wamekuja wengi killa mtu kwa kazi mbali mbali, lakini kusudi lao ni moja, ndio kutusayidia.

Bassi katika hao tumepata kumwona bibi aliyeacha kwake kwa kusudi hilo tu. Tumeona ginsi alivyopenda kukaa kwetu na kuwa tayari kutusayidia kwa huzuni yoyote ya ugonjwa wa mwili. Tumeona alikaa kwetu, hatta mwaka mmoja aliambiwa na Doctari arejee kwake Ulaya kidogo kupata afya. Wallakini hakukaa sana huko kwake Ulaya, amehitaji sana kurejea tena kwa kutusayidia. Bassi amerudi. Wallakini hakukaa naswi sana, hatta nusu mwaka haukupata. Katika mwezi wa Jutte 6, baada ya kazi yake ya kuangalia wagonjwa, akashikwa na homa mwenyewe. Akaugua tangu hapo June 6, hatta katika June 13 mbele hajaja Rev. S. Weigall. Siku ya Juma a mosi asubuhi baada ya kutoka kwetu Kanisani, ilipokuwa bado dakika 20 kupiga saa ya kwanza, ameitwa na Baba, akafariki. Bwana amependa kumwita astarehe. Alikuwa hawezi siku saba, ya nane amefariki.

Sikia bassi!

"Nikifa nzikwe kama watoto weusi niliowasayidia."

Haya ndio maneno aliyoyasema, alipopata hajambo siku moja.

MSIMULIZI. 462

HABARI ZAKE

Hupenda sana kusayidia wagonjwa, alipenda hatta mnyama. Pana punda hapa, ah! killa siku humtunza, humpa chakula, akiwa mgonjwa humtia dawa; shidda sana mwenyewe kulala usiku. Killa mtu humwita, "Rafiki" na punda pia, "Rafiki." Tufanyeje bassi? Bwana alipenda kutoa, amependa kuondoa. R. I. P.

Hii yatukumbusha neno moja: Tuwe tayari killa mtu kusayidiana. C. M.

HABARI ZA MAGILA.

Kwa mtengenezaji wa Msimulizi salamu sana. Baada ya salaam; sisi huku katika June 21 Juma a mosi nayo akafa mtoto wa Ackworth Baruti. Mtu huyu alimleta mkewe hapa auguzwe, hatta alipopata ruhusa kidogo mtoto wao akawa hawezi, na mwisho akafariki, akazikwa assubui yake siku ya Juma a pili.

Katika June 24 siku kuu ya Kuzaliwa Yohana Mbatizaji tulifunga safari na mapema kabisa kiisha sala ya Usharika Mtakatifu. Tukachukua pamoja nasi kondoo ambao kondoo, zumari ikalia, tukashika njia ya kwenda Mlembule kushinda. Tulienda watoto wote pamoja na mwalimu wetu Bwana Bone na Bwana Lister. Ndio furaha ya watoto hiyo, njiani mwote huimba tu, hatta kufika, tukajenga hema na baadaye matembezi hatta jioni tukarudi kwetu Magila.

Katika June 27 akatuwasilia hapa mwalimu Ackworth Machaku, akirudi kwa matembezi pamoja na Joseph Hapiuwa wakitoka Unguja; Joseph aja kushika kazi ya kupiga chapa.

Katika July 20 watoto wote watapata holidays, juma tatu; ndizo za siku kuu ya Mavuno; na ikija siku kuu yenyewe, hatupati tena; bassi nyie mkaao

MSIMULIZI. 463

Kiungani sisi twafayidi sana.

Katika June 14 Padrc Woodward alienda Mlembule, akawapa watu 19 misalaba. Kazi ya mwalimu huyu yaendelea kweli kweli, nayo bado ni peke yake, waume 11, na wake wanane, na mtoto wake pia alibatizwa siku ile ile, aitwa Josephin Kalahi. Twataka mwingine aje amsayidie. Katika July 20 nikaanza safari ya kwenda kutembea Unguja, na watoto wakienda zao kwao; tutaonana wote August 8th. J.B.M.

MSIMULIZI. 464

NKOROGWE.

Uzigua wa Luvu, July 14th 1891

Salaam kwa Mtengenezaji. Na baada ya salamu huna buddi kuona katha Msimulizi safari hii aongeza habari mpya za Station mpya ijengwayo Zigua ya Luvu.

July 1st tukatoka Magila safari kubwa, Wazungu watatu na sisi wanne na wapagazi kama asharini na zayidi kidogo. Wazungu ni hawa, Mr. Woodward, Mr Bone, ajaye kwa siku chache na Padre kwa kuchagua mahali patakapojengwa Station, na Mr. Lister ajaye kuwa mkaaji na mjengaji na mimi na mwalimu Wilfred Madudu, na Fabian Bwambwara kama sermalala, na A. Gh. Lukindo aitwaye Koka.

Tukaacha Magila kama saa mbili asubui, tukaenda kwa njia ya Potwe tukafika mto Kihuhwi kama mwendo wa saa 3, pale tukapumzika sana kungojana wote, kwani Padre na Mr. Bone walikuwa nyuma na wapagazi wangine.

Pale tukapika tukapumzika muda wa saa 1 unusu na zayidi, tulipokwisha na wenzetu wakafika tukawaacha pale wapumzike nao, sisi tukang'oa tukaendelea mbele, safari yetu twajulishana njia kwa zomari likilia.

Tukaendelea mto huu Kihuhwi tukauvuka marra nne ndipo twaingia Potwe. Hapo tukalala kwa shuruti na kuwaeleza kama si safari ya Dachii hii, msilogope. Wakasema, "Ah juzi twalitendwa vibaya sana na watu wa Dachii, ndio maana leo tukathani ndio safari yao tena." Bassi wangine wakarudi mjini na wangine wakarathi kulala msituni hatta asubui, wapate kujua hakika kama siyo safari ya Dachii iliyopita, wasiposikia kuthuruliwa vitu watu mjini. Pale tukajenga mahema mawili ya Wazungu, tukalala. Hatta asubui kama saa moja tukang'oa tukaendelea mbele twapita

MSIMULIZI. 465

mahali penyi milima miwili huku na huku na njia yetu kati kati na msitu mkubwa hapo, napo paitwa Nkele ya Mahondo. Kupanda hapo waona inchi ya Zigua sawa isiyo na milima mingi.

Tukaendelea hatta kufika mji wa kwanza wa Zigua uitwao Hamjindawa, tukaendelea hatta kwa mji wa Malomo, wote wa mjini wamekimbia pia, hatta mzee Malomo mwenyewe, ginsi alivyotendwa na watu wa Wadachi akanyang'anywa vitu vingi ng'ombe mbuzi nguo, na vitu vingine &c. Akaenda kumwambia Mdachi mwenyewe kama nimenyang'anywa vitu vyangu na watu wako, akamwonea huruma naona, akawaambia watu wake wakamrudishia vitu vilivyopatikana, visivyopatikana akampa fetha mahali pake. Hii yaonyesha kama mambo haya ya uharabu hawafanwi Wadaehi wenyewe, illa watu wafuatao naye kwa kuwa wengi mno, bassi yafanyikanayo mengi hayajui. Mzee Malomo akasikia kama siye Mdachi ni Mwingereza, akapata moyo tena akaja pale tulipotua mtoni uitwao Mnyuzi akaamkia akaongea sana na Padre, akamweleza habari zote za uharabu aliofanyiwa na watu hawa, akasema, "Ah! sasa mimi nangoja kuuawa tu bassi, baada ya kufanyiwa yale yote, na sina buddi kukimbia." Pale tukapumzika muda wa saa na zayidi tukapika tukala.

Baadaye tukang'oa tukaendelea hatta tukafikia barra ya boonde kubwa illa sawa sawa, tukaenda saaana tena ndilo liitwalo Kolongo la Hede. Hatta kafikia njia panda, iendayo Pangani na hii tutokeayo sisi, tukakutana na Wanubi wawili watoka safari ya Dachi waenda Pangani waliofuatana naye kwenda Mazinde. Tukaendelea hatta Pala la Hode tukaliisha tukafika mtoni uitwao Ulwengela, mahali pabaya kupita juu ya mti, tena pasifiwa hatari ya mamba kukamata watu hapo, kupita taratibu hapo, taabu na shidda hapo; mtu aliye na mzigo ah! kwa taabu sana

MSIMULIZI. 466

kupita, aangalie asiuangushe mzigo, tena asianguke mwenyewe, na maji matulivu hapo. Tukapita salaama tukaendelea, ndio twaona mashamba ya mtama wa Wazigua tena, tukaendelea twaona Luvu na mji wa kwanza ukitokea, watokea kwa Mngumi. Tukaenda kando kando ya mto mpaka mji N'korogwe tukaingia ndani ya mji kwa kuvuka ulalo, ao bauti waitavyo wenyewe, ubao uliowekwa kuvukia juu ya mto Luvu, sababu mji uko ndani ya kisiwa. Mkubwa sana mji zayidi ya nyumba mia. Bonde hapana miji kama huu wa Kizigua ifananayo nao kwa ukubwa wao. Watu wa mji wakatukaribisha vizuri tukajenga mahema ya Wazungu tukakaa, nasi tukakaribishwa nyumba za mamaye Wilfred Madudu, tukalala.

Siku ya kwanza tukapumzika Ijumaa. Siku ya 4 Juma a mosi tukaenda kutafuta mahali pazuri pa kujenga kwa upande wa magharibi kilimani kuutazama mji wa Nkorogwe chini na mto na boonde sawa zuri, siku ille tukaanza kulima mahali palipochaguliwa kuwa pafaa. Siku ya Juma a pili Padre Mr. Woodward akafanya Usharika Mtakatifu hemani na sala za jioni pia. Pale palipochaguliwa pakatupendeza sisi illa hapakupendeza wenyewe wa N'korogwe vema. Wakasema hivi kama wao wanazikia wafu katika mapango karibu ya mahali pale tulipopachagua; bassi huja wakaleta maiti zao sisi tukawakataza; bassi afathali tusogee mbele ya mji wao kidogo. Bassi mzee mwenyewe wa mji, Jumbe aitwaye Sengoye, akaja nasi hatta huku kutuonyesha mahali pema, ndipo hapa iliposimika hema sasa, na nyumba moja tunajenga ya kwanza ya Mission ya N'korogwe Zigua Lavu. Na Wazigua wafurahi sana kupata Mission ya Waingereza kukaa nao. Nao tayari kuleta miti ya jengo na killa kitu bora, mapesa tu.

Tangu kuhamia hapa July 6 tukakaa siku mbili, Mr.

MSIMULIZI. 467

Bone akawa na homa; ikamzidi, hatta Padre akaona vema achukuliwe Magila, siku ya 8 Juma a tano. Akachukuliwa katika wavu na wapagazi watokao Magila, ikawa Mr. Lister na Fabian Bwambwara kwenda kutengeneza pale Ulwengela kufanya penyi gogo lile daraja ya kuweza kupitisha mtu na wavu, wakafanya walivyoweza. Hatta assubuhi juma a tano ikawa safari, illa mbele wakatanguliza watu wawili waende kulalia mbele illi siku ya pili waingie Magila na barua za Padre, Mr. Roberts aje nusu ya njia pale Potwe tulipolalia, aje pamoja na wapagazi wa Magila wawasayidie hawa pale hatta Magila, hawa warudi huku. Tukatoka na mgonjwa hatta Ulwengela. Ndio shida ilikuwapo kumpitisha pale, hauwezekani kwa wavu illa alibebwa na mpagazi mmoja na wangine kusayidia nyuma na mbele na kando kando asiangushwe, naye ameshikika sana, rangi imemgeuka, imekuwa uso wake wa rangi ya manjano, nguvu hapana, amelegea. Tukafanya bidii tukampitisha hatta upande wa pili wa mto. Pale mimi ikanipasa kurudi mjini na Fabian M. kwani Mr. Lister amesalia mjini.

Bassi tukiwa tukirudi tukifika chini mjini Sejayake twasikia kuita mwalimu, Mzungu hawezi atapika ana homa imemshika sana, ikanipasa kupanda upesi upesi. Nikifika ameshikika, tukafanya tuwezavyo huku na huku dawa Quinine &c. Akapata rutuba jioni, hatta assubui hajambo. Alichoshwa sana na kazi ile ya ulalo mchana ule, na tena usiku asilale kumtunza Mr. Bone, Ijumaa akashikwa tena. Tena hiyo haikumpa rutuba mpaka ikanipasa kuwaarifu wa Magila, nilipoona sina tena la kufanya. Kwa mwisho Juma a tatu July 13th akaja Mr. Roberts kumtazama akaona ni vema heri aende Magila kwa kutazama afya, labuda homa itampungua kule. Juma a nne assubuhi wakaenda, illa yeye kapanda juu ya punda, hakuchukuliwa kwa wavu. Hapa

MSIMULIZI. 468

nimeachwa mimi na vibarua wanne kujenga nyumba na kungoja mji hapa.

Mletaji habari za Mission mpya sasa. H.N.

HABARI ZA PWANI

Amani pwani.

Misafara mingi inakwenda barra, wa Wapelekwa wa C. M. S. kwenda Uganda, mmoja wa Wadachi kupeleka mashua ya moshi hatta Victoria Nyanza, ndio bahari ya Uganda, mmoja wa bwana Stokes kufanya biashara. Yule Mwarabu mkubwa wa pande za juu sana Kongo, Tipu Tip, amekuja pwani na pembe nyingi na watu kama elfu saba. Na bwana Stokes ana watu kama elfu tatu, Wanyamwezi na wangine, ndio wapagazi wake.

Meli nyingi huja Unguja siku hizi kutoka Europe. Killa mwezi huja meli ya Kingereza na Kifaransa na Kidachi na Kireno, kuchukua mizigo na barua, na meli ya Mombee na meli ya Seyidi pia.

Unguja unajengewa sana, nyumba za mawe zinazidi sana kuwa nyingi na kwenda juu.

Tunatazamia barozi mpya, Bwana Portal, anakuja mwezi huu, na yule General Matthews, lakini kazi yake kwa Mombasa sasa.

Pande za Zambezi Wareno wamepatana na Waingereza, wanatulia. Tena asikari wa Kihindi wa kwini wamekwenda pale pale, barozi mkuu wa Nyasa awe na nguvu kwa kazi yake.

MSIMULIZI. 469

KUZUNGUKA KISIWA CHA UNGUJA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi Salamu. Nakuarifu habari kidogo za pwani ya pili tulipokwenda kutembea kwa siku tano, si nyingi, nazo ndizo hizi.

Siku ya Alhamisi assubui June 4. 1891, twalitoka hapa saa thenashara unusu, tukapita njia ya chuwini, nyumba ya Bwana, karibu na pwani; hatta saa mbili tukafikia shamba lenyi minazi mingi la Banyani Forotha, hatta saa sita tukatua tupike chakula chetu, na mahali tulipopikia chakula chetu paitwa Zingwezingwe; hatukufikia kwa Mwarabu mwenyi shamba, tulipokwisha kula tukajitupa kwa usingizi hatta saa 9, tukatoka. Kutoka Zingwezingwe, tukapotea njia marra kwa marra, tukatumia dira. Tulipovuka mto, tukapata njia nzuri kwenda Mkokotoni. Njia ya Mkokotoni imejaa mashamba ya mpunga mtupu, na tukaona nyika, hatta saa thenashara unusu tukapata nyumba kwa mzee mmoja Banyani atunzaye nyumba ya Mzungu mmoja aitwaye Mr Freza. Nyumba hiyo imejaa panya na njiwa tele, hatta koti langu likatobolewa mfuko na panya, kwani naliweka mkia wa tipitipi ndani ya mfuko. Walakini tukapewa heshima kama nyumba yetu, hatta assubui tukaenda mtoni nyuma ya nyumba kuoga, kwani mto uko karibu na nyumba. Tulipokwisha, Mr Beetham na Mr Faulkner wakafunga vyombo; mimi, Chuwisi, na Kombo tulipofika tukakuta vyombo tayari. Wazungu lakini hawajavaa viatu vyao; na walipokwisha tukaenda zetu hatta pwani. Huko tukamkuta mtu mmoja mwanamume akasema hamtaweza kufika pwani ya pili kwani mawe tele na magugu mengi mengi, tukasema "Haithuru tutajaribu kufika pasipo chombo." Karibu na bahari pamejaa visiwa vya Watumbatu.

MSIMULIZI. 470

Na tulipotoka pwani tukazidi kuingia ndani, tukakuta maduka ya Wahindi hatta saa sita tukafika mahali paitwapo Mkwajuni, pamekuwa kama Gulio, ndipo wauzapo killa kitu, ndipo tulipokula chakula chetu.

Saa edashara unusu tukaenda hatta banda moja akaapo Mwarabu mmoja jina lake Khalufa bin Sabedi, akasema nimekaa hapa shamba miaka 40. Na Mwarabu huyu alitufanyizia heshima na adabu, alitutaka tukae muda wa siku kumi, hatta saa thenashara akatuletea mbuzi, wallakini hatukuweza kumchinja kwani tukawa na njaa, tukataka chakula upesi, tukamwambia twataka jogoo, tukaletewa jogoo na mchele.

Tulipokwisha kula tukawa katika kuongea na huyu Mwarabu hatta saa mbili tukulala. Saa thenashara assubui tukaenda zetu pamoja na huyu Mwarabu hatta nyumba yake ya pili, tukakaa hatta saa nne. Tukaenda zetu hatta Rupenza inchi iliyo karibu na pwani na iliyo na mabonde, na msitu, na mawe mengi, tukaenda msituni kwa msituni pasipo nyumba, yapata mayili 4 msitu wake, hatta saa kumi tukafika Kiwengwa. Ndio siku ya juma a mosi June 6. Juma a pili, June 7, ndio siku ya kustarehe kwetu.

Lakini tabia ya pwani ya pili, ni mbali na ya hapa petu mjini, mtama wao hupanda katika mawe, na chakula wapata, lakini maji ni taabu kwao. Na Wahadimu ndio wakao pwani ya pili, nao watu wazuri. Hatta assubui juma a tatu tukafunga vyombo kwenda zetu, tukafuatana na mwalimu hatta shambani kwake; akatupa madafu, tulipokwisha tukaagana naye kwa heshima na furaha.

Juma a tatu, June 8. tukafika kijiji karibu na Kiwengwa kiitwacho Pongwa, tulipofika tu watu wote wakakimbia

MSIMULIZI. 471

kwani hawajawaona Wazungu, tukaenda kuwarudisha, waliporudi wakatuletea madafu na vitumbua, tukaagana nao, tukafuatana na mtu mmoja kutuonyesha njia. Tukawa katika kuchomwa na mawe, na msitu mnene, tukaenda hatta tukapumzika msituni, tangu saa tatu hatta saa tano tukawa katika msitu, na msitu huo umejaa kima wakubwa kwa wadogo, Tulipokwisha msitu tukafika Uzi saa sita, tukafika Bweni saa thenashara kasorobo. Tukatoka tukaingia Dunga, tukapewa mahali pa kulala, na tukaletewa kuku.

Na huko Dunga tukaona maanguko ya zamani walipokuwa wakipigana vita zamani watu wa Chuwini na wa Dunga. Hatta assubui nikajiwa na huyo Mwarabu, msimamizi wa shamba hili, akaniambia, "Mwambie Mzungu anipe kipande cha nguruwe kwa dawa," nikacheka kwa maneno yake na ginsi alivyonishika; hatta saa ya kwanza tukatoka kwenda Unguja.

Juma a nne June 9. tulipotoka Dunga tukafika mahali paitwayo Ndinjani, yapata nussu saa tukafika Tungwi, robo saa tukafika Cheju, tukataabika na mahali hapa kwa maji, na matope, hatta saa 7, tukawasili Unguja kuu. Tukapewa heshima, tukaletewa machungwa na Mafutaha. Saa kumi tukaenda zetu hatta Bungi tukalala katika nyumba ya Mwarabu, hatta alfajiri tukatoka kwenda Chukwani.

Juma a tano June 10. saa sita tukafika shamba moja liitwalo Kisayuni tukapumzika; hatta saa kenda tukatelemkia uwanda ulio karibu na Chukwani, hatta saa kumi unussu tukafika Chukwani. Tukawaambia Wazungu tusilale kwani mjini ni karibu aheri twende zetu mjini,

MSIMULIZI. 472

tukatoka Chukwani saa edashara kasorobo, tukafika hapa saa thenashara unussu, kwani twalikwenda kwa haraka. E.N.

HABARI ZA NEWALA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu. Baada ya salaamu, naona katika barua ya mwisho naliandika kama Bwana Askofu atawatia watu mikono, bassi Juma a pili ya pili baada ya Juma a pili ya Utatu ilifanyika. Nao waliotiwa mikono ndio watu asharini na saba, wangine majina yao yamo katika barua ya mwisho, ndio wa nje, nao wa Mission ndio hawa: Yakobo Jumbe, William Mpagweje, Lorenzo Sapila, Edward Lujenje, Yohana Songani, Yonathani Malesho, Petro Malesho, Lamberto Chirembwe, Austino Asmani.

Nayo Juma a pili hiyo ilikuwa furaha sana, na Juma a tatu yake Bwana Askofu akaanza safari yake. Alitoka asubui pamoja na Bwana Hainsworth na Mwalimu Daudi Machina, wakaenda kwa Chisanga wakarudi. Juma a nne na Juma a tano mimi nikasafiri kwenda kwenyi Station yangu, na siku ya Ijumaa, June 12, wakaja Madachi, wale waliokwenda Ng'omano, kuangalia makaa. Na Juma a tatu yake Bwana Watson akaenda Masasi, pamoja na Madachi wale.

Na Mwalimu Daudi Machina akasafiri siku ile ile kwenda kuanza kazi ya Ualimu. Nitawaarifu hadithi ya Jogoo. Jana, June 20, jioni saa tatu ya usiku jogoo akawika marra tatu. Bassi kwa huku, jogoo akiwika usiku washenzi husema ndio mwiko kabisa. Bassi akatokea Mzee Matola akauliza

MSIMULIZI. 473

kama amewika jogoo, watoto wakasema ndio. Naye Matola akaenda kwa Wazungu, akawauliza kama kwao, wakasema hatujaona. Bassi Mzee Matola akasema, maana yake jogoo kuwika usiku ndio kusema, "Vita inakuja, vita inakuja." Bassi usiku ilikuwa machafuko, watu wakaenda njiani kungojea vita, nayo vita isije.

Bassi hiyo inaitwa hadithi ya Jogoo. Na sababu ya kusema vile, Mzee, kama vita vita inakuja, kwani kwanza palitokea uthia wa kusema vita ya Magwangwara yaja, bassi uthia ule ukatulia. Bassi jana alipowika jogoo watu wakasema kama ule uthia wa kwanza unatokea tena. B.M.

HABARI ZA KIUNGANI.

Katika Mwezi wa July 22, Mwalimu John B. Mdoe aliwasili hapa, kwa matembezi kidogo ya siku kuu hatta katika July 31, akaenda zake tena Magila.

Katika Mwezi huo huo July 30, Mr. J. H. Bone aliwasili hapa pamoja na wazungu wengine, akitoka Magila, kwani alikuwa mgonjwa huko, bassi amerudi kupata afya kidogo. Hatta katika mwezi wa Aug 2, akafunga safari, amekwenda zake Ulaya, kuzidi kupata afya.

Katika Aug 5, Mr Roberts aliwasili hapa kutembea; hatta katika Aug 18, akarejea tena Magila. Katika mwezi huo huo Aug 3, mtoto mmoja wa hapa ameingia katika kazi ya upishi ndiye Edgar Mwambala.

Katika Aug 4, tumepata watoto wawili ndio hawa, Mayunga na Tambile.

MSIMULIZI. 474

Katika Aug 10, kisima chetu kimejengwa vizuri; siyo kama kilivyokuwa kwanza kwani sasa, kimetiwa vyuma viwili, virefu tangu upande mmoja hatta wa pili, na kati kati chuma cha kuvutia ndoo; na pande zake zote zimejengwa kwa mibao ya msaje imara sana.

Katika Aug 16, tulijiliwa na Kasisi mmoja aliyetoka Uganda, kwa muda ya miaka 9 alikaa huko. Naye alipokuja hapa kwetu, alitaka sana kutuelezea habari za huko, kwa kadiri ya miaka aliyokaa. Bassi siku hiyo ilikuwa Juma a pili jioni. Akaja kutuhubiria habari hizi Kanisani. Na killa mtu alipenda sana kusikiliza maneno yake, sote pia, tangu wazungu wetu wa hapa hatta sisi pia; tukawa killa mtu ameweka wazi masikio yake kusikiliza. Na habari alizotuhubiria ndizo:

Habari za Mtesa, ginsi alivyowatendea mabaya watu wa huko waliopenda Umasihiya. Tena habari za watu walioshika dini ya Kiislam, ginsi walivyofundisha watu yasiyo mema.

Akatuelezea tena ginsi wazungu walivyoenda huko na kuwafundisha watu hawa; akatuelezea habari za ufukuzo ulivyokuwa. Wengi kuuawa. Tena habari za kuondolewa kwake Mtesa katika Ufalme. Akatuelezea, kama palikuwa na watoto watatu wanne, waliokuwa hodari sana, hatta walikuwa wakifundisha wengine katika mafukuzo yao. Na hawa ndio walikuwa wakimpenda sana Kasisi huyu, na kumsayidia sana. Mwisho akatuambia:

"Ndugu zangu, mwajua mmetaka sana na mmepokea kwa furaha Anjili yake Bwana; bassi, mwe hodari sana kushika Anjili, wasiotikisika katika kuishika."

MSIMULIZI. 475

Katika Aug. 21, waalimu George J. Swedi, na Willie J. Swedi wamerudi tena kutoka Bonde.

Aug. 24, Siku kuu yetu ya Bartolomayo. Hatukuweza kufanya makusanyiko siku hiyo, kwani tulihitaji kutengeneza nyumba. Bassi ilikuwa kazi sana, kukata majani, na ginsi za mapambo pia. Hatta katika siku ya pili yake Aug. 25, Juma a nne, ilikuwa mkusanyiko hapa.

Katika siku kuu hii tulikuwa na mchezo wa kiaskari, kwani tulijifunza sana sana hatta tukajua mambo mengi. Siwezi kueleza mambo yote, illakini, katika mchezo huo, palikuwa ginsi mbali mbali za watu. Sultani alikuwa Mr Mallender, Admiral alikuwa Yakobo Chorola, Balyozi alikuwa Nicholas Kusi. Na palikuwa ginsi mbali mbali za majemadari (officers) na killa mtu kwa kadiri yake, tulicheza kama tuwezavyo. Na mchezo huu ulikuwa tangu saa saba hatta saa kenda unussu; hatta ilipokuwa jioni, Mabaharia wa H. M. S. Conquest walikuja wakauchapa mdundo wao.

Na siku hii walikuwapo wageni wengi kidogo, Wazungu na watoto wa Mkunazini, na wa Mbweni pia. Hatta jioni killa mtu akarejea kwake.

Aug. 28, siku kuu ya Augstino. Ilikuwa mahali pake Aug. 27, bassi ilikuwa, apendaye kwenda Mwera. Na ilikuwa mvua sana huko, hatta walipokirudi, Bwana Mr. Weigall, alianguka akaumia mkono. Sasa hajambo. Na Wazungu wengine walikuwa wagonjwa kwa baridi ya mvua. Hatta watoto nussu pia.

Aug. 31, Filipino Taruka, Tomaso Asuadi, na Oswald Mswakolo wameenda kujifunza kazi mjini, na kukaa huko.

MSIMULIZI. 476

Aug. 27, mwalimu Samwil Chiponde, amerudi akitoka Newala pamoja nao Cecil Majula, Kolumba Mzigala, Klementi Mkajangwiya, Daniel Usufu, Petro H. Musa, Stefano Mteta, Karlo E. Lisomba, Augustino T. Chitenje, Bernado Y. Himili, Paolo Kazinde, Krusostomo Ksungani, Ndauka.

Aug. 26, Rev. H. W. Woodward, aliwasili kutoka Bonde.

Aug. 30, Chad Hamisi akatoka Mkunazini akaja kukaa hapa.

Katika mwezi wa Aug. 30, aliwasili hapa Archdeacon Maples, akitoka Ulaya; naye hakukaa sana. Marra katika Sep. 2, akafunga safari ya Nyasa, wakifuatana naye mwalimu Yohana Chanamila, Tito Kungurukutu, Leonard Mattiya Kangati. Tena pamoja nao watoto watatu ndio Martin Zanga, Gray Feruzi, wameenda kutenda kazi ya kupiga chapa, na Wilfred Zulangeti. Na tena Mwalimu Leonard Pesa, na mkewe Emma Pesa wamekwenda kukaa Newala.

Sep. 4, Mr. Allen amewasili hapa, kutoka Bonde naye asimamia kazi ya kujenga.

Sep. 8, Paolo Akilimali ameingia kazi ya kupiga chapa.

Sep. 14, Bwana Rev. H. H. Clarke amekwenda Ulaya.

Tena siku hiyo hiyo, jioni sisi tumehama katika Class Room ya kwanza tumeingia Class Room mpya, mahali palipokuwa kwanza mezani pa kulia, kwa sababu Class Room ya kwanza kunabomolewa, na kujengwa Class Room kubwa na nzuri. Hizi ndizo habari.

Tumepata habari katika Sep. 13, kama meli aliyoingia

MSIMULIZI. 477

Achdeacon Maples, baada ya kuwashusha Lindi, ilipokuwa ikiendelea mbele karibu na kufika Mozambique imezama. Vitu vimepotea, lakini watu wameokoka. Salama. Mtg.

HABARI ZA NYASA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Habari si nyingi. Tangu mwezi wa April 21 ilipokuja stima yetu, haikwenda tena wahadi June 8 ndipo ilipokwenda pande za chini, mpaka leo bado kurudi, lakini inadeheniwa, imepandishwa; na sasa tungali katika kuitazamia. Je! Akina bwana mliona nini kwenyi mwezi wa May 23. Sisi bwana washenzi wa huku barra twanena Eclipses. Je waungwana mwanenaje. Twalimwona mzee mwezi ameshikwa kabisaaaa hatta nussu shekh haonekani. Lakini mnajua habari za bin Adamu hutwaa mabati upate kuondoka, vilevile na huku. May 24 twalimwona mtu bwana akichungulia uani kwetu tulipomtupia macho twamwona analumenya bwana, tukasema ndiye tuliyemtaka huyu tukamwandama hatta tukamkamata Eeeee bwana, ati mchana mchana bwana wala siyo kusema saa a kumi na moja, la! Bassi tulipomkamata alipelekwa ng'ambo kwa mfalme akashikwa kwa siku kathawakatha.

May 26 watu wa hapa bandarini petu walitutia ghasia usiku, hatta wangine hawakupata usingizi, lakini mwenyi kula pono alilala, kwani usingizi wa pono ni mkuu: bassi watu hawa wa bandarini petu waligombana na watu wa mji mwingine uitwao Chinyanya kisiwa hiki hiki, bassi watu wa petu wakaenda kuwalalika

MSIMULIZI. 478

wenzao wakaa ng'ambo, nao walikuja usiku. Si shindo hilo tulilolisikia; nao watu wa humu kwa mawe loooo masalale si hivyo. Walipigana watu wa ng'ambo wakatwaa mateka, lakini ingawa wametwaa mateka, wamejeruhi sana, kwa ginsi wajomba wa Likoma walivyopasi kwa mawe. Na tangu siku hiyo bado hawajaja bwana.

June 3 S. S. Charles J. ilikwenda Bandawe kumtwaa Mr Frere. Twalifurahi kumwona tena Kasisi wetu, kwani siku zingine twalikuwa hohe hahe hatuna mbele hatuna nyuma.

June 6 Mwalimu So na mkewe walikuja kwa siku ya juma a pili.
June 3 Mwalimu Murphy na mkewe walikuja hapa kwa Juma a pili.

June 14 Alfajiri twalipatikana na huzuni. Mtoto yule mdogo wa Nicholas Mkwarasho aitwaye Caroline amelala. Aliugua kifua kwa siku kathawakatha, lakini siku hiyo ndipo ulipomzidia wala wazee wake na yaya wake hawakulala usingizi, ikawa kazi ya kumtazamia mtoto saa yake ya mwisho. Alfajiri mapema akatoa Roho, akazikwa Juma a pili.

July 2 S. S. Domira imefika hapa imechukua matofali, kesho itatoka, tena imepeleka barua. Kwani mtumishi wetu yuko Matope bado hajaja. July 4 Mwalimu Murphy na mkewe walikuja hapa kwa Juma a pili. July 4 S. S. Domira ilienda ng'ambo pamoja na Mr Frere, kunena juu ya watu wale wa bandarini petu kwani walikamatwa mateka usiku ule walituamsha usingizini.

MSIMULIZI. 479

Bassi ilipofika huko ilipiga mizinga na iliporudi ilipiga mizinga. July 5 Juma a pili wazungu walioenda kwa Chikuse wametupasha habari kidogo. Mzungu mmoja ametoka kwa Wangoni, alihubiri kingoni, na mtu mmoja wa hapa alifasiri. Tena huyu mwingine ndiyo sasa anakuja huku pande za barra, yeye alihubiri kingreza, Mr Frere alifasiri. Albert yule mwalimu aliyetupasha habari za ndugu, amekuja, lakini hawezi, wala hakuweza kueleza habari za upande wa pili. C.K.

HABARI ZA MAGILA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi, salaam. Baada ya salaam nakuarifu habari kidogo tu. Katika July 26, Sister Elizabeth na Bibi Boden walituacha wakienda zao Unguja, wameitwa na Bwana Askofu kwenda Newala. Safari hii ya kushuka Unguja ilikuwa kubwa, kwani Bwana Bone aenda zake (maskini hatuna School Master) kwa ule ugonjwa wake, Bwana Roberts, Mganga wetu Henriques, hawa waenda matembezi ya Unguja, nao hawa walipitia njia ya Tanga kukuta Steamer.

Katika July 27, ikawa harusi ya Fabiano Bwambwala fundi wa sermala, na Neema Mwasbiti.

Katika Aug. 3, Salome Machaku alipata mtoto mke.

Katika Aug. 8, wote tulianza kuja hapa, matembezi ya juma tatu! naam! yamefayidika.

Na katika Aug. 16, tulifanya siku kuu ya mavuno. Juma a mosi tukalipamba vizuri sana; jioni akabatizwa mtoto wa Mwalimu Ackworth Machaku, jina lake Hilda Mary. Bassi Juma a pili katika sala ya pili,

MSIMULIZI. 480

sadaka nyingi sana, hatta hapana mahali pa kutia mihindi, mpunga, mtama, vingi sana. Na Juma a tatu ikawa karamu kwa watoto wote wa vyuoni, wengi sana waliokuja, tuliwafanyia sala kanisani na mahubiri kidogo.

Katika Aug. 15, Padre Woodward alituacha akienda zake Ulaya. Kwani alipoenda Kologwe alipatwa na ugonjwa uliompeleka Ulaya zamani, bassi akaletwa hapa upesi. Alifunga vitu vyake siku moja akatuaga kwa kusikitika sana, akitumaini akifika Unguja labda atakuwa hajambo, bassi atarudi tena? Twatumaini hapo Unguja hataenda Ulaya, illa ataturudia,

Katika Aug. 25, Waimbaji wote walienda kusayidia Mkuzi kufungua kanisa. Mimi nalitoka siku ya pili yake pamoja na watoto wote, assubui sana, tukafikia sala ya pili. Tukarudi Ijumaa jioni, tulimkuta bwana Roberts akitoka Unguja, pamoja na mtoto wa hapa, Maurice Gari.

Katika Aug. 29, akatuwasilia waalimu Karlo Mwaimu na Basil Mhada, wanakuja kutembea kwa mwezi watarudi tena.

Jee Mtengenezaji wa Msimulizi, u hali gani? Lakini umeona yule "Maongezi na Maarifa"? Na sisi twainuka somo, haifai baba "Msimulizi" na mtoto "Mtenga watu" watembee peke yao, sharti wawe na karani, na karani huyo inamfaa avae vizuri kupita bwana na yule mtoto wake wasipate kumtharau. Chapa yetu yaendelea bwana hatta inatupa Maongezi na Maarifa, ebu yasomeni, mtayatambua. J.B.M.

MSIMULIZI. 481

HABARI ZA MKUZI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Na baada ya salaam, nakuarifu habari za hapa petu. July 18, mwalimu John B. Mdoe alifika hapa kwenda Unguja kutembea.

Tena panapo July 20, tulianza kuwatazamia watoto kusoma; aliye wa kwanza katika darasa ya kwanza ndiye Herbert J. Sehiza, wa pili Lukindo. Na darasa ya pili: 1 Sayidi, 2 Sezua. Tena siku hiyo hiyo walipita Wadachi wawili wanaenda Pangani.

Na July 22, ndio watoto wote waliona furaha nyingi sana, hatta usiku hawakulala kwa furaha, kwani ndio siku tuliyopewa ruksa kwenda kwetu; na siku kuu hii tulipewa ruksa mbele ya siku kuu yenyewe. Naswi tulipata juma tatu unussu.

Hatta Aug. 15, walirudi watoto, na mimi nalirudi Aug. 17, kwa sababu nalishikwa na homa kidogo huko Misozwe. Tukaanza school Aug. 18, na ndio siku waalimu George J. Swedi, na William J. Swedi waliposhukia Pangani kwenda zao Unguja, pamoja na baba yao Rev. John Swedi kuwasindikiza hatta Pangani. Na Juma a tano alirudi baba yao. Aug. 22, Rev. J. Haines ameenda Magila kwa afya yake, kwani hana afya vema.

Siku kuu ya Bartolomayo amefika Mr. C. W. Roberts pamoja na M. Gari wakitoka Unguja, nao wamekwenda Magila.

Aug. 26, walikuja mabwana wa Magila pamoja na watoto wao nussu, tayari kwa siku kuu yetu ya kufungua kanisa letu jipya. Hatta Alhamisi yake Aug. 27, assubui

MSIMULIZI. 482

Rev. G. Dale alivalia pamoja ua waimbaji, tukazunguka ndani ya kanisa lenyewe na kuimba. Tena ukatolewa Usharika Mt. na Rev. John Swedi alihubiri. Tulipotoka tukikaa hatta panapo saa 3, mwalimu John Mdoe na watoto wangine walikuja: na saa nne ikawa sala ya asubui, na kanisa lilijaa watu wengi sana, na bwana Mr. Dale alihubiri. Hatta Jumaa watoto wa Magila walienda zao. Na siku hiyo hiyo jioni, walifika waalimu wawili Basil Mhada na Karlo Mwaimu waliokuja kutembea na kuangalia jamaa zao kwa mwezi.

Aug. 29, alifika hapa fundi Heath na H. Chechande wakitoka Magila kwenda Unguja. Hatta Juma a tatu Aug. 31, Mr. H. Allen na fundi Heath na H. Chechande wametelemkia Pangani kwenda Unguja.

Sept. 5, tulipamba kanisa letu tayari kwa siku kuu ya mavuno. Hatta asubui ndio Juma a pili, ndio siku kuu yenyewe, watu walileta mavuno ya mashamba yao kama wawezavyo, na kanisa lalijaa watu sana. Hatta panapo saa sita akawasili hapa Dachii mmoja kutoka Lewa, na alasiri akaenda zake kulala Umba tayari kwenda Tanga Juma a tatu. Hatta jioni akaja mwingine, huyu alikuwa na homa, akalala hapa, na Juma a tatu akamfuata mwenziwe Umba. Tena ndio siku tulipofanya siku kuu kwa watu wote wajao kanisani; ng'ombe aliuawa, watu walipokwisha kula, kama saa kenda wote tukashukia penyi kiwanja chetu cha mpila kufanya michezo. Watoto waume kupiga mbio, na wa kike tumefanya hivi: kati kati tumeweka sanduku, na upande huu tukatia ndimu sita mbali mbali, na upande huu vile vile; bassi upande huu husimama mwanamke mmoja

MSIMULIZI. 483

na upande huu vile vile; nao hushindana kuokota zile ndimu na kutia ndani ya sanduku, atakayeisha kwanza ndiye aliyeshinda, naye hupata zawadi. Watu walijaa sana, nao walifurahiwa sana.

Sept. 10, yule Mdachi aliyepita kwanza kwenda Tanga, amerudi tena kwenda kwao Lewa, na bwana Mr. G. Dale amekwenda Magila, na atapita kwenda Umba kuwafanyia siku kuu huko ya mavuno. Twatumaini ataturudia Juma a tatu hii ijayo. Salaam. H. J. S.

HABARI ZA MISOZWE.

Kwa Mtengenezaji wa Msumulizi salaam. Na baada ya salaam, nakuarifu habari zetu chache tu na thaifu.

July 12, ndio siku ya Juma a pili, siku ile naliona watu wengi kuliko siku zo zote nilizokaa Misozwe, watu ndio walikuwa kama 200 waliokuja kanisa kwa sala yetu. Watu wa miji iliozunguka mlima wa Mlinga, kwani wameona amani kwetu kwa Wadachi wanaopita na wapagazi wao wanavyoharibu inchi ya Bonde na mashamba ya Zigua. Pia nikawaonya vile si vema wajiila kwa fayida yao ya rohoni tu.

July 14, siku ya Gulio Kisinga, nikirudi nikakuta mtoto aliyekimbia kutoka kwa jumbe Makange. Nikamwuliza habari, akasema, nimethulumiwa, bassi ndio kuja kwangu, nikaenda kwa Makange, nikauliza nisione hatta neno, illa yeye ni mtoto mkaidi tu, asiyependa kutumika, bassi nikampeleka kwao kwa Mkange.

July 19, siku ya mvua sana siku ile, wala watu wengi hawakuweza kuja kanisani.

MSIMULIZI. 484

July 20, Juma a tatu akaja Mr. Allen na Mr. Ford; Mr. Allen kajia kutazamia kazi ya jengo badala ya Mr. Brough.

July 21, Wabondei wanafanya shauri kwenda kwa liwali Abdallah kwani waliitwa kwenda kwake. July 26, siku ya Juma a tatu athuuri, akaja mtu anayeitwa Kakucha, akaniambia, "Mwalimu, hatarini uko wewe," nikamwuliza akasema, "Njoo uone." Pana mawe mengi yalioitiwa kwa pakuingilia pa maji, chungu kubwa sana. Kumbe ndani yake mna nyoka kubwa sana kitwa chake chekundu kabisa, tukatia moto kwa shidda sana tumepata kumwua.

August 3, akaja Sister Anne Margaret na Sister Dorothea kwa kubadili hewa, usiku ule ule akaja simba karibu ya mlima wetu, akakamata nguruwe watatu, akala moja, akaacha wawili.

August 4, Wadigo walikuja Bwembwera kwa Mwaiimba kutaka Wabondei waende wawasayidie vita yao na Wadachi, kwani Wadigo wameasi kwa Wadachi. Nami nikipata habari nikaenda Rangaiya ndio mji ilipo bandera ya ufalme nikawauliza habari wakaniambia yote, nikawauliza shauri. Wakasema hatujui tufanyeje. Nikawaonya wasifuate shauri hilo la Wadigo, kwani wakienda kupigana na Wadachi adui zao wote walionyamazishwa na nguvu ya Wadachi wakisikia watafurahiwa watataabika kupita kwanza. Nikafurahi kuona wamesikia vema. Hatta assubuhi wakaondoka kwa Mwaiimba wakawaambia wadogo "Sisi hatutaki, kwenda vitani na nyinyi juu ya Wadoicha kwa sababu mbili.

(a). Zamani nyingi mkapigana na sisi kwa miaka

MSIMULIZI. 485

minane tangu 1880 hatta 1888. Ndio inayoitwa kondo ya Kivindo, na alipokuja mtu huyu Mdachi akatupatanisha sisi nanyi; leo hivi tuende kwa vita nanyi; sio hatuendi, bassi.

(b). Sababu nyinyi Waungwana na Waswahili nao husema tutapiga Mzungu yo yote; nasi tuna Waingereza watu wa zamani waliozoelea na sisi, na waalimu pia inchi yetu imejaa elimu "Ilh Masihi" Kimasihiya wala hatutoi hatta pesa moja kuwalipa waalimu hawa. Bassi kwa sababu hizi mbili hatuendi wala hatutapigana na Wadachi.

August 8, usiku nina mtoto Ambrosi Omari, na wote twatazamia kasisi kuja kwetu. Yule mtoto akaona kama taa njia itokayo Magila, akataka kwenda athani labda kasisi yuaja, ila akasema nitaenda uliza ruksa kwa mwalimu. Akaja, nikamwambia usipoangalia utaliwa. Marra tukiwa tunanena vile asikia lio la simba pale pale alipoona kama taa.

August 10, Sembando mzee wa mji wa Misozwe kafariki. Ndiye aliyeukaribisha upelekwa huu.

August 20, kanisa letu limeanza kutiwa mabahati.

August 27, nalishuka kwenda Tanga nitafute vifao; pana njia tatu za Digo za kufika Tanga, bassi njia mbili zilizo karibu tukazuiliwa nao, sababu wale Wadigo wamekasirika na Wabondei, sababu wamekataa kuwasayidia vita yao. Bassi tukapita njia ya mbali kidogo, ndio kama mayili 30 ao zayidi.

September 6, Juma a pili ya mavuno kwa upande wetu huu, watu watano wamepokea misalaba ndio hao Tupa, Lupatu, Mlangwa, Mbalazi, Mtekwa mtoto

MSIMULIZI. 486

wa kike wa school. Watu wengi walioleta malimbuko yao. Juma a tatu, karamu kwa watu wote, 84 jumla yao Wamasihya na Waanafunzi na wasikiaio ndio habari yetu chache na thaifu. M.F.

HABARI ZA SHAMBA LA MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu, nitakuarifu habari zetu za hapa ndugu. Mwezi huu wa June, ametuwasilia hapa ndugu yetu Cyril Swedi, aliyesafiri Kilimanjaro. Tena huku kwetu tumefiwa na ndugu yetu Persis Akaunguwa. Bassi siku aliyooa Bwana Key, Mr Clarke alitoa kondoo wanne kuchinjwa kwa furaha yake; bassi nyama ikagawiwa kwa killa mtu kidogo. Siku kuu ya Yakobo Mtume, ilikuwa karamu ya waimbaji wote waanaume, tulikusanyika Miembeni, na karamu yetu ilitawi sana.

Siku kuu ya Bartolomayo ilitawi sana hapa petu. Siku ya juma a tatu zilikuwa ngoma sana, hatta kwa alasiri zikavunjwa. Hatta Juma a nne tulisumbuka sana kwenda Kiungani, kwani lilikuwa wingu la nguvu sana, mvua ikanya, halafu ikanyamaza. Bassi tukakaribishwa vema. Tukakaa, hatta kwa alasiri, ilikuwa kwa zamu ya Kwata la nguvu, na machezo ya farasi kwa gurudumu, na ilipokwisha hiyo Merikebu moja ikaleta wapiga ngoma na filimbi, nayo yote tukayatazama; Halafu tukarudi. Mwezi wa September 2, mke wa Basil Kamna amepata mtoto mke, alibatizwa, akaitwa Lucy Durham.

Tena tuna huzuni sana kwa siku hizi, kwani mwizi amekuja usiku akaja akabomoa dirisha la Kanisa kubwa akaiba Msalaba wetu. Bassi hatujui amekwenda kuufanyiaje. N. F.

MSIMULIZI. 487

N'KOLOGWE.

LUVU. UZIGUA. August 3. 1891.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam.

Baada ya siku chache za kuwa hapa peke yangu, kwa jengo la nyumba ya kwanza ya kufungua mji,

July 28, Bwana Herbert Lister akaturudia kutoka Magila, baada ya homa yake, pamoja na mwalimu Cyprian Lizani aliyekuja tembea kwa siku kuu, pamoja na Andrew Lukindo, Yakobo Chamdangwe, na mwalimu Wilfred Madudu na mkewe, na Koka. Tumefurahi mno kuwaona tena sababu twalipooza sana hapa mimi na watu 4 vibarua, wafanyao kazi na kunisayidia kungoja mji wetu mpya, watu wa Magila.

July 30, mimi na Cyprian Lizani twalikwenda mji mmoja uitwao Zavuza, kumwamkia Liwali wa huku, aitwaye Vulu, alitukaribisha vizuri naye siku ya pili yake akaja mwenyewe kumwamkia Mr. Herbert Lister.

Aug. 2, twalikwenda Zavuza pamoja na Bwana Herbert na Wilfred kuangalia mji, na kuwaamkia watu. Walitukaribisha kwa heshima na furaha, walionyesha tofauti ya sisi na Wadachi kuwa mbali mbali, kwani aingiapo Dachi na watu wake, watu wakimbia na kujificha, illa tulipoingia sisi walifahamu kama tu mbali nao kwa hali zetu. Tukawaarifu sababu ya kuja huku na kujenga, ni kuja kufundisha watoto na watu wazima wote mambo ya Muungu na elimu. Na Liwali akatukaribisha vizuri sana, jioni tukarejea kwetu. Usiku wa leo kama saa sita unussu usiku wa manane,

MSIMULIZI. 488

kuku akaruka akilia tukiamka tahamaki ni mnyama aja kamata kuku. Tulipotoka nje marra Andrew Lukindo na Cyprian walipoona majani yalizwa na kukimbia kwake, walibahatisha tu (kwani usiku wa giza,) wakapiga mishindo sita; tulipokwisha twaona watu wa mjini Kologwe wamejifunga na bunduki zao, &c. wanakuja upesi kutazama nini lililotupata? naswi tukawaeleza habari zetu na wakaenda zao.

Thani yao walithani vita ya Wamasai labda kama walivyozoea kuja nyang'anya ng'ombe zao. Tukulala hatta assubui, tulipoamka tukatafuta, tukamwona kuku aliyemkamata hakudiriki kumla, amemwua tu, ginsi naswi tulivyomdiriki marra moja kumpiga kwa kubahatisha kwetu. Tukafuata damu yake illa hatukumwona nyama alikofia ao kujuruhiwa tu hatujui.

Aug. 4, Padre Woodward na Edwardes wamekuja huku kwa siku chache, na mtoto wa Magila William Chala, na wapagazi. Na siku ya pili yake Mwalimu Henry Nasibu alikwenda Bonde kwa siku chache kutazama jamaa Mkuzi.

Aug 7, Bwana Edwardes alitoka Kologwe kwenda Magila pamoja na Mwalimu Cyprian Lizani. Na Padre Woodward akakaa juma a tatu huku kuandika Kizigua.

Aug. 14, Mwalimu Henry alirudi tena Kologwe, na Padre Woodward na Mr Lister akawakuta wote wawili wagonjwa.

Na Aug. 18 Padre Woodward alikwenda Magila, makusudi apate safari ya kwenda Unguja na labda Ulaya na kwa sababu ya ugonjwa na hana afya sana. Na sasa twajenga nyumba kubwa ya udongo kwa Wazungu.

MSIMULIZI. 489

Ungeshangaa kuona ginsi Wazigua wanavyostaajabia jengo la nyumba hii, husema mwajengaje jumba kama hili na ikawa wangine wafanyao kazi watu wao.

Aug. 22, Tumefunga safari Mr. Lister na mimi na Wilfred Madudu na mkewe, na Ibrahimu Tupa, na Yakobo Chamdangwe, na mpagazi mmoja kwenda miji iliyo mbali mbele kwa kaskazini; kuitazama na kuamkia tupate kujijulisha kwao. Tukaendelea hatta mji wa Kwa Bogo, watu wakatukimbia illi tukawaambia wasitukimbie, na watu waliotujua wakatukaribisha vizuri, na wangine wakawapa moyo wakarudi, walipojua kama ni mzungu Mwingereza akaaye hapa Kologwe. Pale mimi hashikwa na mshipa wa mguu nisiweze kwendelea mbele ikanipasa kurudi mjini tena; wao wakaendelea mpaka kwa Sigi hatta Maulwi, (ulio mji mkubwa kama Kologwe) pale wakalala.

Assubui ya leo kama saa tatu wakarudi. Wakituletea habari njema, kama watu wanakubali kabisa kuacha watoto wao kufundishwa kusoma. Illa wangine waliogopa sana, wasema ni zile safari zinazopita siku zote kutunyang'anya vitu vyetu kwa nguvu, illa mwisho wakaona sivyo kama walivyothani. Tangu hapa hatta huko ni kama mwendo wa saa 2; sasa tumepata mtoto mmoja aitwa Nyange mtoto wa liwali Vulu wa mji wa Zavuza, ulio karibu na hapa, akaa naswi mtoto huyu kwa kuuguzwa kifua, na tena afundishwa kidogo kidogo. A B Ch.

Aug. 19, James Kiwayo mpishi kaja kufanya kazi hapa ya kupika pamoja na Msiagi kuwa chini yake afundishwe.

MSIMULIZI. 490

Aug. 26, Safari ya wapagazi wa Dachi imekuja karibu na Kologwe, mtu mmoja amenyang'anywa kuku nyumbani mwa Mzigua; wenyewe wakaja kushtaki kwetu, tuliona afathali tushuke kuangalia uthia huu, mimi na Bwana Lister kwenda kutengeneza maneno, tulipofika mwalimu Wilfred Madudu ameyaisha, akatolewa yule kuku akapewa mwenyewe. Na ndipo alipokuja jumbe wa Maulwi kutuamkia hapa petu.

Aug. 27, wazee wa Kologwe wamekuja hapa kupatana habari ya watoto kusomeshwa. Na Mwalimu Wilfred Madudu ameanza kusomesha Zavuza A. B. Ch. Aug. 28, Padre H. Edwardes amekuja hapa, siku ya Ijumaa aenda zake Magila, pamoja na Mr. Roberts aliyekuja kwa siku chache alikuja hapa, Aug. 21.

Aug. 30, Juma a pili, twalifanyiwa "Siri Takatifu" hapa na Padre H. Edwardes; tena sala ya pili, na hubiri saa ya nne, na jioni tukaenda kuhubiri mjini ndio marra ya kwanza, na watu wengi walikusanyika. Mahubiri yakawa juu ya kuvunja amri ya Muungu na kuumbwa ulimwengu na kukosa kwa Adamu na Hawa.

Aug. 31, Padre H. Edwardes, na Mr. Lister, na mimi twalikwenda Maulwi kuuliza habari ya uaji uliofanyika huko ya watoto wawili. Habari ni hii tulivyobashiriwa: Huko kwa mji wa kwa Sigi pana mji mdogo uitwao Mzingi, yuko mtu aitwa Mlaguzi huyu alikuwa na mtumwa zamani akanwoza mke akapata waana wawili wa kiume, halafu mkewe akafariki. Yule mtumwa akatoka pale pa bwana wake, akaenda pamoja na waanawe inchi ya Zigua, akafika kwa mtu aitwa Kilo mwana wa jumbe Sedenga. Hapa akataka mke, akapewa,

MSIMULIZI. 491

akakaa, Baadaye akaona afathali watoto wale awapeleke huku kwao kwa bwanawe, akawaleta. Yule Kilo akiona vile akakasirika, akamwambia, "Kwani wewe umekuja nimekupa mke umeoa, tena ukapeleka waanao huko ulikotoka." Yule Kidugwe akasema "Si wangu peke yangu ni pamoja na bwana wangu." Naye Kilo akasema "Kawalete niwakomboeni wote nyie kwa ng'ombe tano, sita, ao saba," akamwambia "Mimi sina neno nenda kwa bwana wangu ukapatane naye."

Yule Vulo akapeleka watu 4 huko kwa Mlaguzi kwa habari ile waliyokujia wakasemana naye, naye akasema, "Kama ataka watumwa hawa na alete ng'ombe zangu hapa nitatoa." Pale wakasemana mengi ya ugomvi wawatwae kwa nguvu, wasipatane.

Wakashika njia wakaenda zao; walipokienda mbele, wakafika karibu na ulalo wa mji Mauluri wakakuta vijana wawili watokao shamba; wakamchoma mmoja mkuke, na mmoja wakampiga kwa bunduki wakafa, wote wawili.

Mjini kule akatoka mtu ni baba ya mtoto mmoja aliyeuawa, wale wakakimbia. Mmoja aliyeua akaona watu watoka mji wa Kwa Sige wakaao inchi ile ile watokapo watu walioua vijana. Marra akatoa kisu akampiga tharuba tatu akaanguka mtoni akafa. Tukaeleza hivi na watu wa mji; nao wamejifunga tayari kutoka kwenda kupigana na huyo Kilo na babaye Sedenga.

Lakini Padre akawaambia, "Fanyeni maneno kwanza wajulikane watu hao." Tena akawaambia juu ya "Amri

MSIMULIZI. 492

ya Muungu" kama kulipa kisasi si kwema waende shariani wakapate hukumu kama kwa Dachini pia.

Tukaisha tukarudi kwetu, mvua ilitupiga njiani kwenda na kurudi. Sasa ni wakati wa mavuno, inchi hii watu wakata mtama. Na Mr Roberts amekuja hapa na Hiza na wapagazi wawili. Sep. 1, wamekuja askari watatu wa Dachini mmoja akawatisha watu sana aitwa Abdallah Turki naye alikaa sana Magila. Akiuguliwa akafanya uthia sana, naye alilewa sana. Uthia ukatengenezwa na Padre Edwardes. Na ameambiwa atashtakiwa Tanga kwa uthia huu.

Sept. 2, Mr Lister na Roberts wamekwenda Mauwi waliporudi kwa jioni, na Mr. Edwardes hawezi. Salaam. H. N.

Duniani hapana furaha walla huzuni siku zote. Ndugu habari kidogo za furaha na huzuni. Furaha kusikia kama Bwana Askofu amefika salama Nyasa, lakini alichoka sana kwa taabu za njia: ni furaha mno naona kwa ndugu zetu walioko huko.

Twatumaini atarudi njia ya mto Zambezi na kutufikia December.

Tena ni huzuni ya kuwa Captain Sheriff amefariki. Ugonjwa ulimwanza katika Stima Aug. 2, asilale lakini, illa panapo Aug. 10, ulimzidia, na alipelekwa nyumbani, asiweze kula kwa siku mbili alipolala ndipo. Na Bwana Askofu na Mr. Johnson walikuwa tayari kumpeleka Bandawe kwa Dr. Lawes, illa kwa usiku akaugua sana, na panapo saa 12 asubui alitoa roho. Aliugua Aug. 9 hatta 12 akafa. Alikuwa mvuvi kwanza Ulaya, akasikia habari ya Mission kwa Bwana Johnson, akaviacha vyote akamfuata. Sasa ameweka uzima wake kwa ajili yetu. Upendo gani kupita huo! ya mtu kutoa maisha yake kwa ajili ya rafiki zake.

Amejaribu kutenda kazi zake awezavyo illa sasa astarehe. R.I.P. Mtg.

HABARI ZANGU.

Ah! Rafiki, nimesikia habari kubwa ya Unguja leo. Na mimi najivuna kidogo. Kunrathi sana. Sikilizeni tu. Mimi hapa Msimulizi wa Mission nimetokea ulimwenguni yapata miaka mitatu na zayidi. Kumbe sasa

Wazungu wa mjini wasema, Tazameni, jamaa! Msimulizi kitu kizuri sana. Tuwe naswi na wetu sawa sawa, tupate kujuana habari killa mahali. Bassi Wazungu wakubwa wameniiga mimi niliye mdogo. Wanapiga chapa Msimulizi wao, wamentaja Gazette, mwenyi habari za amri za mabalyozi na matengenezo ya mji na maneno ya serkali na matembezi ya bithaa, na mambo mengi, tena. Haya! Tazama hao kama watoto wangu, yule wa Likoma wa kwanza, yule wa Magila wa pili, huyu wa Unguja wa tatu. Bassi nisijivune kidogo kwa haki? Hatta kuishi mimi tena ao nife, mamoja. Mzee mimi, nimezaa watoto, bassi. Lakini bado kwanza kazi yangu haijaisha. Huyo Gazette mtoto mzuri sana na mkubwa. Hana sanamu lakini. Na bei yake pesa nne. Yataka kutokea killa Juma a tano. Haya! Nitaokota mimi habari kidogo zilizomo, nitawaarifu ninyi, rafiki. Nisimtegeme mtoto kidogo? Atanisayidia sana.

Hatta sasa nimekota kidogo hivi. Tangu Feb. 1st Unguja umekuwa "Free Port," — maana yake, hapana kabisa kulipa forthoni kodi wala ushuru wa kushusha shehena ya vitu vyo vyote ama kupakia. Haikosi matajiri watafayidi, sijui maskini. Tutajua halafu. Haya! Pandeni, vuneni, leteni, uzeni, mtaona. Nafaka, ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku, mayayi, mtama, mchele, — Unguja hula vyote, kwani mkubwa, watu wengi, na pesa zipo. Msimulizi.

>>> Pages 493-509 missing!